المذهب والوطن / السواحلية

# MADHEHEBU NA NCHI

## MAHOJIANO NA MJADALA WAZI KATI YA SHEIKH HASSAN SAFFAR NA USTADH ABDUL - AZIZ QASIM

(Ushia duniani na nchini Saudia)



SHEIKH HASSAN MUSA SAFFAR

© Sheikh Hassan M. Saffar

Kimechapichwa na:

Sh. Hassan Musa Saffar
P.O. Box 1322
Qatif 31911

Tel: + 9663855521

Fax: + 966385126

Website: www.saffar.org
Email: office@saffar.org
Saudi Arabia

Kimefasiriwa na:

Ustadh K. Kea
Mombasa
Kenya

Mhariri:

A. Mohamed
2007 A.D.

# MADHEHEBU
# NA
# NCHI

Sheikh
Hasan Musa Saffar

## YALIYOMO


**MWANZO WA MAHOJIANO** ........................................... 1
Taqiyya .......................................................... 3
Wakati wa utoto .................................................. 5
Lakini wanavyuoni wa Sunni walikuwako wapi? ...................... 8
Kuishi pamoja .................................................... 13
Ni tofauti ya utaifa ama ni hofu tu isiyokuwapo .................. 17
Mji mmoja na utaratibu mmoja ..................................... 19
Kitabu *Al-Kafi* na daraja yake kwa mashia ....................... 24
Kipindi cha kujiunda kitaifa ..................................... 26
Najaf na kutafuta elimu .......................................... 31
Swali muhimu zaidi ............................................... 36
Ibnul Alqamy katika historia ..................................... 38
Msimamo wa Shia juu ya marekani .................................. 40
Najaf tena na hawza .............................................. 40
Pesa na uzito wa jamii kwa Marjaa ................................ 43
Hali ya Kuwait, je ni kutengana au kusaidiana? ................... 45
Imam Khomeini .................................................... 47
Hali ya mashia wa Lebanon ........................................ 50
Tofauti ya Sunni na Shia ......................................... 51
Bali ni Qur'an kamili ............................................ 59
Tatizo pekee na gumu ............................................. 59
Makhawariji au Maamawy? .......................................... 62
Lakini tutaanza vipi? ............................................ 69
Mifano ya Iraq na Lebanon ........................................ 76
Mvutano wa kijamii Kuwait ........................................ 81
Kutokea mema na kuona ukorofi .................................... 85
Kukutana muhimu kwa kihistoria ................................... 89
Kurudi Qatif ..................................................... 91

Mwamko wa Sunni na Shia..........................................94
Lakini msimamo wa watu wa kwenu ulikuwa vipi......96
Kazi ya marjaiyya (uongozi wa mujtahid) wa Shia..103
Madhehebu ya Jaa'fariyya, ni ya tano?..................106
Uzoefu wa maka mingi............................................117
Je Saffar ni Khomein wa Qatif?..............................118
Mandhari ya Ashura na picha yake isiyofaa............121

**YAFUATAYO NI MAHOJIANO KATI YA MWANACHUONI WA KISHIA WA SAUDI ARABIA, SHEIKH HASAN MUSA SAFFAR NA MWANDISHI WA GAZETI AL-RISALA, ABDUL-AZIZ KASSIM, LILILOTOLEWA TAREHE 1 OKTOBA 2004, NCHINI SAUDI ARABIA**

Mwandishi: Kwa kuanzia tunakushukuru kwa kukubali mwaliko wa kuwa mgeni wa heshima katika mahojiano na nakala ya '*Mukashafat*.'

Kwanza nigelipenda kuomba ruhusa ya wafuasi wako na wanafunzi wao ili nianze kukuuliza maswali yangu ya waziwazi.

Sheikh: Kwanza ningelienda kuwashukuru kwa ziara hii na pia kupata fursa hii ya kufanya mahojiano na kuweza kueleza wasomaji watukufu na wananchi walioko sehemu mbalimbali na wenye mielekeo tofauti, na hii ni hatua ya kwanza ya kuishi pamoja, kujuana na kusaidiana kwa ajili ya maslahi ya pamoja, kwetu na kwenye dini yetu.

Nawaahidi kuwa mazungumzo yangu yatakuwa huru kabisa, siamini kama kuna kitu cha kuficha. Ama kuhusu yapi ya kuchapishwa nyinyi ndio mnaojua cha kukichapisha na kukiacha.

Ama kuhusu mimi kuwa wazi ninapojibu hakuna kizuizi kinachonizuia kuwa hivyo au mtu kama mimi kufanya hivyo kwa maslahi ya umma, wakati huo huo kushikamana na adabu za kujadiliana na kuzungumza katika Uislamu.

Kulingana na wafuasi, naamini kwamba hali ya kidini au ya mashekhe na wanavyuoni wamejiweka katika nafasi ya juu no juu ya wafuasi wao inayowazuia wafuasi wao wengi wawe wazi au wathubutu kuzungumza nao, hii naona yahitaji iondolewe.

Mtume (s.a.w.w.) alipokuwa akizungumza na bedui mmoja aliyekwenda kumuona, yule bedui alikuwa akitetemeka, Mtume akamwambia: "Tulia, mimi ni mtoto wa mwanamke mmoja tu aliyekuwa akila nyama kavu Makka."

Kila mwanachuoni wa kidini anapokuwa mnyenyekevu kwa watu ndivyo anavyoweza kuwaingia zaidi ndani ya nyoyo zao, wao wanazidi kuathirika naye. Lakini sasa tunaishi katika katika enzi ambazo tunaona viongozi wakubwa na wanasiasa wenye uwezo na utawala lakini watu wanashindwa hata kuwapinga.

Na haifai kwa viongozi wa kidini wapende kuwa na utisho unaowafanya wasiwe wazi, lakini yote hii inatokana na jinsi watu wanavyoheshimu dini yao na kuwazingatia wao kuwa ni marejeo ya dini yao.

Na katika kikao hiki cha unyenyekevu ningelipenda kuchukua fursa hii kuwa hata wapinzani wa baadhi ya maoni yangu na wanaokubliana na rai zangu waseme kwa uwazi kabisa; huenda wakati mwingine kuna watakaohisi kuwa mfano kama huu hupatikani katika kikao changu lakini si kweli.

Kwa hivyo nakuahidi nitazungumza na kila nionaye kuwa ana kukereketwa, kwa sababu ni lazima tukubali uwazi kwa hiyo ndio nia inayofungua mafundo ya muda mrefu na nyeti.

## Taqiyya

Mwandishi: Mwanzo huu kwa kweli unatoa habari njema kwa sheikh, nami nimefurahi sana kwa roho hii ya uwazi, Kabla ya kuomba ruhusa yako (kicheko!).
Ni kweli kwamba ipo haja ya kuondoa daraja kubwa lililoko kati ya watu wetu, wanavyuoni wetu na wahubiri wao. Kabla ya kuanza kukuuliza, hebu niwe wazi na wewe, kwa sababu wasomaji wengi watayasarifu mazungumzo yako kuwa ya '*taqiyya*' kwa hivyo ningelipenda ufafanue juu ya maudhui haya.

Sheikh: Maudhui haya yamezungumzwa mara nyingi awali katika hafla nyingi yatuingiza kupekua juu ya mashia kuitumia '*taqiyya.*' Kwa bahati mbaya matokeo ya migongano ya kidini yanasababishwa na ya kimadhehebu.

*Taqiyya* si jambo la Shia tu, bali ni jambo liko katika Qur'an na katika Uislamu kwa ujumla, katika Aya nyingi za Qur'an tukufu imesisitizwa kwamba mwanaadamu anapokuwa katika mazingira anapohofia aisipatwe na madhara nafsini kwake, au mahali anapohisi maoni yake yatamletea matatizo basi ataitumia ili kujikinga maisha na maslahi yake.

Qur'an tukufu yasema: "Ila mtakapofanya hivyo (kwa ajili ya ) kuogopa shari zao: Pia yasema: "Ila yule mwenye kulazimishwa na hali moyo wake umetulia kwenye imani." Aya nyinine : "Akasema yule mtu mwenye imani akificha imani yake.." Ziko Aya zinazoonyesha Taqiyya kihujumla. Katika vitabu vya tafsiri twaona kila mwanachuoni kwenye Aya hizi hutaja ufahamu huu, hata katika Fiqh marejeo mbalimbali mafakihi wakifanya utafiti juu ya mambo hayo ya kulazimishwa.

Lakini Sheikh, hoja juu ya haya ni pale hali inapokuwa mbaya sana, lakini tumegundua ndugu zetu wa Shia wameifanya kama ndio msingi wa jamii yao.

Sheikh: Hali hii imesababishwa na mazingira wanayoishi, hapa sisi twataka tuzungumzie msingi wa *Taqiyya*, je hiyo iko katika Uislamu..wakati Shia wanapolaumiwa kwa kuitumia, na je haipo Uislamuni au hipo? Ama kuitumia sana hii yarudi kwa mtu anayeitumia na hali zake. Na wanavyuoni wote wanazungumzia juu ya kudhikika ni kuwa mtu mwenyewe ndiye atakayekisia kiasi cha ule uzito kama vile Uislamu unapomruhusu mtu akidhikika ale mzoga, kiasi cha dharura, Fiqh haikadirii bali ni mtu mwenyewe, na hili ndilo Shia walilolifanya wenyewe.

Kuna mjadala baina ya wanavyuoni, je *Taqiyya* yafaa kuifanya kwa dhalimu kafiri tu au hata dhalimu muislamu? Baadhi ya Sunni wanasema kuwa huenda ikafaa kwa dhalimu kafiri na kwamba Aya za *Taqiyya* mtiririko wake ni dhalimu kafiri.
Baadhi ya Sunni na Shia wote wanaona kuwa *Taqiyya* ni kwa kafiri na muislamu hali inapobidi hivyo, mfano madhehebu ya Shafii yanasema: Kunapokuwa matatizo kati ya waislamu na kafiri, hapo yafaa, kwa kulinda nafsi.

Imetajwa katika kitabu lilichotolewa Kuwait na Wizara ya mambo ya kiislamu Juz. 13, Uk. 196: "Watu wa Hambali wanaona haifai kuswali nyuma ya fasiki au mzushi isipokuwa Swala ya Ijumaa na Idi, inayoswaliwa mahali pamoja tu katika mji, akiogopa mtu kuswali nyuma yake basi ataswali Swala ya *Taqiyya*, kisha atairudia Swala yake tena..
Na Ibn Quddama ametaja kuwa mtu ataswali nyuma yake lakini atatia nia ya Swala ya peke yake."

Na wakati wanavyuoni walipokuwa Sunni wakati wa mtawala Maamun walipoambiwa waseme kuwa Qur'an imeumbwa, walitumia *Taqiyya*. Na upande mwingine Shia wanapoitafiti *Taqiyya* hufanya hivyo kwa misingi miwili: Kwanza kuondoa madhara ya mtu binafsi, na msingi wa pili ni kuondoa madhara kwa umma na umoja wa kiislamu.

## Wakati wa utoto

Sasa Tungelipenda tuzungumzie kuhusu kipindi chako cha utoto ulipokuwa mdogo. kuzaliwa kwako na kukulia katika jamii yako.

Nimezaliwa mjini Qatif mnamo mwaka 1958 (A.D.) – 1377(A.H.), katika familia isiyo na kipato lakini yenye dini, kwani baba yangu upande wa baba alikuwa mwanachuoni, pia babu yangu upande wa mama alikuwa ni khatibu, hata ammi zangu, ndugu na pia baba yangu alikuwa akijishughulisha na mambo ya dini ambaye alisoma misingi ya dini kidogo, kisha hali ya kimaisha ikambidi afanye kazi mbalimbali nyingine lakini alishughulika na mambo ya kidini.

Nikakuwa katika hali hii na katika mkoa wenye dini unaofanywa minasaba na tafrija za kishia, kama vile tuna siku za Ashura kila mwaka, siku kumi za mfungo nne ambapo huwa ni kama kipindi cha mazingira ya kidini kwa elimu ya jamii, kwa wanawake, wanaume, wadogo, wakubwa wote hushiriki, nayo ni kukumbuka masaibu ya kufa shahid kwa Imam Husein (a.s.) mjukuu wa Mtume (s.a.w.).

hapo hutajwa majanga yaliyowasibu Ahlu-bayt wa Mtume huko Karbala mwaka 61 (A.H.), na mwEzi wa Ramadhani pia huwa kuna majilisi na madarasa usiku ili kutoa waadhi, kuongoza watu, Kutaja sera ya Mtume (s.a.w.) na ya Ahlu-bayt wake, kutaja hukmu za sharia juu ya Swaumu, Swala, na mengineyo. Na kila Imam hutajwa na kukumbukwa, kulingana na historia ile siku aliyozaliwa na ile aliyokufa, hapo huja khatibu akazungumza juu ya Imam huyo.
Nilipokuwa mdogo nilikuwa nikienda na babangu katika majlisi hizi, nikapendelea nami nifuate njia hii, nikapenda nafasi ya kuhutubu, nakumbuka nilipokuwa darasa la nne nikiwa na umri wa miaka kumi, nilikuwa nikiwakusanya watoto wa eneo letu nikiwahutubia kama khatibu anavyohutubu.

**H**akika wasomaji wetu watajua kwa mara ya kwanza ufafanuzi wa madhehebu ya Shia, nakuuliza kama mwandishi, swali langu ni: Je ulihifadhi Qur'an ukiwa na miaka kumi?

**L**a, sikuhifadhi yote, bali nilikuwa nimejifundisha kuisoma yote na kuhifadhi baadhi yake, katika vyuo vilivyokuwa vingi hapo kwetu wakati huo. Vilikuwa vikifundisha kusoma Qur'an lakini si hatukuwa na madrasa za kuhifadhisha Qur'an.

Nilianza kuhutubia watoto wa rika langu mpaka watu wazima wakaanza kuhudhuria, wakagundua kuwa yale niyasemayo ni yale niliyoyasikia kutoka kwa wanavyuoni na makhatibu, wakawa wakiniita nihutubu, nami umri wangu wakati huo ni miaka kumi na miwili tu, nikihutubu kama makhatibu wengine mjini, watoto wenzangu wakanipa moyo sana, habari zikaenea huko

Ahsaa kwamba kuna mtoto anayehutubu, kusoma na kuhifadhi, nikaalikwa huko, kisha pia nikaalikwa sehemu zingine kama vile Bahrain na Kuwait, hii ndiyo iliyonipa moyo kujihusisha zaidi na masomo ya ilmu ya sharia baada ya kumaliza ilmu yangu ya msingi.

Sawa, baada ya haya ningelipenda ututajie baadhi ya waalimu na mashekhe zako uliovutiwa nao ulipokuwa mdogo.

**Sheikh:** Nilivutiwa sana na baadhi ya mashekhe wa kwetu-katika mbinu za kuhutubu kwangu- kama vile Sheikh Seyyid Hashim Seyyid Sharafud din (1323-1387 A.H.) kutoka mji wa Safwa. Pia Sheikh Khatibu Abdul - Haid Al-Marhuni, na Sheikh Said Abul-Makarim ambao bado wako hai, na makhatibu wengine, lakini hao watatu ndio walinivutia zaidi na saa nyingine nahifadhi wayasemayo na kuwahutubia watu wengine.na saa nyingine nahifadhi wayasemayo na kuwahutubia watu wengine.

Baada ya hapo nikaingia kwenye vitabu na kuelimika kwa dhati na kwa kuwa nilikuwa nikihutubia huko kulinifanya niwe karibu zaidi na wanavyuoni. Miongoni mwao ni Sheikh maarufu wa Qatif, Sheikh Faraj Al-Imran (1321-1398A.H.).

Huyu alikuwa mwanachuoni mkubwa na anayeheshimiwa mno na kuaminiwa na watu, nilikuwa naye kila siku hasa wakati wa mapumziko ya kipindi cha kiangazi, nilivutiwa naye sana hasa jinsi alivyokuwa akijibu maswali, na alijulikana kwa uwazi wake na kumbukumbu zake za kihistoria, na alikuwa na kitabu kilichotumiwa kama marejeo katika historia kiitwacho '*Al-Azharul arjiyya fil athaaril farjiyya'*.

Yeye alikuwa kiandika matukio ya kila siku, anayekutana naye, anayezungumza naye, anayemzuru, vitabu vyake, mashairi yake na majibu yake ya dini akisajili kila kitu, na akichapisha juzuu baada ya juzuu, hata alipofariki, idadi ya juzuu zake zilifikia kumi na tano.

Nilifurahishwa sana na kitabu hiki na kuikisoma kila siku na pengine zaidi ya mara moja, na hapo ndipo nilipowajua wanavyuoni wengine watajwapo, basi hujikuta nina hamu ya kujuana naye huyo aliyetajwa katika kitabu, hata niliposafiri kwenda Iraq na Iran kwenda kuwaona mashekhe waliotajwa na Sheikh kuwa aliwatembelea, nami nikawazuru kwa sababu majina yao yalikuako akilini mwangu.
Pia kulikuwa na masheikh wengine kama Sheikh Mirza Husein Al-Barki (1329-1395 A.H.). Lutfy Al-Manfluty, Abdalla Al-Ayayili, George Jardaq na George Zaydan na wengineo, na alikuwa akinukuu ibara kutoka kwa vitabu hivi, hilo likanifanya niwe na hamu ya kuvisoma.

Miongoni mwa niliopendezwa nao ni Sheikh Abdul-Hamid Al-Khatty (1331-1422 A.H.). Aliyekuwa kadhi wa mahakama ya nyakfu na mirathi wa Qatif, huyu alikuwa mwanachuoni, fasihi aliyekuwa akitoa darsa za Fiqh kila usiku katika msikiti wake baada ya Swala ya Maghribi na Isha, nilikuwa nikihudhuria kila siku na kufaidika sana. Pia nilivutiwa na Sheikh Ali Al-Marhuni, huyu alikuwa mwanachuoni, khatibu, na mnyenyekevu.

## Lakini wanavyuoni wa Sunni walikuwako wapi?

Naelewa jinsi ulivyoathirika na wanavyuoni wa kwenu, lakini je hukuvutiwa na wanavyuoni wa Sunni uliowasikiliza?

Wakati huo hakukuwa na uwazi (wa kujuana), kwa hivyo sikuweza kumjua mwanachuoni au khatibu yeyote wa Sunni.

**Mwandishi:** Je naweza kusema wazi hapa kwamba, kulingana na jibu lako, kuna fikra zilizoganda kwa jamii dhidi ya wengine, na kuwaona wengine kama mwiko kwao.

Ndio, mwanzo wa maisha yangu makuzi yangu yalikuwa yamezungukwa na mazingira ya kwetu Qatif ya Shia tu, sikuweza kuwajua wanavyuoni wa Sunni lakini nilivijua baadhi ya vitabu nilivyovisikia kutoka kwa masheikh wanapozungumzia vitabu hivyo hapo nilivisoma, na wanavyuoni wa Shia maktaba zao zimejaa vitabu vya Sunni kama Sheikh Faraj Al-Imran, na Sheikh Mirza Hasan Al-Bariki wana maktaba ambayo vitabu vya Sunni ni vingi kuliko vya Shia.

Nikawa navisoma, na wanavyuoni wetu wakitoa dalili kutoka humo, kwenye maoni ya tafsiri na ya Fiqh, lakini kwenye uhusiano wa kijamii hatukuwa na uhusiano wa kujuana na wanavyuoni wa nje ya madhehebu yetu.

**Mwandishi:** Je bado kuna kutokaribiana katika wakati wetu huu wa sasa tunaoishi na hasa mji wa Qatif?

Hivi sasa kuna uwazi kwa sababu ya kupanuka kwa mawasiliano, kutangamana kwenye vyuo vikuu na makazini, lakini katika jamii bado kidogo hakujafunguka kati ya pande mbili, na hivi sasa kunajitokeza picha nyingine, Shia wanajaribu kuwa karibu na upande mwingine, lakini upande wingine bado haujakuwa wazi.

Mimi binafsi nawatembelea masheikh wa kisunni na makadhi wa mahakama kuu wa Qatif lakini hadi sasa hatujafanikiwa kuwakinaisha hata mmoja wao kututembelea, ila ilitokea kadhi mmoja mwaka uliopita alikubali kumtembelea Sheikh Swaleh Darwesh, na kwenda kwake ni kwa ajili ya mazungumzo yahusuyo jamii ya Qatif.

Yaonekana Sheikh, matukio mengi ya kihistoria yanahitaji muda wa kuyatatua, hapo wenye akili watakapoweza kuyatatua.

Sisi, hivi sasa, tuko katika kipindi cha kuleleza hali, ama kuyachambua kuna maneno mengi mno.

**Mwandishi:** Sawa, hapana neno, hebu turudi kwenye kipidi chako cha kusoma, ni kama ulikuwa umeelekea upande wa kidini, je hukuinglia elimu nyingine kama za fasihi, mashairi na falsafa.

Kusoma kwangu wakati huo upande wa fasihi na fikra kulikuwa ni kidogo, nilisoma vitabu vya Taha Husein, Abass Mahmud Al-Uqqad na Manfluti, na hivi ni vya ni vya fasihi lakini vyagusa upande wa kidini. Nilikuwa nikisoma kile kinachohusu dini wakati huo wa mwanzo mwanzo.

Je kulikuwa na mtu aliyekuwa akimuongoza, akimlea kielimu na kufuatilia anachokisoma mtoto Hasan Saffar wakati huo?

**Sheikh:** Mambo hayakuwa hivyo wakati huo, bali ni mapenzi ya mtu na bidii yake, hakukuwa na mwanachuoni aliyetilia umuhimu kukusanya wanafunzi

Na wafuasi na kuwalea, wanavyuoni wengi niliojuana nao walikuwa kwenye kiwango cha kijamii kwa ujumla, wakihutubu kenye kadamnasi ya watu, pengine kulikuwa na baadhi yao wenye wanafunzi waliokuwa wakisoma kwao masomo ya dini lakini kwa kikomo chake tu, na kulikuwa na baadhi ya wanavyuoni kwenye majlisi zao wakikuza ilimu kwa kiasi kidogo tu.

Harakati za kielimu wakati huo Qatif zilikuwa dhaifu, idadi ya wanavyuoni na wanafunzi huo ilikuwa ni chache, lakini baadaye kulitokea badiliko wakatoka kwa wingi wanafunzi wa dini kwenda kusoma

Idadi ya wanavyuoni na wanafunzi wakati huo ilikuwa ni chache, lakini baadaye kulitokea badiliko wakatoka kwa wingi wanafunzi wa dini kwenda kusoma na tukawa na idadi kubwa ya wanavyuoni na wanafunzi wa dini, lakini wakati huu-nazungumzia kipindi cha mwaka 1385 A.H.- wanavyuoni mjini Qatif na vitongoji vyake walikuwa ni wachache wakihesabika kwa vidole.
Kulikuwa na mahatibu wengi lakini si kila hatibu ni mwanachuoni. Ni wachache waliosoma ilimu ya sharia, wengi wao walisoma mashairi na historia.

**Mwandishi:** Madrasa ulizosoma, je zilikuwa ni za kiserikali au ni vyuo tu?

Nilisoma elimu yangu ya msingi katika Madrasa ya Zainul-abidina, sekondari ya kati katika Madrasa ya Ami zote ziko Qatif.

**Mwandishi:** Zimebaki kumbukumbu nyingi tamu za wakati wa utoto zisizofutika, ni zipi unazozikumbuka hadi sasa ukiwa katika umri huu Sheikh.

Zimebaki kumbukumbu nyingi tamu za wakati wa utoto zisizofutika, ni zipi unazozikumbuka hadi sasa ukiwa katika umri huu Sheikh.

**Sheikh:** Ninachokikumbuka sana ni baadhi ya waalimu wa kipalestina na wakijordan walikuwa wakati mwingine wakituzungumzia hali ya Palestina na yanayotokea Jordan na wengine wakitaja fikra za uzalendo wa kiarabu, na yanayohusiana na Jamal Abdu Nasir, niliyasikia haya kutoka kwa walimu ambao wengi walikuwa si wasaudi, kwa hivyo nilisikia juu ya miji yao, madrasa ikanipa picha nyingine mpya tofauti na mahali ninapoishi.

Kingine ni kuwa wakati huo tulikuwa tukiishi kwa tabu kutoka kwa usimamizi wa shule na waalimu, kulikuwa na ukali usio na kikomo.Nakumbuka mwanafunzi alikuwa akichapwa viboko kwa kosa dogo sana, na wengine kuwekwa juani, au darasa zima kuadhibiwa kwa kosa la wachache tu.

**Mwandishi:** Hii ilikuwa hali ya kijumla ya shule za Saudia?

Haikutokea kwangu lakini nilipata baadhi ya adhabu nilipokuwa sihudhurii hafla, hasa tunapokuwa na hafla za kidini ambapo nilihutubu, kisha niliwafahamisha wakaelewa wakawa wakiniita 'Mutawwa', nakumbuka mwalimu mkuu wa shule ya Zainul abidina, Qatif, Ustadh Saad rahil wa kabila la Khawalid wa kijiji cha Akka, Qatif kijiji cha ndugu zetu wa kisunni, akiniona mimi kama Mulla na hatibu, hivyo aliamiliana nami kitofauti, wakati wa Ashura alinisamehe nisipoonekana, ambapo hapo huwa na hotuba nyingi kwa siku kumi.

Nakumbuka mwaka 1388 A.H. nilikuwa nina hotuba huko Ahsaa nikaenda kwake na kumuomba livu ya siku kumi, naenda Ahsaa, akaniruhusu, na nikamshtukiza na ombi jingine la kumuomba amruhusu rafiki yangu nifuatane naye huko, naye akamruhusu.

Hapo nilikuwa darasa la sita, nilipokuwa sekondari waliniomba niwe nikizungumza kwenye idhaa asubuhi, hata kuandika mashairi hafifu, wote wakawa wakiniheshimu kwa kushughulikia dini.

**Kuishi pamoja**

Katika majibu yako umetaja kijiji cha Anak na kabila la Al-Khawalid la kisunni, na jinsi mwalimu wako mkuu alivyokuwa akiamiliana na wewe, mimi naona kuna uzuri katika kuishi pamoja (Sunni-Shia) lakini akilini inakuwa kinyume, je unaweza kulisahihisha hilo?

Kulingana na watu, walikuwa wakiishi vizuri katika ya Sunni na Shia katika mkoa wa Qatif, kama mjuavyo watu wengi wa mkoa huo ni mashia, lakini kuna baadhi ya vijiji vya kisunni kama vile: Akka, Darayn, Ummu Sahik na baadhi ya vingine ambavyo uhusiano wake na shia ni mzuri, hata baadhi ya wanavyuoni wa Sunni walikuwa wakisoma kwa wanavyuoni wa Shia.

Baba yangu alikuwa akiniambia kuwa Imam wa Swala ya jamaa wa Darayn akiitwa Sayyid Ibrahim alikuwa akija Tarut kusoma elimu za lugha ya kiarabu na Nahw kwa wanavyuoni wa kishia na akiwasiliana nao na pia watu wa Akka na mpaka sasa kuna uhusiano mzuri na watu wa Qatif.

Soko kuu la Qatif lilikuwa ni soko la jamii yote, kwa hivyo masunni na mabedui wa mikoa yote walikuwa wakija kununua na kuuza, wengine wanaposafiri kwenda vijijini walikuwa wakiacha amana zao kwa watu wa Qatif, kulikuwa na uhusiano wa kijamii na kiuchumi, na hakukuwa na mizozo wala mikwaruzo wala vizuizi kati ya Sunni na Shia, hiyo ni Qatif, ama hali ya Ahsa ni bora zaidi hata mmoja aliniambia, wao wamesoma vyuoni na wanavyuoni wa kishia na walikuwa wakihudhuria majilisi zao na hakukuwa na matatizo yoyote.

## Marekani na kucheza na mhimili wa kitaifa

**Mwandishi:** Lakini Sheikh: Hasan, nami nikikusikiliza sasa na kulinganisha na uyasemayo, naona kuna kutoelewana nyinyi na wengine mkizungumza katika hafla zenu na mnatuhumiwa kwa kujitenga, naona kuna tofauti na maneno yako, naona lengo ni mambo ya nchi yanayotuhusu sana hasa katika hali hii tuliyo nayo si siri wewe ni mwanasiasa waona mwamerika anavyofanya kaskazini mwa Iraq na zaidi, je waweza kutufafanulia?

Hebu nieleze yafuatayo: Kwanza, kama mjuavyo vyombo vya dola vimeanza kuonyesha dalili nzuri kidogo kidogo, kitambo mambo yalikuwa yakiendeshwa kwa hali ya chini, serikali haikujihusisha na mambo mengi,na Mashia hawakupewa nafasi katika mambo ya kidini na ya kijamii, akawa mtu wa Shia anagombana na kanuni ambazo hazimuangalii na kumzingatia.

Hii moja, la pili, ni wafanya kazi wengi wa serikali si watu wa kutoka mkoani Qatif, Mashia wakawa wanajiuliza kwa nini wanatengwa kwenye taasisi na hasa kwenye vyeo, na hata sasa huwapati katika sehemu nyingi,

nami sisemi kama mshia au sunni bali kama mwananchi wa eneo hili la Qatif, kwenye taasisi za serikali, mtu wa Qatif ametengwa na ana uwezo hawezi kuwa mkuu wa polisi au mkuu wa manispaa ya mji (Meya n.k.) Au mkuu wa chombo chochote, hii ndio inaleta maswali kwa mshia, kanuni haziangalii maslaha yao kidini na kijamii na wanabaguliwa kwenye vyeo.

Ndipo baada ya mapinduzi ya kislamu ya Iran eneo hili liliingia kwenye mtazamo mpya, upinzani ukaanza, wakaanza kusikiliza idhaa za Iran na kufanya wanayoyasikia huko, Sunni nao wakaanza kuiingilia Shia kidini na kielimu upande wa hotuba na fatwa wakati huo, hilo ni jambo linalojulikana.

Hayo ni masuala mengine. Naomba turudi nyuma, je, lini ulimaliza masomo ya msingi?

**Sheikh:** Nilimaliza masomo ya msigi mnamo mwaka 1388A.H.

Hebu niruhusu, Sheikh nimekuacha ukamilishe na sikukujadili juu ya kwamba najadiliana nawe juu ya mapinduzi ya Iran na athari zake kwenu na eneo lenu. Na tunapoweka kwenye meza ya ufafanuzi suala hili na mikanganyo yake ya kidini na kisiasa na kihistoria tutaona natija isiyokuwa hii, hebu tuache maudhui haya na nikuulize: Je baada ya maelekezo ya Amir Abdallah bado mnahisi hivyo kama ulivyosema?

**Sheikh:** Baada ya mjadala wa nchi na maneno aliyoambiwa mrithi wa ufalme yaonyesha kuna ngwe mpya, lakini bado tupo katika kipindi cha kungojea.

Nirudi kwenye kazi yangu na nakuuliza suali la mwalimu wa watoto, uwezo wako kimasomo ulikuwaje?

**Sheikh:** Ulikuwa mzuri wa wastani, sitaki kujitetea nafsi yangu kuelekea kwenye ilimu za kisharia kulikuwa ndio sababu ya hilo.

Nitaondoka hapa Sheikh, kwenye huu wastani wako na tuende kwenye kipindi cha elimu yako ya sekondari, kipindi cha hatari, kwa sababu ya kuanza alama za kubaleghe, sauti kuwa nzito, na kujihisi kuwa umekuwa mwanamume, utatueleza nini juu ya kipindi cha sekondari.

**Sheikh:** Kipindi hicho uhusiano wangu wauongozi na walimu wa shule ulianza kutambulika, nilianza kufanya, kwenye idhaa, vipindi vya asubuhi, na wakinitegemea mimi katika kutatua matatizo ya wanafunzi au wanapoacha kufanya wajibu wao wa shule, wao kwa kunizingatia kuwa mimi ni 'Mulla' walinitaka niwe nikizungumza nao, nikaanza kufanya kazi hiyo ndani ya shule, siwezi kusema niliyoyafanya zaidi ya haya.

**Mwandishi:** Vipi kuhusu waalimu wako na upeo wa kuathirika nao.

Uhusiano wangu nao ulikuwa mzuri, hakukuwa na athari yoyote kwa sababu athari za nje ya madrasa zilikuwa kubwa zaidi, kilichokuwa kipya kwangu ni kusoma lugha ya kiingereza kwenye sekondari, na nakumbuka bibi (nyanya) yangu na baba yangu walikuwa wakisema:"Ukiwa unataka kusoma Qur'an na ulikuwa kabla umezungumza kiingereza, basi ni lazima

Uutwahirishe mdomo wako kwanza."Hii inaonyesha jinsi ile hali ua uhafidhina ilivyokuwa kwetu. Lakini sikumaliza shule ya masomo ya sekondari kwa sababu nilienda Iraq kuendelea na masomo ya dini. Kabla ya kumaliza sekondari, niliona nimechoshwa na masomo hayo, hivyo nilimuomba ruhusa baba yangu niende Iraq, nikajiunge na Hawza, na nilienda.

**Ni tofauti ya utaifa ama ni hofu tu isiyokuwako**

Hapa nitakuuliza waziwazi, kama nilivyosikia kutoka kwa watu wenu kwamba kuna ubaguzi shuleni, je umehisi kitu hiki kwenye shule za serikali?

Wakati huo hakukuwa na hisia za ubaguzi kwangu ila masomo ya dini baadhi yake yalikuwa yakitaja madhehebu ya Shia kwa ubaya kuwa ni bidaa na ni shirki, lakini maelekezo katika mazingira yetu yalikuwa yakifafanua mambo yanayolingana na maedhehebu yetu.

**Mwandishi:** Kulingana na mazungumzo yako, kuna sisitizo la nguvu kwa mtoto wenu kabla ya kujiunga na shule.

Si hivyo ila ni hali tu ya kimaumbile, mtoto huathirika na wazazi na familia yake, sikumbuki kama kuna madrasa inayofunza watoto hao ila hali ya kimaumbile ya mshikamano wa watoto na wazazi wao, Hakuna vipindi vya Televisheni au vya vikaragosi au michezo ambavyo mtoto anavifuata ni uhusiano tu ulio na nguvu wanaishi pamoja na kimaumbile huchukua mafunzo ya dini na tabia kutoka kwao,na waalimu waliokuwa wakifundisha dini wakati huo hawakuwa wakisisitiza masuala ya hitilafu

Kwa kuwa wengi wao walikuwa ni wa kutoka nje ya nchi na wengine kutoka mazingira yenye uhuru zaidi, kwa hivyo walifundisha vipindi vile vilivyo hawakusisitiza hayo sana.

Lakini badaye baada ya waalimu wa Kisaudi kutoka kwenye vitengo vya sharia walipokuja kusomesha walielekeza sana kwenye itikadi, hapa ndio wanafunzi wa kishia walipoingia ngwe mpya na wanaendelea nayo mpaka sasa.

Haupiti mwaka ila utasikia yakizungumzwa juu ya masomo ya dini, kwa sababu mwalimu wa dini huja na ujumbe wa kutaka kuwaongoza watu waliopotea wenye bidaa, kulingana na maoini yake- na hapo ndipo panazuka matatizo. Wakati huo sisi hatukupata matatizo haya.

Ee Sheikh Hasan, lakini suala hili hili ukilirejesha kwa nchi kama Iran, mathalan, kwa kawaida itakuwa ni kuendeleza aidiolojia yao, kwa hivyo sisi si tofauti mpaka tulaumiwe katika wakati mgumu wa kisiasa, nataraji ujumbe wangu uko wazi hapa.

**Sheikh:** Kipindi cha utoto hakina mgongano akilini mwake, ndio tukaona mathalan, Iran haiachi nafasi hii ipite bure. Mtaala wa masomo ya Iran wa kidini katika miji ya kisunni inaenda na mazingira ya madhehebu yao, hakufundishwi ushia.

## Mji mmoja na utaratibu mmoja

Nitakwambia wazi kuhusu unavyosema, sisi ni taifa moja, lazima tuwe na utaratibu mmoja, ama fikra ya zamani ya kugawanya sehemu za Sunni na Shia, ikifaa ni miaka arubaini iliyopita, na si sasa.

**Sheikh:** Hii itahitaji mambo mawili: Kwanza tufanye utaratibu wa elimu wa mwanzo uwe ni wa ushirikiano. Pili, kama ilivyozungumzwa kusiwe na utangazaji wa dhehebu moja kwa watoto, mwalimu anayekuja sehemu za Shia ni lazima alizingatie hili kwa makini, ana haki ya kueleza fikra yake kwa watoto wa shule za msingi na sekondari, lakini kusema baba zenu ni washirikina na mama zenu ni wazushi na koo zenu zote zitaingia motoni hili halikubaliki na haliingii akilini. Na mikoa yetu imekuwa na masunni na mashia na aje mwalimu aseme maneno kama hayo ni wazi atapata mzozo baina ya wanafunzi, na haya ndio yanayotokea sasa katika baadhi ya mashule.

Itakapokuwa kuna Sunni na Shia, na aje mwalimu aseme hao wanaabudu makaburi na kuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na wanaotawasali kwa na maimamu na manabii, ni washirikina na mengineyo.Na uwe na mjadala miongoni mwa wanafunzi, na darasa lagawanyika huyu Sunni na huyu Shia wewe mushriki, wewe wahabi n.k. Je hili lafaa kwa nchi moja?

**Sheikh:** Isitoshe lazima masomo yawe na mwelekeo wa pamoja, kusema upande mwengine ni wa shirki au bidaa si sahih, kwa mfano katika Hijaz kunasomwa maulidi, ndiyo kwa mfano uje useme, kusoma maulidi bidaa, kama maneno yaliyomo katika mitaala ya masomo inavyosema,

huyu mtoto mwingine anaona ukoo wake ukisoma maulidi, huyu mtoto atatatua vipi tataizo hili la mgongano huu wa kifikra? Kwa hivyo ni lazima tuepuke mafundisho kama haya.

Hebu nirudi kwa kijana Hasan Saffar aliyekulia katika mazingira ya kisheikh akiwa mdogo sana, hiyo haikuathiri kukua kwako?

**Sheikh:** Sijui unaposema kuathiri unakusudia nini.

Nakumbuka maneno ya Shafi kuhusu kijana na nimekuuliza hivyo kwa sababu wewe hukukua pamoja na wenzako kama mtoto mwingine, swali ni, je kipindi hiki ushekhe haukuathiri makuzi yako, fikra zako na hiyari zako mpaka sasa ukiwa mtu mzima?

**Sheikh:** Kwa kuzingatia kuwa nilikuwa napenda na hakuna mmoja aliyenilazimisha mwelekeo huu, mwanzo babangu hakunipa moyo wa kuenda kusoma dini na sababu ilikuwa ni hofu yake nisiende Iraq au nisisafiri nikiwa mdogo.

Nahisi kwamba mimi sikucheza vya kutosha nilipokuwa mdogo kama wenzangu, nilikuwa nikicheza kidogo tu wakati fulani, lakini hali ya ushekhe nikiwa mdogo ilinizua kupata fursa ya kupitia maisha ya utoto.

Hebu nikuulize Sheikh, ulipokuwa ukimuomba baba yako akuruhusu uende kusoma Iraq, je hali hii ilikuwa ni kwa wote kwenu Qatif zile familia kubwa zenye ilimu kupeleka watoto kwenye Hawza? Na kwa nini Iraq na sio Iran?

**Sheikh:** Ilikuwa imeenea hali hiyo kitambo kuwa zile familia za ilimu zilikuwa zikipeleka watoto wao kwenye Hawza, lakini muda niliokulia mimi haukuwa hivyo, kulikuwa na ulegevu, hata zile familia za dini pia hazikufanya hivyo, Qatif tukawa twaishi katika hali ya kutounganisha kizazi chetu na ilimu katika kipindi hicho.

Samahani, kabla ya kujibu swali hili laini ilinijia fikra ya kujua sababukwa nini ulienda Najaf na hali Qatif kulikuwa na Hawza na kama nilivyoona katika vitabu vyenu ilikuwa ni Najaf ndogo.

**Sheikh:** Hiyo ilikuwa katika kipindi cha zamani kabla ya kipindi ninachokizungumia, Qatif ilikuwa nyuma sana kelimu wakati huo.

Lakini kwa nini hukuenda Iran?

**Sheikh:** Jamii ya Shia ya kiarabu yote ilikuwa ikisoma Iraq, si Iran, na ufuasi wao kimadhehebu –kihistoria- ulikuwa ni Iraq, si Iran. Pia Iraq ilikuwa ni karibu zaidi Sababu ya pili ni lugha ya kiarabu, tatu, makao makuu ya kielimu kwa Shia ya dunia, ikiwamo Iran, ilikuwa ni Najaf. Hakukuwa na Hawza Iran iliyochukuwa uongozi wa kishia ila baada ya mapinduzi ya kiislam ya Iran, na kukandamizwa kwa Hawza za Iraq kulikofanywa na chama cha Baath kilichokuwa kikitawala wakati huo.

**Marjaiyya ya kishia, je ni ya wasiokuwa waarabu au ni ya waarabu?**

Turudi kwenye kwenda kwako Najaf, je waweza kutuambia vizuri zaidi mtaala wa kielimu wa mwanafunzi wa Shia katika kusoma kwenye Hawza?

Nilienda Najaf mwanzoni mwa mwaka 1391 (A.H.) na niliishi na jamii ya Qatif na Ahsaa, kulikuwa na wanafunzi Wengi na wengine walikuwa wameishi hapo kwa muda mrefu. Na wakiwaangalia wanafunzi wanaokuja wapya, nilisoma kwao na nilisoma kwa ulama wengine wa kilebanon na baadhi Wa kiiraq na masomo yetu ni kama vikao misikitini sio masomo kama yaliyopangwa kwenye mashule bali kila mwanafunzi ana uhuru wa kuchagua somo alitakalo na mwalimu amtakaye. Na pia kuna masomo katika kipindi hiki ya lugha ya kiarabu katika *Nahw, Sarfa, Mantiki,* na *Usuulul fiqh*.

**Mwandishi:** Vitabu gani vya *Fiqh* mnavyovisoma?

Mwanzo kuna ile inayoitwa '*Al-risaalatul amaliyyah*' yaani ni kitabu cha Fiqh cha Marjaaa aliyeko, kila mujtahid huleta rai zao katika hukmu za kisheria bila ya kufuata waliopita, yeye hufanya ijtihad na na kutoa rai zake katika mas'ala ya fiqh, rai hizi hukusanywa na huwa ni *Risaalatul amaliyya* yaaani anayoifuata muqallid (mfuasi wake).
Mwanzo husoma hii risala ili mwanafunzi ajue yanayompasa ili akiulizwa ajibu kulingana na mujtahid aliyeko.
Baada ya hiyo kisha twasoma kitabu, *Sharaiul islam* cha Muhaqiq Al Hilli, Sheikh Jafar bin Hasan (602-676 A.H.) huyu ni fakihi Muiraq.

Baada ya kumaliza kitabu hiki tunasoma *Lumma'a damishiqiyya* na sherhe yake, mtunzi wake ni Sheikh Muhammad Makki Al-Amili wa kutoka Jabal Amili, Lebanon (734-786 A.H.). Hiki kilifafanuliwa na Sheikh Zainuddini Al-Amili (911-965 A.H.).

Hivi ni ufafanuzi mpana kuhusu Fiqh. Kisha baada ya hiyo tunasoma *Al-Makasib* kinachohusianaa na mambo ya chumo, biashara na kuuza na yanaihusiana nayo.Kisha mwanafunzi anaingia katika daraja ya *'Bahth khariji'* hapo mwanachuoni hutoa mas-ala na dalili zake kisha na rai yake, halafu huwaacha wanafunzi wakajadili juu ya hilo.

Kisha kuna kipindi cha kusoma Usuulul Fiqh inapitia vitabu vingine, kama: *Al-rasaail* cha Sheikh Murtadha Al-Anari, *Kifayatul usuul* cha Sheikh: Muhamad Kadhi Al-Khurasani 1255-1339 A.H.). Kisha huwa *Bahth khariji* kwenye Usuul. Ikifuatana na kwenye Fiqh.

Na baada ya miaka kwenye mijadala hii, mwanafunzi akithibitisha wakati wa mijadala yake na mwalimu wake na wenzake au maaandishi yake, kwamba yeye ana uwezo hapo huwa mujtahid, na mwalimu wake humpa '*ijaza'* ya ijtihad. Kwa maana ya kuwa huyu anaweza kufanya *istinbat* ya Hukmu ya kisharia.

Ndio kuwa mujtahid hakuhitajii ijaza, lakini ili watu wajue kwamba huyu ni mujtahid, daraja yao iko tofauti, kuna ajuwaye na kuna ajuwaye zaidi, watu sio wamfuate tu mujtahid yeyote, bali watafute aliye mjuzi zaidi (*a'alam*).
Na huenda kusiwe mmoja huenda wakawa watatu au sita au saba ambao wanajulikana kwa ujuzi zaidi na mara nyingi kuna mmoja anayejitokeza zaidi kuwa Marjaa mkuu.

**Mwandishi:** Hii ni kwa upande wa Fiqh, lakini upande wa itikadi ndio naupa umuhimu sana kutaka kujua kutokana na hitilafu iliyoko kati yenu na wengine, je wasemaje juu ya vitabu vya itikadi?

Sana katika upande huo kitabu tunachosoma ni ni *Tajridul itiqad*, cha Sheikh Muhammad Hassan Tusi (aliyekufa 692 A.H.), na ana maelezo marefu ju ya masuala mengi pia katika tawhid na utume, Kiyama na uimamu, kisha kuna *Babul hadi-a'shara*, nacho ni sehemu katika kitabu cha Sheikh Hasan bin Al Muttahari Al Hilli (726 A.H.).. Na katika miaka ya mwisho mwanafunzi husoma kitabu *Aqaidul imamiyyah* cha Sheikh Muhammad Ridhaa Al Mudhaffar, huyu ni katika wanavyuoni wapya wa kiiraq vyote hivi vyaleza madhehebu ya shia, itikadi zake bila ya kukufurisha wengine.

**Kitabu *Al-Kafi* na daraja yake kwa mashia**

Hebu niulize juu ya kitabu kiitwacho *Al-Kafi*, ambacho kwenu nyinyi ni kama kwa Sunni Kitabu Sahih Bukhari, hiki mnakisoma darasa la ngapi?

**Sheikh:** Hiki hakisomeshwi kamwe, wala hakichukuliwi kuwa ni kitabu cha kiitikadi wala cha kifiqh, ila tu ni kitabu cha mkusanyiko wa Hadith, na sisi Shia hatuamiliani nacho kama ndugu zetu Sunni wafanyavyo kwa Sahih Bukhari na Muslim.

Sio kwamba Hadith zote humo ni sahih bali ni kwa mujtahid asome kila Hadith ana sanad yake matini yake na ailniganishe na zingine na kisha atoe rai yake kama ni sahih au si sahih, Sunni wanawapatiliza Shia kwa yaliyomo katika kitabu hiki na hili ni kosa kubwa.

Kitabu *Al-Kafi* kamwe hakisomeshwi katika hawza zetu, wala si kitabu cha itikadi wala cha Fiqh, wala haifai kuwalaumu Shia kwa kila Hadith iliyomo humo.

Kwa uwazi kabisa mimi nashtushwa na majibu yako Sheikh Hassan Saffar, mwanachuoni wa Shia, je ni maoni ya Sheikh Saffar au ni maoni ya wanavyuoni wote wa Shia waarabu na wasiokuwa waarabu?

**Sheikh:** Wanavyuoni wote wa Shia wanasema hivi, kulikuwa na kikundi cha fikra kwa Shia kikiitwa Muhaddithuuna na Akhbariyuuna, kikundi hiki kilionelea usahihi wa Hadith zilizomo kwenye vitabu vine: *Al-Kafi, Tahdhiibul ahkaam, Al-istibswaar na man laa yahdhuruhul faqiih*, wao kwao ni kama vitabu vya sahih Bukhari na Muslim na kikundi hiki ilikuwa katika karne ya kumi na moja na kumi na mbili (A.H.).

Ama kabla ya hao mwelekeo ulikuwa ni kuona kuwa Hadith zilizomo humo si zote ni sahih. Lau mtu atasoma kitabi kimoja cha Shia cha Fiqhul istidlali ataona ukweli huu uko wazi.

Mwanachuoni mkubwa kabisa wa Shia wa sasa na pengine mshamsikia Sayid Abil Qasim Al-Khui, ana kitabu kikubwa kiitwacho '*Mujam rijaalul hadiith*' chenye juzuu ishirini na katika utangulizi anaeleza waziwazi kuhusu rai yake na rai ya wanavyuoni wahakiki wa Shia juu ya Kitabu *Al-Kafi* na juu ya vitabu vine. Riwaya za vitabu vine sio kwamba ndio zenye uamuzi wa mwisho.

Na katika utangulizi wa juzuu ya kwanza asema: "Baadhi ya wanavyuoni wamesema kuwa riwaya zilizomo katika vitabu vine ndio zenye kuamua kila jambo (uamuzi wa mwisho). Kauli hii ni batili, vipi iwe hivyo na ni riwaya zilizopokewa na moja moja, na hasa kuna baadhi ya wapokezi walikuwa wakijulikana kuwa ni waongo na wazushi."

Kilichothibiti kwa Shia ni kuwa *Al-Kafi* ni rejeo la Hadith tu, kwa hivyo watu wanaotushambulia kwa Hadith zilizomo katika *Al-Kafi* ni kama vile sisi tuwalaumu Sunni kwa Hadith zilizomo katika Musnad ya Imam Ahmad bin Hambal, au juu ya Hadith zilizomo katika Kanzul-Ummal, mimi sikulaumu unaposema kuwa Hadith hii si sahih au imetungwa tu au dhaif, Shia, kwa mujibu wa vitabu vyao vine vya Hadith wanaamiliana navyo kwa misingi hii.

## Kipindi cha kujiunda kitaifa

Ningependa kuuliza lini mwanafunzi wa Shia anapoanza kujiunda kitaifa dhidi ya Sunni.

**Sheikh:** Katika vyuo vyetu hatufundishwi kitabu cha kujiunda kitaifa dhidi ya Sunni bali kinyume na hivyo, vingi miongoni mwa vitabu vyetu hasa vya ilimu ya lugha ya kiarabu, sarfa na Mantiki ni vya wanavyuoni wa Sunni. Kwenye Nahw, twaanza kusoma kitabu *'Sharhul Ajrumiyya* cha Ibn Ajrumi Swanhaji, kisha twasoma *Qatrun nada* cha Ibn Hisham, kisha *Alfiyya* ama sharh ya Ibn Aqil, kisha tunasoma *Mughni llabiib an kutubil agharib* pia cha Ibn Hisham, hivi ni vya Nahw tunavyosoma vyuoni mwetu.
Ama vya Sarfa, pia ni vya Sunni kama kitabu, *Shadha lurfu fiahkaami sarf* cha Ahmad Hamlawi, na kattika Mantik na balagha twasoma cha *Taftazani, Mikhtasarul maaany wal badii*. Ama vitabu vya Fiqh vinaonyesha maoni ya kifiqh na pengine kuonyesha maoni yanayopinga.
Hatuna kujiunda katika kipindi chetu cha masomo kwani vitabu ni vitabu vya kielimu, na kujiunda ni ada inayoenea kwa watu wote.

Ama masomo yanakuwa ni kielimu, bali ni kinyume na hivyo mara nyingi masomo yetu ya fiqh yanakuwa ni ya kulinganisha yakaonyesha rai ya Sunni upande mmoja nay a Shia upande mwingine. Iwe ni kwenye Fiqh au kwenye *Usuul*.Isitoshe, ratiba yetu ya ilimu ni ratiba iliyo wazi na mtu yeyote anaweza kuiona.

Lakini ee Sheikh Hasan, historia haifutiki na mzizi wa utengano wa Sunni na Shia u wapi uliosababisha hali hii, kwa mfano suala la kutukana maswahaba?

**Sheikh:** Hii ilitokana na sababu mbili: Ya kwanza, shia walikuwa wana uwakilishi mdogo sana kiserikali, na mara nyingi Fiqh ilikuwa ni ya madhehebu rasmi ya Sunni, mara nyingi Shia walikuwa wakikandamizwa, kama kipindi cha utawala wa kiamawi, wa kiAbbas na wa ki-Uthmani, walipokuwa wakifanyiwa hivyo kulipatikana kuakisi kwa Mashia ndio wakashikana sana katika madhehebu yao na kujaribu kuihami wao na vizazi vyao kutokana na sharia zilizoko, na haipingiki kwamba kulikuwa na mvutano katika Historia na mzizi wa utengano ulitokana na kutoheshimu kwa maoni ya wengine na kuwakandamiza wafuasi wake.

Mwanzo wa hitilafu, kama ijulikanavyo, ni za kihisia juu ya ukhalifa na uimamu lakini haukudumu hadi kufikia kuwa ni wa kidini na kisharia kwa kila upande na hapo ndipo zikajiunda madhehebu na miongozo.

Samahani Sheikh kwa kuhitilafiana nawe hapa. Umesema kuwa Shia walikuwa na uwakilishi mdogo daima, hii si sahihi, kulikuwa na Dola ya Safawiyya, na ya Bawhiyya na Hamdaniyya. nikutajie dola ya Fatimiyya na historia ya kutawala kwao?

Je nikutajie dola ya Fatimiyya na historia ya kutawala kwao?

**Sheikh:** Ndio, kwenye utawala wa kiislamu walikuwa ni wachache, nao walikuwa wanatawala baadhi ya sehemu kwenye baadhi ya nyakati, Fatimiyy walitawala Afrika ya Kaskazini, Misri na baadhi ya miji ya Syria, na Wahamdany walitawala Mosul na Aleppo, na Wabahwy walitawala sehemu ya magharibi ya Iran na Iraq, Waswafawy walitawala Iran.

Utawala wao ulikuwa ni wa muda fulani wa kijografia lakini haumaanishi kwamba hawakuwa na uchache kiujumla.Ama juu ya kuhusu kuamiliana Sunni na serikali hizo kunahitaji utafiti mrefu wa kihistoria.

Utawala wa Shah wa Iran, mathalan, ulikuwa ukichukuliwa kuwa ni wa Shia lakini wanavyuoni wao hawakukubaliana nao na mwishowe waliuangusha.

Sitojadiliana nawe sana Sheikh juu ya hitilafu hiyo lakini swali langu hapa ni juu ya asili ya Shia, mimi japo sijui naona kuwa msingi wake ni wa kisiasa kwa kiwango cha msingi, yaani umesimama kwa misingi ya fikra za kisiasa.

**Sheikh:** Hata misingi ya Sunni pia ni ya kisiasa kama tukichukua siasa ndio kipimo cha utengano. Maana ya maneno yangu haya ni kuwa si sahihi kuwa upande mmoja ujione kuwa ni wa kidini na kuuona mwimgine kuwa ni wa maslahi ya kisiasa. Hii ni makosa, kila upande wajizingatia kuwa misimamo yake ya kisiasa imetokana na ya kidini. Na kila moja ina mrengo wa kiitikadi na kifiqh.

Baada ya kufariki Mtume (s.a.w.w.) uungwaji mkono wa khalifa wa kwanza ulipatika kwenye baraza ya Bani Saida ndipo pakawa msingi wa ufuasi wa Sunni katika ukhalifa. Na ndipo ukaanza upinzani kutoka kwa baadhi ya Bani Hashim na baadhi ya masahaba waliona kuwa afaaye kwa uimamu ni Imam Ali bin Abi Talib, hapo ukawa ndio msingi wa ufuasi wa madhehebu ya Shia, ikawa ni jambo la kawaida kila upande kutetea wafuasi wake kutetea rai zao na misimamo yake, na baada ya kupita masiku na kutukia matukio mbalimbali, ndipo zikawa hizi madhehebu mbili tofauti.

Na katika karne ya pili madhehebu za kifiqh zikaaanza kujiunda ndipo wakatokea wanavyuoni na wapokezi wa Hadith na kufuatiwa na wanafunzi wao kama vile Imam Malik, Abu Hanifa, Imam Shafi na Imam ahmad bin Hambali.

Hakuna anayekanusha daraja ya juu ya kielimu ya maimamu wa Ahlu bayt haikanushiki wao kuwa na madhehebu. Imam Jafar Sadiq, kwa mfano, alikuwa ni mwalimu wa wanavyuoni na mafakihi wakubwa zama zake na walikuwa wakimkubali.

Samahani Sheikh, tuje kwenye suala la Imam aliye ghaib (Mahdi) ambalo ni moja katika nguzo za dhehebu la Shia, je hii si fkra ya kisiasa ya kiwango cha juu?

**Sheikh:** Lakini moja katika nguzo za madhehebu ya Sunni ni kwamba Uimamu na Ukhalifa hupatikana kwa ushindi na uchaguzi na nguvu, hii pia ni fikra ya kisiasa, Sunni pia ni kama Shia ikiwa tutazingatia ukhalifa kuwa ndio chanzo cha tofauti.

Mwanzo wa hitilafu sio kama vile suala la je Mungu ataonekana kesho Akhera, bali asili yake ni yule mwenye kushika cheo hicho. Tofauti ni kuwa Sunni wao ni kama jambo limetokea kuwa utawala ulikuwa mikononi mwao lakini Shia hawakuwa nao.

Kwa hivyo ni makosa kusema kuwa asili ya madhehebu ya Shia ni ya kisiasa bali twasema asili ya hitilafu ni juu ya kadhia ya kisisasa ambayo ilifanya Sunni wakashika upande wao na Shia pia wakashika njia yao. Nataraji hapa fikra hii imeeleweka wazi.

Lakini Sheikh, naona kama asili ya hitilafu si ukhalifa tu bali iligeuka na kuwa kwenye misingi ya kiislamu kama vile, taawili na uthibitisho wa nassi za Uislamu, isma, maswahaba, Qadar, Tawhiid, uungu, na misingi mingineyo.

**Sheikh:** Ndio msingi wa hitilafu ni kuhusu uimamu na ukhalifa kisha ikakua na kugawanyika, kwa sababu Shia wanaonelea kuwa ilimu za dini zichukuliwe kutoka kwa maimamu wa Ahlu bayt (a.s.) inapotokea hitilafu kati ya maimamu na wengineo wao huchukua kauli za maimamu wao. Ama Sunni wao wanaona ni bora kuchukuwa kutoka kwa maswahaba na tabiina.

Ama maneno kuwa kuna hitilafu katika misingi hayo ni sahihi, lakini sio katika dhati ya misingi, kwa kuwa Shia na Sunni wanaafikiana juu ya kuamini Mungu moja, Mtume wake, Muhammad (s.a.w.w.) kuamini Akhera, kurejea kwenye Qur'an na Hadith, hapo hakuna maafikiano katia ufafanuzi wazo, na hivyo hata kwa Sunni wenyewe pia. Kuna Ashaira, kuna Mutazila, kuna Salafi na kuna Sufi.

Pia vilevile hakuna maafikiano ya kila jambo kwa mashia wote katika maelezo yote.Ama kuthibiti nassi ya Qur'an kumeafikiana kati ya Sunni na Shia, hata maoni ya kipekee ya kuwa kuna upotofu umefanyiwa Qur'an pia si kuwa kuna mjadala wa kuthibit nassi za Qur'an iliyopo bali yakubalika na yatumika ila baadhi wanaona kuwa ina upungufuna imefutwa baadhi ya Aya, hii rai ni yenye kupingwa lakini na tofauti katika kuzifahamu Aya za Qur'an na kuziawili zipo kati ya madhehebu, na ndani ya madhehebu.

Kwa hivyo nasisitiza kauli yangu kwamba kuna tofaut ya asili kati ya Shia na Sunni kwa sababu yakisiwa kuna tofauti katika dhati ya misingi, kama invyokisiwa kuwa kuna maafikiano katika Sunni wote katka maelezo yote ya misingi.

## Najaf na kutafuta elimu

Umri wako ulikuwa miaka mingapi wakati huo?

**Sheikh:** Ulikuwa ni miaka 14.

Vipi muda ulioishi na wenzio wa Saudia, na je uliwahi kukutana na mshairi marufu wa Iraq mzaliwa wa Najaf, Al-Jawahiri?

**Sheikh:** Niliishi kipindi hicho na wanafunzi wa Saudia na Bahrain tukiwa na baraza la kila wiki kwa hafla za kidini wakikutana kwenye nyumba ya Sheikh Ahmad bin Mansur Al-Saif mmoja katika wanavyuoni wa Tarut, Qatif (1326-1406 A.H.). Na baadaye kwenye nyumba ya Mansur bin Abdallah Al-Bayat, ni katika wanavyuoni wa Qatif (1325-1420 A.H.).

Na mengine ni kwa baadhi ya wanafunzi na watu wa Ahsaa na Bahrain.Na kulikuja hapo baadhi ya wanafasihi wa Qatif kwa sababu za kisiasa zilizowapata huko waliishi Najaf kwa muda mpaka mambo yalipokuwa mazuri wakarudi Qatif. Miongoni mwao ni Sayyid Baqir Al Awami, alikuwa ni mwanasheria na mwanafasihi nilifaidika naye kwani alikuwa akiwashajiisha wanafunzi na wanavyuoni kuwa na harakati na akiandika barua nyingi kwa viongozi wa kidini.

Pia kulikuwa na Sheikh: Abdallah Al-Khinizi, hakimu wa mahakama wa mambo ya mirathi na nyakfu hivi sasa akijionyesha kwa vazi la kidini naye marufu kwa kitabu *Abu Talib muumin Quraish* ambaye aliutetea Uislamu wa Abu Talib akapata matatizo.

Kisha alikuja Najaf kwa hali za kisiasa. Kwenye majlisi zake nilikutanaa wasomi wa Iraq, Misr na Lebanon na wanafunzi wa Saudia wenye hima, pia Sheikh Abdul Ali bin Yusuf Al Seif aliyejiunga na kitengo cha Fiqh na kupata shahada yake ya juu (Phd.) na akatunga vitabu vingi juu ya elimu fasihi na uhusiano wa wasomi; nami nilikuwa na uhusiano mzuri naye, hivi sasa yeye ni mwanasheria wakili wa Qatif.

Sheikh Ibrahim bin Abdallah Al Gharash alinipa malezi mazuri katika miaka ya mwanzo yangu Najaf, huyu sasa ni Imam wa Ijumaa na jamaa wa Qatif, nilishirkiana naye kupangisha nyumba moja na familia yake ikinitazama vizuri, na nilijifunza kwake misingi ya lugha ya kiarabu, na kuipa umuhimu sana Nahw, nilihifadhi kwake kitabu *Alfiyya* cha Ibn Malik kwa kuwa yeye alikuwa ni kipofu.

Wakati mwingine nikihudhuria majlisi za Marjaa kama vile Sayyid Khui (1317-1413 A.H.).Na majlisi za Sheih Shahrudi, na majlisi za Sheikh Muhamma Baqir Sadr (1335-1400 A.H.). Na majlis za Sheikh Al Kasshiful Ghitaa, na za Sheikh Muhammad Amin Zainud diin (1333-1419A.H.).

Pia nikaona wengine niliokuwa nikiwasikia kama mtafiti Asad Haidar na nilisoma kitabu '*Al imamus sadiq wal—madhahibul arbaa*'. Na mwanachuoni Sheikh: Baqir Sharif Al Qarashi mwenye tungo nyingi juu ya Ahlul bayt. Pia khatibu maarufu Sheikh Daktur Ahmdul Al Waili, na khatib Sayyid Jawad Shibr.

Pia nilienda kwenye maktaba kwa kudurusi kama maktaba ya Amirul muuminiin na maktaba ya Al-Hakim. Nikahudhuria hafla nyingi na maonyesho ya kidini, sikukutana na mshairi maarufu Al Jawahiri yeye alikuwa akiishi Baghdad, na pengine nje ya Iraq na hali ya kidini tuliyokuwa tukiishi ilikuwa haimpingi ilimzingatia kuwa nje ya hali ya kiislamu, japo hali yake ya kifasihi ni ya kuheshimiwa.

Na Najaf kulikuwa na vita vya kiislamu na mirengo kama ya kikomunisti, kidemokrasi, na migongano baina ya Baath na Qawmiyya. Kabla ya kwenda kwangu Najaf sikuyajua haya kwa sababu nilikuwa naishi katika mazingira ya kuishi kama nilivyokulia tu
Najaf nilisoma kwa makini kitabu cha Baqir Sadr '*Falsafatuna*' na *Iqtisaduna* na nikawa nasoma jarida la Al-Ahwaa likitolewa na wanavyuoni.

Pia kitabu cha Sheikh Muhamad Amin Zainu ddin '*Ila talliatil muumina*'. Na *Al-Islam yanabiuhu ghaayaatuhun aal Aaf baina salbi waijabi*.

Nitakusimamisha kidogo hapa; ni kuwa nyinyi Qatif hamkuathirika na aidiolojia hizi kama ulivyosema lakini aliyesoma historia yenu yaoekana kuwapo aidiolojia nyingi kama za ukomunisti, Baath, na Nasriyya na zinginezo zilikuwako, nami nakukumbusha kuwapo kwa chama cha Shia cha saudia, Baath cha kisosholisti, kukiwa na kiongozi Hamza Hasan na watu wa Qatif wengi walijiunga na vyama hivi, wasemaje.

**Sheikh:** Nilipokwenda kusoma Najaf sikuwa na fikra zozote za kisasa na hivyo ni kwa kuwa nilikuwa mdogo lakini huko Najaf nilianza kujua mapambano ya Uislamu na fikra zingine hizo, ni kweli Qatif kulikuwa na fikra hizo lakini hali ngumu ya wakati huo hazikufikia hali ya kuathiri sana jamii kwa kuwa serikali haikuruhusu hizo ziendelee ambapo zingne kama Baath ilikuwa ikitawala Iraq. Hii ndio hali niliyoishi huko Najaf.

Hebu tumuache Hasan Safar akiwa mdogo na tuje kwenye Hasan Safar Sheikh na mwanachuoni. Nakuuliza sasa, kwa nini vijana wa Shia wanakumbatia fikra hizo, je hawaridhiki na mambo yalivyo nchini? Mathalan mimi najua kuwa nusu ya walioshiriki katika maandamano ya ARAMCO walikuwa ni mashia, utaeleza vipi juu ya hili?

**Sheikh:** Fikra hizi zilipenya kwenye mikoa mbalimbali ya Saudia na kuenea kwa Mashia kwa sababu mbili:
Kwanza: Kuhisi mapunjo na kukandamizwa kunasababisha kuwe na fikra za kimapinduzi.
Pili: udhaifu wa harakati za ilimu na kidini, kwa kuwa ilimu ilikuwa ni ya kuiga na kufuata tu, hakukuwa na fikra mpya za kuingia ndani ya bongo za vijana na kujibu maswali yao

Ukiongezea na kutopata fursa ya kufanya kazi za kidini rasmi hasa kwa mashia, kiasi kwamba hawakuwa na nafasi ya kuanzisha ofisi au kuchapisha vitabu au kutoa jarida au hata kuwa na taasisi ya kielimu.

Baadaye nilikuja jua kuwa wengi waliojiunga na fkra hizi ni kwa kuwa kujiunga kwao ni kwa karibu zaidi kisiasa ili kujikinaisha kifikra.

Hebu niruhusu nieleze kustaajabu kwangu.Mimi nayaangalia haya kwenye upande mwingine. Huoni kwamba kushikamana na dini kwa jamii kuna nguvu zaidi kuliko kushikamana na ukomunisti au baath? Na hasa –kama ulivyosema- kuwa idadi yao ni kubwa?

**Sheikh:** Hakuna njia ya kuweza kuwaukusanya wote hii iko katika kila jamii ya kibinaadamu, mfano Najd, japokuwa hali ya kidini inayotawala ina nguvu ya inavyoamrisha lakini pia hilo halikuzuia kujitokeza watu kama Abdallah Al-Qasimi na vikundi mbali mbali vyenye mielekeo ya kisiasa.
Ikiwa ni sahihi kuwa mwelekeo wa jamii ya kishia ulikuwa ni mkubwa zaidi kuliko kwa wengine inadhihiri kwangu kuwa hayo na kwa wale wa zamani, na kuhisi kupunjwa na kuwekewa mipaka shughuli za kidini na pia kuongezea kuwapo kwa ARAMCO nchini.

**Swali muhimu zaidi**

Pengine swali hili lanipa nguvu ya kufungua suali nyeti, nalo ni kule kutuhumiwa Shia juu ya kupenda kwao sana katika kufuata na kushikamana kiakili na kihakika, na pengine maudhui haya yamekuja mara nyingi

Na napenda luthibitisha nawe Sheikh, hasa kipindi hiki tunachopitia, ningependa kusikia kwako juu ya suala hili ambalo linawaelekea mashia wa jimbo la Mashariki.

**Sheikh:** Tuhuma hizi wanazoelekezewa Shia ni ni katika kudhihirika kusumbuliwa kwao na kuwapo kwa mawimbi ya kifikra na kisiasa si kwa upande wa Shia tu, mfano vita vilivyokuwapo kati ya Salafiyya na Hadithiyya hapa nchini Saudia havikuwa kwa upande wa Shia na kwa nini jambo hili lielekezwe kwa Shia tu na si kwa wengine? Vyama na mawimbi ya kifikra na kisiasa pia vilikuwapo katika majimbo mengine ya kisunni kama inavyojulikana kwa nini itajwe Shia tu?

**Mwandishi:** Sheikh, nahitaji mwanasiasa ili tujue msimamo tunaoishi nao sasa kama jamii pamoja na kuingia mmarekani kwenye msitari na kututia msongo na hatimaye ni wizara ya mambo ya nje ya marekani kutangaza uhuru wa kuabudu nawe wajua kuwa kuna jamaa katika Shia wanaokumbatiwa na wa magharibi katika marekani na Uingereza nayo ni jamii yenye upinzani.

Ni jambo la kawaida kwa wamarekani waende mbio kujifaidisha na udhaifu unaopatikana na watafute njia za kutusonga na kujiingiza katika mambo yetu ya ndani.

Ama uliyotaja kuhusu mashia wanaoshikiliwa na watu wa magharibi hilo ni jambo limetiwa chumvi, huenda kukawa na mashia hutoa rai zao bila ya kukubalika lakini kuwatuhumu wote kwa kushirikiana na wa magharibi ni jambo lazima lithibitishwe na naamini hapo kumetiwa chumvi.

Samahani Shekh, niliposema kuwa wao kujiunga na upinzani ni kama wanavyofanya upande wa Saad Al-Fakihi ni kitengo kinachodaiwa sio hali ya Shia tu, hasa bali ni hali ya ujumla.

**Sheikh:** Nilisema, ndio lakini jambo kama hilo liko kwa watu binafsi haifai kulichanganya kwa wote inapasa suala hiolo ulipe matazamo wake wa kisiasa na lisipewe mtazamo wa kiujumla.

**Mwandishi:** Tuseme kuwa ni sauti ya Shia ipingayo.

Kama ilivyo kwa Shia zipo na kwa Sunni pia. Kwa nini kunapokuwa kwa masunni huko Ulaya inachukuliwa kuwa ni upinzani pekeee na inapokuwa Mshia inachukuliwa kuwa ni mashia kama inavyochukuiwa kwa Saad Al-Fakih amathala au Mas'ari au wengineo, lakini kwa nini inapokuja kwa suala la shia inahisabiwa ni mashia tena wote? Je huu si ubaguzi?

Ningependa kusema kuwa kutiwa chumvi sana mambo haya juu ya mashia kuhusu msimamo juu ya marekani ni jambo lisilokubalika. Mashia wao ndio walioanza kupinga marekani ndani ya Mashariki ya Kati na si Salafiyya, na katika kipindi ambacho kulikuwa na uhusiano wa pande za masunni na wamarekani kuhusu Afghanistan, Mashia wa Iran, Lebanon, na sehemu zingine walipinga wamarekani na hili ni ni jambo lilikuwa wazi.

Kama tukio la Iraq limefungua baadhi ya Mashia kuwa pamoja na wamarekani hiyo imekuja baada ya jamii za kisunni kushiba kushirikiana na wamarekani nao pia

Ni kama mashia wa Iraq kuna upande unaounga mkono na kuna upingao. Na bada ya kutangaza Marekani uhuru wa kuabudu nchini Saudia, sisi tulikataa nchi hiyo kuingilia mambo yetu ya ndani.
Yapasa tuache kutia chumvi mambo na tuhuma kwa sababu hayo hayajengi umoja wa nchi bali yanaleta uadui.

Nimekusudia katika kuuliza kwangu huko kutaka kuzindusha juu ya hali ya kuigiliwa na wamagharibi na wamarekani kutuchezea nchini.

**Sheikh:** Nakubaliana nawe kuwa ni suala nyeti na nguvu ya marekani nchini kwetu ni ya hatari watatusonga sana hii ni kweli na inatia wasiwasi kwa kila muislamu mzalendo halisi lakini vipi tutapambana nayo?
Namini kuna mambo mawili ya kimsingi:
1. Kutafuta tiba ya zile sehemu dhaifu na kufanya bidii katika kuleta maelewano kama katika hotuba aliyoitoa mtumishi wa haram mbili (mfalme wa Saudia) alipokuwa akifungua kikao cha pili cha bunge.
2. Kuwe na umoja wa kitaifa na kutupilia mbali tofauti za kimadhehebu na kujitambulisha kikabila.

**Ibnul Alqamy katika historia**

**Mwandishi:** Wallahi Sheikh mimi si mwandishi maalum wa historia lakini kile ninachokijua kwa kweli juu ya Ibnul Alqami ni kuwa alifanya hiyana kubwa kihistoria na alistahiki laana ya kila umma tangu hapo, kwa sababu ya kazi yake chafu katika kumfanyia khiyana khalifa wa Bani Abbas na kuwasaidia Tatar.

**Sheikh:** Je wajua kwamba tuhuma dhidi ya Ibnul Alqmi kuligana na mustawa wa kiutafiti wa kielimu wa kihistoria hazina ithbati; wanavyuoni wa historia wa Shia wamejadili kama Seyyid Hasan Amini katika kitabu chake juu ya vita vya Mogul na kujibu kwa dalili za wazi, licha ya huyu wa Shia hata Mwanachuoni wa Sunni Dkt Saad bin Muhamad Al Ghamidi, profesa wa historia katika chuo kikuu cha Almalik Suud cha Riyadh amejadili tuhuma hizi na kwa insafu kabisa. Kwenye kitabu chake *Suquutud dawlatul abasiyya,* kimechapishwa Riyadh mwaka 1401 (A.H.) na kutumiwa na vyuo vikuu vya Saudia kama marejeo. Na kilichapishwa tena mwaka 1403 (A.H.).

Alisema huyo kwamba kumtuhumu Ibnul Alqami hakuna dalili yoyote bali kuna dalili zaidi ya kumi na moja zinazomvua na tuhuma hizo za khiyana na kwamba msingi wa tuhuma hizo ni tofauti za kimadhehebu na kikabila, lakini lenye kusikitisha ni kutolewa ripoti upande wa kidini kwa kukusanya kitabu kutoka kwenye maktaba na kukichoma na kukipiga marufuku hata nakala iliyoko kwenye maktaba ya chuo kikuu imeichwa hawezi kuisoma yeyote ila kwa ruhusa maalumkama nilivyoambiwa- yote hii ni kwa hoja kuwa kitabu hicho kinatetea Rafidha.

Lau tufaradhie mtu wa Shia amefanya khiyana, je Shia wote watalaumiwa kwa huyo katika historia yao? Je kwa Sunni hakuna watawala na wanasiasa na wengineo waliopotoka na kukhini? Je yafaa kuwatuhumu masunni wote? Unapotokea ugaidi kutoka kwa Sunni husemwa ni kikundi kidogo tu chao, haisemwi Sunni wote au Salafi wote, lakini inapokuwa upande wa watu wa Shia inatajwa kwa wote, je huu ni uadilifu?

## Msimamo wa Shia juu ya marekani

**Mwandishi:** Mbali na kusihi au kutosihi uliyoyasema nakubali kwamba matatizo ya pande zetu zote ni kutokana na historia ya ukinzani sasa umefikia wakati wenye akili wa pande zote kuondoa hayo zibaki zile za msingi ambazo haziwezi kuondolewa na Hasan Safar wala Abdul Aziz Qasim. Ningependa kutoa shukrani zangu kwenu kwa msimamao wenu juu ya taarifa zenu za kila siku juu ya kamati ya marekani kwa kuujua mchezo mchafu wa wamarekani.

Napenda kusema na kutangaza kwa sauti ya wazi kuwa kila Muislamu na wananchi wa marekani wao wanataka kulinda maslahi yao nao ni kushirikiana wazi na Israel na wanatangaza msaada wao, na ridhaa zao kwa uzayuni hivyo wao hawakuja kwa ajili ya Demokrasi na kulinda haki za binadamu bali ni kwa ajili ya maslahi yao. Kwa hivyo nawatahadharisha waislamu wote na wananchi wote wasidanganyike na mambo haya ya wamarekani na pia serikali yetu isiipe fursa marekani ya kufanya njama zao.

## Najaf tena na hawza

Tukiachilia mbali haya ya Marekani, hebu turudi nyuma kwenye mazungumzo yetu juu ya kule Najaf ulikaa kwa muda gani huko?

**Sheikh:** Nilikaa miaka miwili tu hali ikawa mbaya wanafunzi na wanavyuoni wakatoka hata wa Qatif.

**Mwandishi:** Lini hiyo, na je kutoka huku kulisababishwa na mambo yenu ya kisiasa?

**Sheikh:** Si kwa sababu za kisiasa, lakini kwa tuhuma kwamba wao ni majasusi wa serikali zao, hii ni kutokana na vile utawala wa kibaath ulivyokuwa ukipambana na dini na hawza za kielimu.

Je hu ulikuwa ni wakati wa Ahmad Hasan Al Bakr au wakati wa Abdul Karim Qasim.

**Sheikh:** Wakati wa Ahmad Hasan Al Bakr. Hatukumkuta Abdul Karim Qasim, tulikuwa tushaondoka, wanafunzi wengi wa Qatif walikuwa wakiogopa ila baadhi ya wachache wakubwa ambao waliona wao hawana chochote, baadhi walirudi na mimi nikajiunga na Hawza ya Qum, Iran.

**Mwandishi:** Hiyo ilikuwa lini?

Hiyo ilikuwa mwaka 1392 (A.H.) wakati huo ilikuwa ni kipindi cha Shah na kulikuwa na umoja wa wanafunzi wa kiarabu kutoka Iraq waliohamia Iran kwa hoja kwamba wao asili yao ni Iran.
Pia walebanon na wa wakhozistan waarabu, alitupokea wakati huo Marjaa mkubwa Sayyid Muhammad Kadhi Shariat Madar, naye alikuwa na Taasisi iitwayo Daru tablighul islami, alikuwa ni mtu aliyeshirikiana vizuri na taasisi za kisunni kama vile Rabitatul alamii Islami, hata muda ule nilipokuwa Qum ulikuja ujumbe kutoka Rabita ukiongozwa na Sheikh Abul Hasan An Nadwi, walipokewa vizuri na wakajadiliana juu ya mkuruba baina ya wafuasi wa madehehebu za kiislamu.
Taasisi yake ilikuwa ikitoa jarida liitwalo Al-Hadi kwa lugha ya kiarabu na kulikuwa na makala za wanavyuoni wa Sunni, isitoshe harakati hii ilishirikisha pia watu kama

Seyyid Hadi Khusru Shah, Sheikh Muhammad Ali Taskhiri, Sheikh Muhammad Al Asifi, Sheikh Muhamad Said Numani na wengineo ambao walifanya kazi kubwa baada ya mapinduzi ya kiislamu.

**Mwandishi:** Wasaudi mlikuwa wangapi huko.

Tulikuwa kama kumi na watano tu hivi. Baadaye tuliongezeka lakini hapo Qum nilikaa mwaka mmoja tu.

**Mwandishi:** Mungu wangu! Wewe mpenzi wa madhehebu na hukuweza kusihi mazingira ya hapo?

Nilikuwa natafuta mazingira mengine ya kiarabu na karibu na kwetu. Mwanachuoni mmoja aliyetoka Iraq alichagua kwenda Kuwait naye ni Marjaa Sayyid Muhammad Shirazi, alikwenda Kuwait mwaka 1391 (A.H.) akaanzisha madrasa ya dini, nikazuru madrasa nikapenda hali yake na nikajiunga nayo mwaka 1394 (A.H.).

**Mwandishi:** Nataka nijue mnapata wapi pesa huko kote, ulipokuwa Najaf, Qum.. je kuna pesa za watu wema au ni za Hawza? Au mkiletewa na watu wenu?

Hawza na wanavyuoni walioko ndio wanaotoa pesa kwa wanafunzi lakini kwa kiasi maalum.

**Mwandishi:** Je ni zile Khums wanazopokea?

**Sheikh:** Ndio, kutokana na Khums wanazopata hizo hupewa wanafunzi.

Marjaa anayefuatwa hupata kulingna na upana wa ufuasi wake. Yeye hutoa kiasi kikubwa au kidogo inavyotegemea, kwa mfano kuna Marjaa waliokuwa wakitoa mkate tu kila kwa siku kwa kila mwanafunzi, na kawaida mwanafunzi hupokea kwa Marjaa wane watano, na mara nyingi ilikuwa ni kama dinari kumi za Iraq kwa mwezi, na dinari moja ilikuwa ni sawa na Riyal kumi za Saudia na vitu vilikuwa bei nafuu.

Kwa wanafunzi wa Iran na Afghanistani wao ilikuwa kiasi hiki cha pesa kikiwatosha, lakini kwa wa Ghuba la Bara Arabu, kwa kuzingatia matumizi yao yako juu, walikuwa pia wakisaidiwa na wazazi wao, baba yangu alikuwa akinitumia pesa.

**Pesa na uzito wa kijamii kwa Marjaa**

Sheikh, wallahi hizi Khums zinawapa uzito Marjaa wenu na nafasi kubwa katika jamii lakini tulivyosikia ni kuwa mapinduzi ya Iran yalisaidiwa na wauza nguo waliomsaidia Khomein kumuangusha Shah..

**Sheikh:** Kweli, Khumsi kwa Shia ndio inayowasimamia Marjaaa wao na taasisi zao nayo ni fardhi ya kiislamu kama Zaka, lakini Shia wanaonelea kwamba kila anachokichuma mtu akapata faida atoe Khums (Fungu la tano) katika ziada yake.

Ama medhehebu mengie yanaonelea kwamba Aya hii inahusu ngawira ipatikanayo kwenye vita tu.

Kwa nini hukuweza kukaa Iran na ukaenda Kuwait, hiyo ilikuwa lini?

**Sheikh:** Mnamo mwaka 1394 A.H. nilienda Kuwait huko alikuwa Marjaa Sayyid Muhammad Shirazi, na alikuwa na wanavyuoni wengine, licha ya kuwa yeye alikuwa ni Marjaa wa kifiqh, lakini pia alikuwa ni mwenye mwamko wa kiislamu, uandishi wake na fikra zake zilikuwa wazi upande huu, nilifaidika sana naye, na lazima niseme kwamba upande wangu wa kifikra, kielimu na kiharakati katika maisha yangu niliupata wakati nikisoma kwa Sayyid Shirazi.

Alikuwa akifasiri Qur'an kila usiku na tafsiri yake ikitufungulia pambizo za upeo mkubwwa mbele yetu, haikuwa tu ni tafsiri ya kufuata tu na kutaja sababu za kushuka Aya au maana ya maneno, alikuwa akitoa katika Aya ufahamu wa kijamii, kisiasa na kifikra na akiwaamsha waislamu na kupinga wamagharibi na ukoloni.

Pia alikuwa na darsa kila wiki kwa juu ya tabia, vipi anavyotakiwa awe mwanafunzi katika mwenendo, nishati, tabia na kutangamana na jamii, kila wiki akichagua nukta moja na kuizungumzia hiyo kwa kina.

Tulifaidika sana, na mimi nilijifunza na kufaidika na kulelewa kuliko Hawza nyingine yoyote ile, katika zingine sikuwa nikihisi kuwa kulikuwa na mwanachuoni aliyenilea, pengine kwa kuwa umri wangu na haukuniwezesha wakati huo kuamiliana moja kwa mja na wnavyuoni wengine, lakni Kuwait ukizingatia pia idadi maalum ya wanafunzi na shakhsiyya ya Sayyid Shirazi ilikuwa ni ya ubaba na si mimi peke yangu bali wote katika kiwango hiki.Mmoja katika wanafunzi wake alikuwa Sayyid Muhamad Taqi Mudarrisi ambaye sasa ni Marjaa, huyu ndiye aliyekuwa akiongoza harakati za kiislamu ana alikuwa na uelewa wa kutosha na Hizbut tahrir,

Ikhwaanul-muslimiina, na harakati za kiislamu za Iran. Nilikuwa sijui juu ya harakati za kiislamu lakini kwenye madrasa ya Seyyid Shirazi nilielewa kuna harakati zenye lengo la kutengeneza hali ya Iraq na kuwaandaa watu waupinge utawala wa kiBaath Iraq, nikaishi katika mazingira hayo, nikafaidika sana na Sayyid Muhammad Taqi Mudarrisi na nduguye Hadi Mudarrisi aliyekuwa akiishi Bahrain na akija mara kwa mara Kuwait.

**Hali ya Kuwait, je ni kutengana au kusaidiana?**

Mimi nashangaa wewe na wanavyuoni wa Sunni nami nafuatilia uhusiano wako na masunni wa Kuwait je ni kama kawaida kuna hali ya kutengana kitaifa na kijamii?

**Sheikh:** Hali ya utangamano wa Shia na Sunni ya Kuwait ilikuwa ni ya kawaida, kwa kuwa madhehedu yaongozayo huko ni ya Malik nao hawana msimamo mkali juu ya Shia na hapo kwa mara ya kwanza niliishi kwenye anga ya uwazi ya kijamii mimi mwenyewe nilisuhudia wanavyuoni wa Kisunni wakimzuru Sayyid Shirazi naye pia akizuru majlis zao hata niliwahi kufutana naye katika baadhi ya vikao hivyo.

Pia gazeti la Kuwait lilikuwa likichapisha kitabu cha Shia na kutoa nakala za matukio ya Shia. Na kulikuwa na jarida la kila wiki la Baqir Kharibt mshia, likiitwa *Swautul khalij* ambalo tulikuwa tukilisoma na kuona masuala ya jamii ya Shia, kifupi hakukuwa na utengano wala mizozo wakati huo.

Ningependa kujua kipindi chako cha kusoma Kuwait, ni vitabu gani ulivyopendelea sana kuvisoma?

**Sheikh:** Nilikuwa naishi kwenye mazingira ya Sayyid Shirazi ya harakati chini ya madrasa inayosimamiwa na Sayyid Muhammad Taqi Mudarrisi ambaye jina lake likawa maarufu akiwa kiongozi wa chama cha Amal Islami Iraq, nacho kikishirkiana na chama cha Daa'wa cha upinzani nchini humo. Serikali ya Kuwait haikuwa ikuruhusu harakati za waziwazi.

Wakati huu niliamka na kuingia kwenye harakati, nikasoma sana vitabu vya Al-Maududi, An Nadawi, Hassan Al Banna, Seyyid Qutbi na Fathi Yakin na vingi juu ya suala la Palestina, bado nakumbuka kitabu cha kwanza kilichonipa mori ni cha Abu Ayyad Salah Khalf kiitwacho '*Falastin bila hawiyya.*'
Na wakati huo zilidhihiri harakati za Imam Musa Sadr huko Lebanon na harakati za Amal naye alizuru Kuwait, nilifurahi sana kwa kukutana naye na kusikiliza mihadhara yake. Pia kulikuwa na uhusiano na harakati zinazopinga utawala wa Shah wa Iran ambapo tulikuwa tukipata vitabu na mihadhara ya Imam Khomeini ambaye wakati huo akiishi Najaf.

Pia kulikuwa na Sheikh Muhammad Muntadhari mtoto wa Marjaa Muntadhari, hapo ndipo nilianza kufungukiwa juu ya harakati za Iran kabla ya miaka mitano ya k uangushwa utawala wa Shah.

**Mwandishi:** Ningependa kujua jinsi unavyoweza kuijua lugha ya kifursi ya Iran.

Naweza kusoma vitabu na magazeti ya kifursi hata darsa na mihadhara ya lugha hiyo. Lakini kwangu kuizungumza ni ngumu kidogo.

**Mwandishi:** Wallahi ajabu Sheikh! Watu wengi huweza kusema kuliko kusoma.

Pengine nilikuwa naishi katika mazingira ya kielimu niijuayo ya kiarabu, na wanavyuoni huko wakisomesha kwa kiarabu hivyo sikulazimika kusema kifursi wengine wakipenda kuzungumza nasi kiarabu ili waweze kukitamka vizuri, mfano Sayyid Khamenei kiongozi wa Jamhuri ya kislamu ya Iran tulikuwa tukimzuru usiku kabla hakujakuwa na vikwazo vya kiusalama, na alikipenda sana kuzungumza kiarabu.

Pia sikupenda kuzungumza kifursi kwa ajili ya kutokizungumza vizuri, na hii ni kawaida kwa lugha mpya kwa mtu, kwa hivyo huenda kwa sababu hizi mbili ndipo sikuweza kuzungumza vizuri kifursi pia kuwa na azma ndogo juu ya lugha hiyo.

**Imam Khomeini**

**Swali** lifuatalo ni juu ya mtu hatari katika historia ya Shia kwa ujumla, nakusudia ni Khomeini, je uliwahi kukutana na mtu huyu Iraq kabla hajaenda Paris?

**Sheikh:** Nilipokuwa Najaf, Imam Khomeini alikuwa akiishi hapo, alikuwa ni Imam katika msikiti ulio karibu na nyumba yake, msikiti huo ukiitwa *Masjidut-Turki* yaani (Msikiti wa Waturuki), kila siku alikuwa na majlisi akipokea wageni pia kila siku bada ya Swala ya Isha alikuwa akienda maqam ya Imam ali (a.s.) kwa wakati maalum.Na nilisikia wanafunzi na wanavyuoni wakimsifu juu ya kuchunga kwake wakati. Alikuwa akifika huko kwa wakati maalum bila ya kuchelewa au kufika mapema sana hivyo kwa mwaka mzima.

Nilikuwa nikiswalishwa na yeye kwa baadhi ya siku na nilimtembelea zaidi ya mara moja kwenye kikao chake nikiwa kama mwanafunzi wa dini bila ya kuwa na uhusiano wa moja kwa noja naye au na watu wake. Kwani nilikuwa ni mwanafunzi mdogo sikuweza kuwa na uhusiano mkubwa naye.

Na katika wakati huo ndipo ikatokea rai yake ya kusimamisha serikali ya kiislamu, na vikachapishwa vitabu vitano juu ya suala hili. Ikawa ni rai mpya kwenye Hawza za kidini na ikawa ni mjadala, lakini Imam Khomeini alikua ameshikilia maoni yake niliyasoma maoni hayo kwenye anuani '*Al-hukumatul Islamiyya wawilayatul faqih.'*

**Mwandishi:** Aliyoyafanya Khomeini ni fikra pana kwa madhehebu ya Shia na hasa fikra hiyo ilikuwa ni njia ya kuondoa mataizo makubwa yaliyowakabili Shia, na kuwafanya kuingia siasani bila ya kumngoja Mahdi aliyeghibu, je waweza kutufafanulia?

Mwelekeo uliokuwako wakati huo ni kutoingilia siasa, na mwanachuoni wa kidini, wajibu wake ulikuwa ni kusomesha elimu ya dini tu, na kufutu mas'ala ya kidini ya watu wake tu.

Na wakaona kuwa maulama wao kuingia mambo ya siasa ni kutojishughulisha na kazi zao za dini, na pia ni kupambana na serikali ambayo itawaona kama ni wapinzani wao. Pia ilionekana kuwa katika siasa kuna aina fulani ya kutokuwa na ucha Mungu na upaji nyongo aanaohitajika kuwa nao mwanachuoni, lakini hilo halikuwazua wao kupambana kwa nguvu na ukoloni wa kigeni kama ilivyotokea Iran kwenye suala la waingereza juu ya tumbaku na vita dhdi ya Urusi.

Pia Iraq juu ya kupinga utawala wa kiingereza ambapo wanavyuoni waliongoza mapinduzi ya mwaka 1920 yaliyoishia kuwafukuza waingereza.

Ama inapotokea dhulma katika siasa za ndani, wanavyuoni walisimama kuwapa nasaha zao viongozi. Na wao wana tahadhari sana kusitokee umwagaji damu au uvunjaji wa heshima au kutokea fitna nchini.

Na wengi walionelea kuwa serikali ya kiislamu haisimami ila kwa mkono wa Imam anayengojewa, lakini Imam Khomeini aliwapa changamoto wanavyuoni ya kusimamisha serikali ya kiislamu, na wasiwaachie mambo hayo ya wasilamu wale wanaofuata wamagharibi, kwa kupinga Uislamu, na kwamba wasingojee kuja kwa Imam Mahdi, kuna waliomtangulia kutoa rai hii kama Sheikh Mahdi Nafi aliyefariki mwaka 1244 A.H. lakini yalibaki kwenye maoni ya kielimu tu.

Imam Khomeini akaichukua rai hii na kuifanya iwe ni yenye kutumika kisiasa na ilihakikishwa wakati wake kwa kuanzisha jamhuri ya kiislamu ya Iran.

Swali linalojiuliza lenyewe ni je, hiyo kusimamisha hukmu ya kisheria katika Fiqh ya Shia imefungika katika utawala wa mwanachuoni aliouchukua Imam Khomeini?

Iko rai nyingine juu ya uwezekano wa utawala wa kisheria kwa umma kuchagua viongozi wake alieleza Sheikh Naibi (1277 – 155 A.H. ) kwenye risal`ayake iitwayo '*Wilayatul umma ala nafsihi.*'

## Hali ya mashia wa Lebanon

**Mwandishi:** Linapotajwa jina la Muhammad Mahdi Shamsu din linakuja swali la hali ya mashia wa Lebanon, naona iko tofauti na ya wa Iraq, Kuwait na Iran, wao ni mfano wa kipekee wa kusameheana na kuishi pamoja na uwazi, nami nahisi kuathirika kwa Hasan Saffar na Madrasa ya Lebanon, je uko pamoja nami juu ya hili, na kwa nini iwe Lebanon pekee?

Maumbile ya jamii ya kilebanon na ushirkiano wao katika utawala kiasi ambacho hakuna kundi linalotawala wengine, kumewafanya walebanon wawe wanakubali kuishi pamoja. Wanavyuoni na wanafikra wao wameenda na hali hii kiasi ambacho lau muislamu atamkosea mkristo basi taasisi za kiislamu ndio zitakuwa za mwanzo kukemea na hivyo hivyo kwa wakristo. Kimadhehebu pia mshia wa huko akimkosea msunni basi baraza la kiislamu la Sunni litakuwa la kwanza kumkemea na hivyo hivyo Shia.

Kweli nakubaliana nawe na nakiri kuwa niliathirika na madrasa ya Lebanon na hasa fikra za Sheikh Muhammad Mahdi Shamsu din ambaye nilikuwa na uhusiano naye hasa na mara nyingi nikimzuru mara nyingi ajapo Syria au nikienda kwake na kila alipozuru Saudia kwa Hijja au vikao aliniarifu kabla nikaenda kumuona Jeddah au Madina au Riyadh. Ama simu pia tuliwasiliana naye mpaka alipokuwa mgonjwa Paris na siku mbili kabla ya kufariki kwake Beirut.. Nilisoma na kujadiliana naye kwa urefu juu ya maandishi yake.

Nilipomuonyesha kitabu changu '*At-taaddudiyya wal hurriya fil islam*' alifurahi sana na kuandika utangulizi na hiyo ni dalili ya ushujaishaji wake juu ya hili.

Nilikutana na Sheikh Shamsu din miaka mitano iliyopita tukampokea na Ustadh wangu marehemu Dkt. Abdul Qadir Tash katika idhaa ya Iqra. Maoni yake yalikuwa juu ya umoja na kuishi pamoja na hivi sasa twasikia hayo hayo kutoka kwa Sheikh Muhammad Husein Fadhlu llah, je utatueleza sababu za maendeleo haya ya masheikh wa Lebanon?

**Sheikh:** Juu ya haya kama nilivyoeleza na nawafikiana nawe juu ya sababu mbili za kimsingi:

Kwanza: Daraja ya juu ya fikra wazi wanazoishi watu wa Lebanon, uko mwanachuoni wa dini huchukua pia fikra zingine na hukutana na mielekeo tofauti na huisihi akichunga maslahi ya jamii nyingine. Ama Iran na Iraq hali haikuwa katika daraja hiyo.
Pili: Iran na Iraq kuna taasisi za kidini zinazoongozawa na Marjaa na Hawza za kdini na hazikubali fikra mpya. Ama Lebanon hakuna taasisi za kidini zinazopinga fikra za mageuzi na kuacha mambo yaliyozoeleka.

## Tofauti ya Sunni na Shia

Hebu sasa Sheikh utueleze juu ya tofauti za kimsingi za madhehebu ya Sunni na Shia.

**Sheikh:** Tofauti kubwa ni suala la uimamu na marejeo ya uongozi wa kidini (*marjaiyya*). Hivyo ni kwa sababu uimamu kwa Shia uko katika pande mbili: Uongozi wa kisiasa, ukhalifa. Shia wanaamini Imam Ali alitajwa kwa ya uongozi, alitajwa na Mtume (s.a.w.), Na kwamba yeye alikuwa ni bora zaidi kwa uongozi, na baada yake ni maimamu wa Ahlu bayt, lakini hili ni siala la kuhistoria

Ambalo lahitaji kujadiliwa, maadam tofaui ya mwenye kuwa na haiki hiyo ni ya kimaoni na kifikra basi halihitajii kuzozana. Upande wa pili ni uongozi wa kidini (*marjaiyyah*), ambapo hapo hupatikana maongozi ya kidini na sharia baada ya Mtume (s.a.w.)

Sunni wanaonelea kuwa yafaa tuchukue sunna kutoka kwa maswahaba, na tujifunze kwao yale mambo yenye kukanganya katika Qur'an.

Ama Shia wanaonelea kuwa marejeo yabaki kwa Ahlul bayt tu, wala hawachukui yanayokwenda kinyume na wao, na hii wanafuata amri ya Mtume (s.a.w.) kama ilivyo katika vitabu sahih na Hadith zinazotegemewa.

Ametaja Muslim katika Sahih yake: Hadith Na. 2408 Kutoka kwa Zaid bin Arqam amesema: "Mtume alisimama mahali paitwapo Khum, kati ya Makka na Madina, akamhiidi na kumtukuza Mwenyezi Mungu, akatoa mawaidha na akasema: "Enyi watu! Mimi ni mwanaadamu na huenda akatumwa mjumbe wa Mola anijie nami nimuitikie, Mimi nawaachia vizito viwili, Cha kwanza ni kitabu cha Mwenyezi Mungu humo mna uongofu na nuru, basi chukueni kitabu cha mwenyezi Mungu na mshikamane nacho., kisha akasema: "Na ahlu bayti wangu nawakumbusha kwa Mwenyezi Mungu kuhusu Ahlu bayt wangu, nawakumbusha kwa Mwenyezi Mungu kuhusu Ahlu bayt wangu, nawakumbusha kwa Mwenyezi Mungu kuhusu Ahlu bayt wangu.
Ametaja Sheikh Muhammad Nasrudiini Al-Albany katika mfululizo wa Hadith sahih Juz. 4 Uk. 355. Hadith Na. 1761 amesema Mtume (s.a.w.): "Enyi watu! Hakika ninawaachia vitu ambavyo lau mtashikamana navyo hamtapotea: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Ahlu bayti wangu."

Na akasisitiza Al-Albany kuwa Hadith hii ni sahih kwa njia nyingi na ana ushahidi kwa Hadith zingine na akamjibu yule anayeifanya kuwa ni dhaifu Hadith hii.
Ametaja Tirmidhi na Tabrani, Imam Ahmad na wengineo kwa Hadith hii ndipo Shia walifahamu kwamba Mtume alipanga kurejelea kwa Kitabu na Ahlu bayt wake baada yake, na kwamba yeye ataondoka duniani na kuwaachia umma vitu hivi viwili na kuchukua miongozo kutoka kwavyo pekee ndio kujiepusha na upotevu.
Hapo ndipo iko hitilafu kati yao na Sunnina ndipo vikatokea vitawi vingi katika akida na Fiqh ambapo Sunni wanachukua kutka kwa baadhui ya maswahaba na tabiina, na Shia hawachukui ila kutoka kwa maimamu wa Ahui bayt au yae yanayowafikiana na hayo.

Ama riwaya ya Sunni isemayo kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna yangu,' hiyo hikuthibiti kwa Shia, Ibn Hajar Al-Haithami ametaja katika '*Sawaaiqul muhrqa*' kuwa kuna wajhi wa kukusanya baina ya Hadith mbili hizi.

**Mwandishi:** Naam Sheikh, lakini nijuavyo katika maudhui haya ni kuwa Sunni hawajasema katika maudhui haya kwa kuwa ni kwa ajili ya kuwa Swahaba ni katika Ahlu bayt au wengineo, bali ni kwa ajili ya elimu na ubora, kwa hivyo wamepokea kutoka kwa Ali, Abbas, Jafar Sadiq, Zainul abidina na wengineo, nitaacha maudhui haya na niende kwenye kutaka ufafanuzi juu ya maudhui mengine ya hitilafu.

Baki ya maudhui ya hitilafu ni ya kimatawi, ameandika Seyyid Murtadha Al Askari cha Juzuu mbili kiitwacho *Maalimul madrasataini*' ametaja misingi ya kila madhehebu, ya wafuasi wa maswahaba na wafuasi wa Ahlu Bayt.

Kwanza: Tunapozungumza juu ya Ahlu Bayt, ni juu ya wale aliowapanga Mtume (s.a.w.) kama alivyopokea Imam Ahmad na Tirmidhi na wengineo. Na Sheikh Ibn Taymiyya pia amenukuu katika '*Huquuq ahlu bayt*' kuwa: "Imepokewa kutoka kwa Ummu Salama Aya hii: "Hakika Mwenyezi Mungu anataka awaondolee uchafu enyi watu wa nyumba ya Mtume na kuwatakasa kabisa," iliposhuka, Mtume alizungusha shuka yake kwa Ali, Fat*i*ma, Hasan na Husein, akasema: "Ewe Mola! Hawa ndio Ahlu bayt wangu, basi waondolee uchafu na uwatahirishe kabisa." Kisha Ibn Taymiyya ameongeza: "Sunna yake inafafanua Kitabu cha Allah na kukibainisha na kutoa dalili. Aliposema "Hao ndio Ahlu bayt wangu" mtiririko wa Aya waonyesha kuwa ni wakeze, licha ya hivyo lakini hao (Ali, Fatima Hasan na Husein) ndio wapaswa zaidi wawe ni Ahlu Bayt wake kwani uhusiano wa nasaba una nguvu zaidi kuliko wa kuoana."

Pili: Mapokezi ya Ahlu bayt katika marejeo ya Sunni ni nisba ya ilivyopokewa na wengine, pengine hiyo yarejea kwenye hali za kisiasa walizokuwa wakiishi Ahlu bayt, kama tukichukua Sahih Bukhari kama mfano, tutatapata kuwa Ibn Hajr Al asqalani katika utangulizi wa *Fat-hul baari* anataja mfano wa namba zifuatazo: Idadi ya Hadith zilizopokewa kutoka kwa Sahih Bukhari kutoka kwa Anas bin Malik ni 268, na kutoka kwa Abdallah bin Umar ni 270, Abu Huraira ni 446 , Ummul muninina Aisha ni 242, ama Imam Ali bin Abi Talib ni 29 na Bi Fatima ni Hadith moja.

**Mwandishi:** Hebu twende kwenye maswala yanayogusa hisia za Sunni kama vile kuwatukana maswahaba, msahafu wa Fatma, sijui Sheikh vipi nimkubali Shia anayewatukana maswahaba wa Mtume (s.a.w.) hebu fafanua Sheikh.

**Sheikh:** Nimejadiliana na masheikh wengi wa Sunni wa miji mbalimbali, na nimekutana na ulama wengi wa kishia wanaofanya juhudi ya kuwa na ukaribu kati ya waislamu, nikaona kuwa matatizo ya Sunni wanayolalamikia Shia yanasababishwa na moja kati ya sababu zifuatazo: Kutokukubali ukweli wa hitilafu ambapo Sunni wanawalaumu Shia kwa kuwa rai zao zinazowapinga kama kwamba Shia yawapasa kukubaliana na rai zote za Sunni ama sivyo walaumiwe. Jambo ambalo ni lazima lieleweke ni kwamba, kuna madhehebu mbili zinazowafikiana katika misingi ya dini, lakini zinatofautiana katika maelezo ya kiakida na kifiqhi. Kama ilivyo hali ya kutofautiana ndani ya madhehebu ya Sunni kati ya Ashaira, Mutazila, Salafiyya na Sufi.

Ama kusema kwamba ni lazima kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna hilo lakubaliwa na wote, lakini kuna tofauti ya kufahamu na kukubali baadhi ya mapokezi.

Na baada ya karne kumi na nne za migogoro na kujishughulisha na hitilafu ni lazima sasa tukubali kuwa kuna madhehebu mengine, na kuwa kuna ukweli wa kuhitilafiana, na tujaribu enzi mpya ya kuwa pamoja na kupeana heshima.
Jambo la pili: Kuzilaumu rai za kipekee kwa wote. hapa nakubali kuna baadhi ya Shia mathalan wanaudhi wengi kwa kuwatukana maswahaba ama kwa kutofahamu ama kwa kujibu mashambulizi ya muamala wa kisunni kwao wao haifai tulaumu madhehebu yote kwa hilo, kama ni hivyo ingefaa watu wa magharibi walaumu waislamu na waarabu wote kwa kufanya ugaidi.
Tatu: Kufahamu vibaya ukweli wa rai za Shia kwa kusudi au si kwa kusudi, au pia kwa kukosa kusoma

au kwa kusikia maneno, kwa mfano sisi hapa Saudia vitabu vya Shia haviruhusiwi kuingia wala hawana fursa ya kutoa maoni yao katika vyombo vya habari, na baadhi ya wanavyuoni wa kisunni hawataki kujisumbua kusoma marejeo ya vitabu vya Shia vinavyotegemewa, ndipo wakabaki na picha mbaya ya Shia.

Wakati mmoja nilimuuliza mmoja kati ya makadhi wa Qatif kama amesoma marejeo ya fiqh ya Sunni juu ya uwanja wake wa ukadhi na hali ya kuwa yeye ni kadhi katika eneo la mashia na kuna mambo ya maisha yao, mipaka na mizozo. Akanijibu kwamba hajasoma kwa sababu hana wakati wa kutosha na hana haja ya hilo.

Mfano mwingine ni juu ya wanaosema kuwa Shia wameipotoa Qur'an ambapo vitabu vya Shia vya tafsiri Fiqh na itikadi vinaeleza wazi kabisa kwamba Qur'an imehifadhiwa na kupotoshwa ambapo matukio katika matangazo kielimu na kijamii hawana Qur'an nyingine ila hii waliyo nayo waislamu idhaa zao inasomwa hiyo hiyo na katika Swala zao yasomwa hiyo hiyo, watoto wao wanasomeshwa hiyo hiyo, riwaya zilizoko katika vitabu vya Shia juu ya upungufu katika Aya za Qur'an pia kwa Sunni zipo,na kama Sunni wamepata matokeo kuwa kuna *naskh*, hiyo ni sahihi.
Kuna rai ya baadhi ya wanavyuoni wachache wa Shia wamekubali riwaya hizo na wakasema kuwa zipo zilizonasikhiwa lakini wanavyuoni wa Shia wengi wamepinga hilo na wakatunga vitabu juu ya suala hilio kwa nini basi tukariri na kung'ang'ania shubha hizi?

**Mwandishi:** Nikukate kidogo sheikh, je waweza kutupa majina ya mashia waliosema hivyo ili tuweze kulinganisha, kutoa hoja na kukubali mpaka...

**Sheikh:** Ulama wa Shia waliosema kuhusu kuwa Qur'an imehifadhiwa na kupotoshwa na kupunguzwa na wakaikataa riwaya zisemazo hivyo ni wengi vigumu kudhibiti idadi yao lakini nitataja baadhi tu:

Sheikh Saduq, Abu Jafar Muhammad bin Ali bi Husein (aliyefariki mwaka1381 A.H.) amesema: "Imani yetu juu ya kwamba Qur'an aliyoiteremsha Allah kwa Mtume wake ni ile ambayo iko mikononi mwa watu hakuna zaidi ya hiyo, na anayesema kwamba sisi tunasema kuwa kuna zaidi ya hiyo basi huyo amesema uongo..."

**Mwandishi:** Vizuri. Yote uliyoyasema lakini Sheikh, nachanganyikiwa ninayoyasikia kutoka kwako na aliyosema Al-Kualyni katika Usuulul kafi (2381) kutoka kwa Jafar bin Muhammmad amesema: "Hakika sisi tuna mas-haf ya Fatima mbayo ni mas-hafu kama Qur'an yenu hii mara tatu, wallahi hakuna yaliyomo katika Qur'an yenu hata herufi moja. Nawe wasema kuwa hakuna katika sisi anayesema kuwa mashafu ya Fatima ni Qur'an nyingine? Je hapa ni mgongano ama ni kusahau kwako?

Riwaya zilizomo kwenye Al-Kafi si dalili ya kuwa Qur'an imepotoshwa au kuna Qur'an nyingine, bali zazungumzia kitabu cha Fatima umbo lake linalingana na la Qur'an mara tatu lakini hakuna kitu cha Qur'an humo.
Na hii ndivyo walivyosema masheikh wa Shia kama Sheikh Majlisi katika *Miraatul uquul* na Mazandarani katika *Sharh Usuulul kaafi* zimekuja riwaya 8 katika mlango huu kwenye *Al-Kafi,* Majlisi amezisahihisha mbili amesema mbili ni *hasan* na nne ni *mursal*, Na ya pili ni *dhaif* ya tatu na ya nne ni *majhul* sanad yake.

Inaeleza wazi moja ya riwaya hizio kuwa mas-haf ya Fatima ni riwaya alizozisikia Fatima na kumsomea Ali naye akamuandikia. Riwaya nyingine yaonyesha kuwa mas-haf ya Fatima kwamba katika maisha ya Fatima hakuna Qur'an bali ni ilimu ya kidini ambapo Imam Jafar Sadiq amesema: “Mas-haf ya Fatima sidai kuwa ndani yake mna Qur'an, ndani yake mna wanayoyahitajia watu kwetu sisi na hatuhitaji yeyote.”

Imekuja katika riwaya nyingine: Kwamba mas-haf ya Fatima ni wasiya na watoe mas-haf ya Fatima kwani mna ndani yake wasiya wa Fatima (a.s.).

Kwa hivyo hakuna katika riwaya hizi ishara ya kuonyesha kuwa kuna kupotoshwa au kuwa hiyo ni badili ya Qur'an pengine mkanganyo umekuja kwenye hilo jina la Mas-haf ya Fatima! Kwa kuzingatia jina msahafu i la Qur'an..

Tukirejea kwenye vitabiu vya lugha tutakuta kuwa kila kitabu kilichokusanywa kilugha ama huitwa mas-haf kama ilivyo katika *Lisanul arab* na katika *Qamus* na *Sihah*.

Ametaja Al-Hafidh Abu Bakr bin Abi Daud Sajistani (aliyefariki mwaka 316 A.H.) katika kitabu chake Al masahif, akataja mfano Khalid bin Midan katika wanavyuoni wakubwa wa Sham na tabiina ilikuwa ilimu yake kwenye msahafu wenye izar.
Na nimesoma kitabu cha Dkt. Nasir din Al-Asadi kiitwacho *Masaadirus-shi'r al jahily* nikapata akisema: “Walikuwa wakiita mkusanyiko wa kitabu kwa jina la msahaf wakikusudia mkusanyiko wa kitabu. Si Qur'an pekee kwa hivyo kuitwa mas-haf ya Fatima ni kwa sababu hii tu ya kilugha.

## Bali ni Qur'an kamili

**Mwandishi:** Sheikh, aidha ijmai ya Sunni juu ya ukamilfu wa Qur'an haikupungua hata herufi moja hiyo wamekubaliana tangu zama zilizopita kwetu hakuna kama ulivyosema hivi punde.

Waislamu hawawezi kutuhumu kuwa Qur'an utukufu wake kuwa imepotoshwa, Sunni wanatuhumu Shia kwa hilo, na Shia wanatuhumu Sunni pia kwa hilo na hii ni fursa ya kutia shaka walioitumia fursa hii wale mustashrikiina na wanoupaka matope uislamu

Nami najua kuwa Ijmai ya Sunni na Shia yakubaliana juu ya Qur'an na kwamba haijapungua hata herufi moja kama ilivyo katika vitabu vya Shia riwaya ya upungufu ina upotofu pia vilevile katika vitabu vya Sunni lakini kwa nini Sunni hawakubali maelezo ya riwaya zetu na wengine kutuelekezea tuhuma kwetu?

## Tatizo pekee na gumu

Kadhiya ya msahafu wa Fatima umeifafanua kwamba Qur'an yenu ndio hii hii yetu lakini suala la kuwatukana mswahaba na kumtukana Sheikh wa waislamu Abu Bakr (r.a.) na Umar hili ndilo suala tata kati ya Sunni na Shia, utatueleza nini hapo.

Kutukana si katika hulka ya muislamu wala ya mwenye akili, nami nakataa tabia ya kuwatukana makhalifa na maswahaba, na naamini hii ni sehemu tu ya historia mbaya waliyoish nayo waislamu, kulikuwa na utawala uliokuwa ukiwakandamiza Mashia,

ikawa majibu makali ya shia ni kutukana maswahaba na ni lazima tukubali kwamba dola ya kiamawi ndio iliyoweka matukano kwa kumtukana Ali bin Abi Talib juu ya mimbari.
Ametaja Muslim katika Sahih yake: Muawiya alimuamuru Saad bin Abi Waqas, na akamlaumu kwa kukosa kumtukana, kama ilivyokuja katika mlango wa Fadhail Ali.
Imepokewa kuta kwa Amir bin Saad bin Abi Waqqas, kutoka kwa baba yake, amesema: "Muawiya bin Abu Sufiyan alimwamuru Saad akasema: "Nini kilichokuzuia usimtukane Abu Turab?" Akajibu: "Je hukumbuki matatu aliyoyasema Mtume (s.a.w.) juu yake? Sitamtukana (Hadith). Lakini ajabu ni kwamba baadhi ya watu wanajaribu kuiawili Hadith hii kwamba haionyeshi wazi amri ya Muawiya ya kumtukana Ali.
Imekuja katika Sunan Ibn Maja ya Al-bani Hadith Na. 98, kutoka kwa Saad bin Abi waqas amesema: "Alikwenda Muawiya katika baadhi ya Hajj zake akaingia Saad kwake, wakamtaja Ali. Muawiya akamtukana (Ali). Saad akakasirika akasema: "Juu ya mtu huyu nilimisikia Mtume (s.a.w.) akisema: "Atakayekuwa mimi ni bwana wake basi na Ali pia ni bwana wake." Na nimemsikia Mtume akisema: "Wewe (Ali) kwangu daraja yako ni kama alivyokuwa Haruna kwa Musa, ila tu hakuna mtume baada yangu."

Na nimemsikia akisema: "Kesho nitampa bendera mtu anayempenda Mwenyezi Mungu na mtume wake." Na inavyojulikana katika historia khalifa Umar bin Abdul Aziz ndiye aliyeondoa kumtukana Imam Ali.
Imekuja katika *Tarikh dawlatul amawiyyah* kitabu cha Sheikh Muhammad Al-Khadhari anayetegemewa sana katika somo la historia katika vyuo vikuu vyetu vya Saudia:

Moja katika kazi zake kubwa alizozifanya Umar bin Abdul Aziz ni kuacha kumtukana Ali bin Abi Talib juu ya mimbari, Bani Umayyah walikuwa wakifanya hivyo, akaliacha na akawaandikia kwenye miji waliache mahali pake akaweka maneno "*Innallaha yaamuru bi a'dli wal-ihsaan.*

Na imekuja katika Musnad ya Imam Ahmad bin Hambal Hadith Na. 28284, kutoka kwa Abi Abdalla Al- Al Jadaly, amesema: "Niliingia kwa Ummu Salama, akaniambia: "Je Mtume anatukanwa kwenu?" Nikasema, Mungu apishe mbali! Akasema: "Nimemsikia Mtume (s.a.w.) akisema: "Anayemtukana Ali, basi amenitukana."

Ikiwa Ali daraja na ubora wake kwa Shia halinganishwi na yeyote baada ya Mtume na licha ya hivyo anatukanwa na kulaaniwa katika mimbari miaka na mashekhe wa Sunni wamenyamaza hilo linasabaisha wengine pia kuthubutu kuwatukana maswahaba wengine na makhalifa kama ambavyo haikubaliki sababu za kufaa kuwatukana masheikh wawili Abu Bakr na Umar, pia haikubaliki kumtukana Ali ati kwa sababu yeye alijitahidi na akakosa.

Na yapasa iwe hukmu ya kuwatukana makhalifa na maswahaba ni moja, ama iwe kumtukana Ali ni ijtihadi ya makosa, na kuwatukana wengine ni kufru! Hii si sahihi kabisa ki-mantiki nami sikusudii maneno yangu haya kwa kumuunga mkono anayewatukana makhalifa na maswahaba ila natoa mwito wa kuifahamu hali ya kutokea hayo ambayo tuyawache kwa kuweka uhusiano mzuri, baina ya pande mbili za Sunni na Shia mpaka tuheshiminane.
Katika mashia wanaowatukana masheikh wawili Abu Bakr na Umar hao hawajui,

Kwa sababu hali halisi ya kishia haikubali hilo ukiangalia idhaa za Redio na Televisheni za Shia za Iran, Lebanon na Iraq zathibitisha hilo. Kuna pia hotuba zao za ijumaa na magazeti yameenezwa kila mahali na hakuna kitu kama hicho.Bali ilitokea mwaka huu kwamba Sheikh Yakub Rastikari alichapisha kitabu alichowakejeli masheikh wawili, basi akafungwa na serikali ya Iran.

**Makhawariji au Maamawy?**

Samahani, hapa kuna mkanganyo wa kihistoria. Je walioanza kutukana a maswahaba si Khawarij waliomkufurisha Ali na Uthman, kisha Shia wakaichukua hii na kumtetea Ali na kumtukana Uthman, Abu Bakr na Umar ikaenea hiyo mpaka ikawa maarufu kisha yakaja ya Muawiya kumtukana Ali.

**Sheikh:** Makhawarij ni kikundi kichache kilichokataliwa na Sunni na Shia na kuwatukana Ali na Uthmani kwao hakukuwa na nguvu hivyo. Lakini Muawiya anayetukuzwa na ndugu zetu masunni, alifanya hilo ni la lazima, na kumwadhibu anayelipinga kama alivyomlaumu Saad bin Abi Waqas. Sipendi kuzungumza suala hili sana kwa sababu si mtu mwenye kushughulika na migogoro.

Lakini tena sikubaliani nawe kuwa Sunni wanamtukuza zaidi Muawiya, bali wanamchukulia kuwa ni mwandishi wa wahyi, na alikuwa ni swahaba kabla ya ushindi wa Makka na wanaitakidi kuwa hakuwai bora kuliko Ali, na kwamba Ali ni mwenye haki na Muawiya ni mwenye makosa sasa kutukuza kuko wapi?

**Sheikh:** Sunni wako huru wakimtukuza Muawiya

wasimtukuze, silaumu, nasema kuwa wao wanaona sawa Muayiwa kumtukana Ali na mara nyingine wanaona ni ijtihadi yake akakosa na mara nyingine ni mambo ya kisiasa, basi pia wasione makosa kwa mashia wanaowatukana masheikh wawili.

**Mwandishi:** Nakuuliza tena juu ya msimamo wako juu ya kuwatukana maswahaba.

Sipendi kuingilia maswala haya sana lakini kutukanwa Ali juu ya mimbari kuliendelea mwaka wa 41wakati wa Muawiya mpaka alipotawala Umar bin Abdul Aziz mwaka 99 A.H. Ama msimamo wangu kibinafsi nimeeleza mara nyingi katika mahojiano na idhaa mbaimbali na magazeti kuwa mimi napinga hilo.

**Mwandishi:** Licha ya kuwa katika mtandao wa Tovuti (*Internet*) kuna kipande cha sauti yako wewe kushambulia baadhi ya maswahaba wa Mtume (s.a.w.)?

Kipande hiki cha sauti kinaletwa na kikundi adui kwa Shia, marejeo yake si ya kuaminika, ni rekodi ya kutengezwa hii inajulikana kimataifa ni lazima ichunguzwe kwanza na kuthibitishwa rekodi yoyote inayonasibishwa na mtu, mazungumzo ya Saddam kabla ya kushikwa, au rekodi ya Bin Ladin au Dhawahiri, basi pande zingine huchukua fursa ya kuthibitisha usahihi wa mhusika kama kawaida inavyotangazwa, pamoja na kuwa wao ni watu mashuhuri. Nami natangaza kuwa sihusiki kamwe na rekodi hii na nataja kauli ya Mwenyezi Mungu: "Akiwajia fasiki na habari.."

**Mwandishi:** Ee Sheikh, ukiwa Muislamu umepata ufanisi kwa kutowatukana maswahaba na waliona hilo

ni haram, halifai, maadam huu ni msimamo wako, alhamdu lillah, imedhihiri kuthibitisha kwako kuwa uharamu huu kutoka kwako, pengine anaweza kuja msomaji akasema, Sheikh hakusema hivyo kamwe katika majibu yake kuwa ni haram kufanya hivyo.

**Sheikh:** Niliyoyatangaza na kuyataja yako wazi kabisa kutokana na kukataza, lakini mimi najiuliza kwa nini wanang'ang'ania baadhi ya watu daima kuwaweka Shia katika tundu la tuhuma, na kwamba yawapasa wao siku moja wajitoe katika wanavyowatuhumu kwa wanayowanasibishia, wakati ambapo fatwa na rai za kuwakufurisha mashia watu wanajifanya hawazijui, zinahimizwa na kushujaishwa juu ya kuvunjiwa haki zao, za kibinaadamu, hivi juzi tu kwa nini anajitokeza mmoja katika walinganiaji mashuhuri katika idhaa mashuhuri ili azungumzie ukafiri wa mashia wanaosema kuwa Jibril alikuja na utume kwa Ali lakini akakosea au kuhini na kumpa Muhammad.

Hebu niambie-kwa Mola wako!- ni mashia gani hao wanaotajwa? Na katika rejea gani katika rejea zao kumesomwa uzushi huu? Je huku ndiko kuwaumbia watu majibu ya kuleta farakano na dhana mbya ila ya kuwa na dalili? *Subhaanak!* Huu ni uzushi mkubwa.

Kabla hatujafunga faili hili inaonekana maneno ya mmoja wa walinganiaji wa masunni yako wazi kuwa mashia wanajulikana kwa kuwatukana maswahaba, mpaka dola zao zilizotawala za shia kama vile Bahwiyya na Swafwiyya zilifanya hivyo na haikuishia kutukana tu, bali pia kukufurisha, miongoni mwayo ni aliyoyaandika Khomeini katika kitabu chake '*Kashful asraar*,' Uk.16, 127, 130, 137 na 176

Ni matusi makuwa, shutma na tuhuma.Na katika kitabu cha kilichoandikwa na Muhammad Ridha Ridhwi chenye anuani, *kaddhabuu a'la shia,* Uk. 210 kwamba ukhalifa katika Uislamu ulikuwa ni hadaa kwa Uislamu na vitimbi, na kwmba Swala na Swaumu zao zote zilikuwa ni unafiki na upotevu tu. Je Sheikh, hapo una maelezo?

**Sheikh:** Sioni kama kuna haja ya kueleza kitu juu ya Maneno haya. Kusema kwamba mashia wanajulikana kwa kutukana ni maneno yanayokadhibishwa na ukweli ulivyo wa hali unayosihi wewe sasa na wenzako kama wewe na unayoiona wazi. Mashia wa Iran sasa hivi wana dola inayotawaliwa na wanavyuoni kwa kiasi cha robo karne sasa, ni katika madola yenye nguvu na wana nyenzo za habari na mawasiliano ya kimataifa kama vile katika lugha mbali mbali na uhusiano wake na dola zingine haukuwa mzuri wakati wa vita yao na Iraq.Je wairan walikuwa wakiwatukana maswahaba?Je mlipata katika matangazo yao ratiba za kutukana maswahaba?

Mashia wa Lebanon ni taifa kubwa na ni wenye harakati zenye nguvu, waliwashinda sana mazayuni na kulazimika mazayuni kuondoka kusini mwa Lebanon, na wana idhaa kubwa kama vile Al-Manar, je mmewahi kuwasikia wakiwatukana na kuwashutumu maswahaba na makhalifa?Mashia wa Iraq, baada ya kukandamizwa kwa vipindi vitatu wamejikwamua kutoka katika udikteta na yote yaliyowapata ya mashambulizi yaliyolenga nembo zao za kidini, na maadui kuleta fitna ya utaifa; je mmesikia Marjaa wao Iraq au uongozi wao wa kisiasa au vyombo vyao vya habari vikitukana?
Ama kuhusu maneno yanayonasibishwa na Imam Khomein katika *Kashful asraar*, mimi sijakisoma kitabu hicho,

Lakini nilisoma juu ya kitabu hcho kwamba ni cha zamani na alikitunga alipokuwa anaingia ujanani kisha alikataa kuchapishwa tena kabla na baada ya mapinduzi ya kiislamu. Dkt. Ibrahim Shatta Dusuqi, kutoka Misri, ambaye ni bingwa katiKa lugha ya kifursi, ameandika kuwa tafsiri ya kitabu hicho katika lugha ya kiarabu imepotoshwa sana na si sahihi.

Kwa kweli siwezi kukanusha kuwa katika mashia hakuna kinachotukana na kushutumu na kuwa wana vitabu juu ya maudhui haya; lakini ni vichache na vyenye athari ndogo, na wao kufanya hivyo kumesababishwa na kuakisi kwao kwa wale wengine wanaopinga shia. Watu wenye mwamko ni lazima wafanye kazi ya kuondoa umma kutoka kwenye vitendo hivi viovu na majibu mabaya yanayoakisi wale wanaofanyiwa ubaya.

Wakati unapopendekeza kuwe na mkuruba na mazungumzo na kuusahihisha uhusiano baina ya pande za umma huu, iwe ni kwa kuokoa uwanja wa kiislamu usivunjwe na waharibifu wa pande mbili.

**Mwandishi:** Sheikh, tumemaliza mkondo uliopita ulipozungumzia juu ya aliyoyaandika Khomeini katika *Kashful asraar*, na kwamba hujakisoma. Kadri tulivyoingia katika tofauti za kiakida na kutofautiana kifikra kwa karne nyingi, yaonekana Sheikh, nami nikiwa naishi katika zama hizi zenye utata nasikia ghera moyoni ya mwananchi na Muislamu, ningelipenda nikuulize juu ya njia ya kujikwamua kutokana na vichochoro hivi vya kihistoria, ili tuweze kufika nukta ya kukutana kati yetu sisi na nyinyi, nazungumza hapa kwa mustawa wa watu na si kwa kiwango cha utawala kwani adui amejikita na anangoja tuanguke tu....

**Sheikh:** Nia ya kujitoa kwenye vichochoro hivi vya kihistoria iko wazi kabisa, ni kuchukua heshima ya kiislamu ya kuamrisha uadilifu na wema na kuheshimu haki za wengine. Pia kujifundisha kutoka kwa jamii zingine zinazoamiliana vyema kidini, sisi si umma pekee unaohitilafiana katika madhehebu, mayahudi, wakristo, makalasinga, mabaniani na mashanti, wote hao wa dini mpya na za zamani wana madhehebu mbalimbali, tuangalie wanavyoishi pamoja, na tujichukulie sisi kuwa ni bora ya wao.

Nchi kama Singapore imo katika bara letu hili la Asia upande wa kusini mashariki, kuna jamii nne: Wachina ambao ni 75%, Wamalay 15%, Wa Indo-Paki 7% wamagharibi 2%.

Pia kuna dini sita: Budha, Tawia na Konfush 54%, Waislamu 18%, Wakristo 13% mabaniani 44%. Na kuna vyama vingi vipatavyo 20 vilivyosajiliwa rasmi. Licha ya uingi huu nchii hii inaishi kwenye utulivu wa ndani, na wote wako kwenye harakati za kutengeneza uzoefu wao uliopita na kujenga uchumi unaokua.

Wazungu, Ulaya waliishi miaka na mikaka ya kupigana na mizozo ya kidini, lakini sasa wameshaipita yote hiyo na wameneeemeka na amani na kuhakikisha kuwa wana umoja wa Ulaya.Zaidi ya hayo pia kulikuwa na ugomvi mkubwa na wa muda mrefu kidini baina ya mayahudi na wakristo uliozitangulia tofauti zetu sisi kwa miaka mia tano, lakini sasa wameshayapita hayo na wanaishi kwa amani kwa kiwango cha kuishi pamoja.
Je vipi kwa umma wetu ambao nembo yake ni amani "Ingieni katika amani yote" ambayo inabeba ujumbe wa rehema ya viumbe wote: "

"Na hatukukutuma ila uwe ni rekma kwa viumbe vyote." Kuweza kuhakikisha amani na kuwa pamoja ndani kati ya madhehebu yanayohitilafiana? Ili tuodoe mgongano wa kitaifa, naona kuwe na mabo yafuatayo:

1. Kukubali kuwapo kwa pande mbili za kiislamuna watu wa Kibla moja kuacha kukufurishana na kukubali kuwepo haki ya kutofautiana kimaoni.

2. Kuheshimiana na kuchunga haki ya mwananchi yeyote awaye katika nchi yake, hata awe ana madhehebu gani.

3. Kuchukia kufanyiana ubaya upande mmoja kufanyia mwingine.

4. Kushujaisha mazungumzo katika kadhia zenye kuhitaliiana kiitikadi au kifiqhi au kihistoria ili kila upande mmoja ufahamu mwingine uhakika wake na wagundue njia za kukutana.

5. Kushirikiana na kusaidiana katika kuhudumia mambo yanayohusu Uislamu na umma kwa ujumla.

Na hapa napenda taasisi ziwe za jumla za kiislamu haifai ziwe kwa majina maalum yenye kuhusika na madhehebu maalum tu.

**Mwandishi:** Samahani, sipendi kuongezea swali hili nisitoke nje ya swali lenyewe, lakini ee Sheikh Hasan, hizi taasisi ulizozitaja zina utaratibu na misingi yake kama zile zilizoko Qum, Teheran na Najaf pia kuna madrasa na taasisi zenye misingi yao, anayeikubali, wao watamkubali, vinginevyo haingii, naona suala hapa linahitaji zaidi maudhui kuliko hisia mnazozihisi..

**Sheikh:** Taasisi zenye majina ya kimataifa ya kujumla ya kiislamu hapana budi zihudumie waislamu wote zisibague taifa au dhehebu fulani sawa iwe ni Saudia au Iran, au nchi nyingine yoyote, maadam ni ya kuhughulikia mambo ya wote.

**Mwandishi:** Hebu nirudie tuliyoungumza awali sijui ni kupitikiwa na ulimi au la, mahasimu wenu wanasema kuwa kuzuru makaburi ni kumuabudu asiyekuwa Mwenyezi Mungu, ni bidaa, ni haram, Sheikh sioni kuwa hakuna mwanafunzi-wacha mwanachuoni- anayesema kuzuru makaburi ni bidaa au haram, pia pia mzuru kaburi (*Qubuuriyyu*) hii ni lakabu anayopewa yule aombaye makaburi. Ama kuzuru kaburi la Mtume (s.a.w.) Hilo ni jambo limewekwa na ni lenye kupendelewa, nafupisha kwako hili, nafupisha kwako hili, mimi nimekulia katika vitabu hivi vya kisalafi.

Nakusudia yanayofungamana na kuzuru makaburi kwa kusafiri kuyaendea, na kuzuru kwa wanawake, na ibada ya Mwenyezi Mungu mtukufu mbele ya makaburi ya manabii na watu wema, na kujenga mash-had na misikiti juu ya makaburi yao, na kutawasali nao kwa kumuomba Mwenyezi Mungu, na ufafanuzi unaohusiana na maudhui ambayo ni yenye hitilafu kati ya masalafi na waislamu wengine wa Sunni na Shia.

**Lakini tutaanza vipi?**

**Mwandishi:** Turudi kwenye asili ya swali, tusibaki kukanganywa, Swali hapa ni: Juu ya kuganda kwenye nafsi za makundi mawili hayo, sisemi kuwa tutaliondoa lakini vipi tutaweza kulisahilisha usongo wake?

**Sheikh:** Swali hili ni muhimu sana, inapasa wenye mwamko na walinganiaji wa umoja na ukaribu wajitahidi kujibu, naona kuna mambo matatu yatakayotusaidia katika kushinda usongo huu uliozama nyoyoni kati ya pande mbili kulingana na maneno yako:
La kwanza, kutochochea haya na kuzuia kuyakuza, na kuyachukia, kulikuwa na mwenendo wa kuchukia kupingwa rai na hasa upande wa ndugu zetu wa kisalafi, wana maneno makali dhidi ya wanaowapinga rai zao, wawe ni mashia au ni masufi au wengine katika waislamu wanaohitilafiana maoni.

Yapasa walinganiaji wa pande mbili kuwafanya watu wao wawe dhidi ya watu wengine, na kuwafanya waonekane kama upande hatari, kuna baadhi ya rai na fatwa ambazo zimesema kuwa Rafidha-yaani Shia- ni hatari hata kushinda mayahudi na wakristo hali hii inazuia kuondoa kasumba hiyo bali inaizidisha.
Isitoshe, yatupasa tuwache kujishughulisha na tofauti za kiitikadi na kimadhehebu kuna mambo wanayoshirikiana watu katika kila dini na kila umma ambayo yanastahiki zaidi kuyapa umuhimu na kuyashughulikia.
Sunni wamesema yote waliyo nayo, na Shia wamesema yote waliyo nayo, wala hakuna mmoja anayeongeza kitu kipya ila ya kimedhehebu tu, mpaka lini iwe hivi?

Pili, ni kueneza mafunzo ya kusameheana, kukubali kuwapo madhehebu mengi na kuheshimu rai ya mwingine na kutumia lugha ya kujadiliana.

Tatu, Kuweka uwezo wa kuishi pamoja kwenye uadilifu na usawa na kuchunga haki za mwananchi na za binaadamu, kushujaisha kuponya na uwazi wa kiislamu na kinchi.

**Mwandishi:** Hapa kuna maneno lazima niyaseme, mwanzo ni yaliyotolewa katika vitabu, majarida na makala kutoka kwa mashia ya kuwatukana na kushutumu maswahaba na walinganiaji wa kisalafi ndio wanaotuhumu sana licha ya kuwa zimejaa makosa pengine kuchukulia kwao wao hivyo na maneno yao makali ni utaratibu usio wa kisomi.

Sikanushi kwamba katika mashia hakuna mushadidina waliowataja vibaya baadhi ya maswahaba na makhalifa, katika vitabu na majarida na magazeti, kama ambavyo wewe huwezi kukanusha kuwa kuna vitabu, fatwa na hotuba kutoka upande wa masunni zinazowakufurisha mashia na kuwatuhumu kwa tuhuma na sifa mbaya.

Sisi hivi inabidi tuipite hali hii mbaya isiyoambatana na umma unaobeba ujumbe wa kiislamu, na unaoishi katika enzi za upinzani kwa makundi mbalimbali. Badala ya kuzama katika kuhesabu mafaili dhidi ya yetu yenye matukano mengi, na tuelekee kwenye mshikamano wa utukufu wa kiislamu, tuache mgongano wa kimadhehebu, kutilia mkazo umoja wa umma chini ya uongozi wa Kitabu cha Qur'an na Sunna, kuheshimiana na huduma kwa masilahi ya umma.

Ama ulivyosema juu ya kupinga ulamaa wenu kadhia ya kutabaruku, ni haki ya kila mwanachuoni au upande wowote kutoa rai yake, lakini iwe kwa lugha ya kielimu, na kulazimika na adabu za kuzungumza za kiislamu na kutowashuku katika dini wanaopinga rai zao, au kuwatuhumu na shirki na upotevu, hii lugha inabidi tuiache na kubadilisha kwa lugha ya mazungumzo mazuri na kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa hekima na mawaidha mazuri.

Ama ulivyosema juu ya kupinga ulamaa wenu kadhia ya kutabaruku, ni haki ya kila mwanachuoni au upande wowote kutoa rai yake, lakini kwa lugha ya kielimu, na adabu za kuzungumza za kiislamu na kutowashuku katika dini wanaopinga rai zao, au kuwatuhumu na shirki, hii lugha inabidi tuiache, tuibadilishe kwa lugha ya mazungumzo mazuri na kulingania kwa Mwenyezi Mungu kwa hekima na mawaidha mazuri.

**Mwandishi:** Hebu niwe mkweli na muwazi katika tukijadiliana haya yaliyoko kati ya makundi yetu mawili, kwa rai yako, Sheikh, ni nani atakayeangika kengele? Yaani litakuwa ni jukumu la nani la atakayeanza majadiliano haya ya kufahamiana, je ni kwa upande wa kisiasa au kwa upande wa ulama wa dini na walinganiaji?

Ilikuwa yapasa jukumu la mwanzo liwe kwa ulama wa dini na walinganiaji, lakini kwa hali ya hivi sasa yanifanya niamini kwamba mwanasiasa ndiye mwenye jukumu la kwanza.

**Mwandishi:** Vyema. Umetuwekea wanasiasa hapa lakini je unazo sababu zako?

Uongozi wa kisiasa kila nchi una jukumu la kuangalia hali za wananchi wake pamoja na tofauti zao za madhehebu na kabila zao, ukifanya usawa na uadilifu na kutoa fursa, wote watajikuta wako mbele ya fikra ya kuishi pamoja na kuheshimiana haki zao.

**Mwandishi:** Si vibaya ulivyosema Sheikh, lakini wewe umeangalia hali ya mshia wa Saudia tu, bali mimi swali langu ni lenye upeo wa hali ya Uislamu kwa ujumla.

Pia katika jibu langu nimekusudia hali ya Uislamu katika miji yote ya kiislamu, lakni nimeona kuwa miji mingi ya kiislamu haina matatizo mengi ya kundi fulani (jamii fulani).

**Mwandishi:**(Akadakia), Samahani...samahani.... tunayosema juu ya ndugu zetu wa kisunni wa Iran, kuna baadhi ya ripoti zinasema kuwa wanakandamizwa zaidi ya mnavyolalamika nyinyi.

Hebu nipe nafasi, juu ya ulivyosema juu ya masunni wa Iran. Hapa ningependa kutaja vidokezo vifuatavyo:

Kwanza, haifai tufanye suala hili kwenye msingi wa kusawazisha, masunni wa Iran ni wananchi na ni lazima wapate haki zao wachilia mbali hali ya mashia wa nchi zingine, na mashia wa Saudia ni lazima wapate haki zao, wachilia mbali hali ya masunni wa nchi zingine.

Pili, Kabla ya kuangalia serikali nyingine katika ulimwengu wa kiislamu, sisi ni nchi yenye mambo yake maalum, nchi yetu ndiko kulikoshuka wahyi na ina serikali inayoshikamana kufuata Qur'an na Sunna, ni muhimu kwetu tuitangulize hali yetu kama mfano wa wengine, kama wengine wakizembea katika kutimiza wajibu wao, hiyo isiwe sababu kwetu ya kuzembea, na hilo hatulikubali sisi wenyewe.

Tatu, Mimi sijipi haki ya kuzungumzia juu ya mashia au masunni wa Iran, inawezekana ukazungumza nao moja kwa moja, na napendekeza kwa jarida lenu muweke mjadala juu ya mambo mbalimbali ya Iran katika maudhui ya kiserikali, kijamii, kisunni na kishia,na hasa mambo ya masunni, naona hili lina umuhimu kwenu na kuwa lafaa hasa.

Wallahi Sheikh, ni mwito wenye kukubaliwa, na sidhani kama wasimamizi wa gazeti watazuia kazi ya umoja wa umma wetu nawe uturahisishie jambo wahusika wakikubali. Lakini, samahani, bado sijatosheka na hali ya masunni huko Iran, nawe umekaa huko kwa kipindi si haba. Nataka maelezo yako juu ya nano aliyemuua Imam wa masunni Ahmad Mufti Zaadah, nani aliyemuua Nasir Farqani, na ni nani aliyeharamisha masunni hata haki ya kuwa na mwakilishi ambapo wako waakilishi wa mabahai, waabudu masanamu wa Majusi, natamani ujibu kwa uwazi kwani utayoyataja hapa yatasajiliwa na historia.

**Sheikh:** Ndugu yangu mwema, wewe unaona jinsi serikali ya marekani ilipoanza kuishinikiza Saudia ilisisitiza kuwe na uhuru wa kuabudu, na haki za majimbo ya kimadhehebu, kama ilivyotajwa katika ripoti ya wizara ya nje ya Marekani hivi karibuni.

Na sote twajua kuwa imetangaza vita na Jamhuri ya kiislamu ya Iran tangu iliposimama, serikali hiyo ndiyo iliyohimiza utawala wa Saddam kupigana vita na Iran na kuiwekea vikwazo vya kiuchumi, na leo hii Marekani inafaya kampeni kali juu ya nuklia ya Iran, katika kivuli hiki ni kutaka kuleta vita vya ndani nchini humo, ndiyo wakazusha.

Hatusemi kuwa Iran haina makosa, yawezekana kuna makosa katika vyombo vyake, na yakagunduliwa, inawezekana kuna miongozo ya kikabila katika baadhi ya vyombo vyake pia, au kwa viongozi wanaohusika kama vile pia baadhi ya masunni wa huko wnavyojiingiza katika misimamo ya kimakosa, haya yote yapo.

Binafsi sijui ukweli wa mauaji uliyoyataja ya baadhi ya watu wakubwa wa kisunni huko Iran.
Lakini nina habari kwa ujumla za hali ya masunni wa huko, katika muda niliokuwa huko, na na habari za watu wakubwa wa kisunni waishio Teheran, lakini sikuzuru mikoani kwao.

Katika katiba ya Iran ya kiislamu nimesoma kifungu kinachoeleza kuyatambua madhehebu ya kisunni nayo ni mada ya 12 ina ibara ifuatayo: Madhehebu za kiislamu zingine, Hanafi, Shafii, Maliki, Hambali na Zaydi hizi zinapatiwa heshima kamili na wafuasi wa madhehebu haya wako huru kufanya mambo yao ya kiibada ya kimadhehebu kulingana na Fiqh zao, nazo zina mazingatio rasmi katika masuala ya kielimu, mafunzo ya kidini na hali za kimaisha (k.v. Ndoa, talaka, urithi na wasiya), na yanayohusiana na kesi mahakamani.
Na kila jimbo (mkoa) ambao wafuasi wa madhehebu fulani hapo ni wengi, basi hukmu za mahali hapo zitakuwa kulingana na itakavyoafiki madhehebu hiyo yenye watu wengi hapo, hii ikiwa ni pamoja na kichunga haki za wafuasi wa mmadhehebu mengine wanaoishi hapo."

Pia nilijuwa kuwa mitaala ya masomo ya kidini katika shule za serikali katika maeneo ya masunni ya hapo Iran, pia inafuata madhehebu ya hapo.
Na nilisoma aliyoandika Ustadh Fahmi Huweidi, mwandishi wa magazeti maarufu juu ya hali ya masunni wa Iran, katika kitabu chake, '*Iran ruuyatun min dakhil*' (Iran kwa mtazamo wa ndani) na alikuwa na nadharia nzuri.Pia najua kuna washauri wawili wa kisunni wa Rais wa Iran, wanaomshauri juu ya mambo yaona najua pia kuna mshauri wa waziri wa mambo ya ndani wa Iran

anayeshughulikia mambo ya masunni.Ama kauli yako kuwa masunni wa Iran wananyimwa haki ya kuwakilishwa hii si sahihi abadan, kwa sababu wanashiriki katika chaguzi, nao katika bunge la sasa wana viti ishirini na kimoja. Na hizi ni habari zinazotangazwa pia unaweza kuzipata.

Pia vitabu vya kisunni hasa marejeo, vinachapishwa Iran, na vinaingia. Mimi mwenyewe nimenunua vingi kutoka kwenye maduka yao ya Qum na Teheran nilipokuwa huko. Isitoshe kuna maonyesho ya kimataifa ya vitabu Iran ambayo Saudia inashiriki.
Masunni nchini humo wana mashule na Hawza zao za kidini na wana jarida lao rasmi mkoani Zahidan lenye anuani '*Nidaaul islam*' (mwito wa kiislamu) kwa lugha ya kifursi, humo kuna maoni yao na habari zao.

Umenifanya nizungumzie haya na sikupenda kuyazungumzia ila tu kwa kiasi cha kadhia ya umoja na siko katika propaganda za Iran wala kuwatetea makosa yao. Ikiwa masunii wana matatizo Iran au matakwa, ni haki yao kufanya bidii bila ya kutafuta kuingiliwa na wageni kama sisi tunavokataa kuingiliwa mambo yetu.

## Mifano ya Iraq na Lebanon

**Mwandishi:** Wallahi sitokujadili ila nina uhakika kuwa wanaotafiti mambo haya watatoa rai zao kusahihisha au kukubaliana, hebu niende kwenye mfano mzuri, mfano wa kuishi pamoja na kuelewana, huu ni wa Lebanon na Iraq, je, kwa maoni yako mifano hii miwili inaonyesha kwa umma yale unayoyataka ya kuelewana baina ya Sunni na Shia na kuacha hitilafu zao za kihistoriana wasaidiane katika hali yao ya sasa na ya baadaye, je una maelezo?

**Sheikh:** Huenda mfano wa Lebanon wa kuishi pamoja, kuelewana na kushirikiana na kuheshimu uhuru wa wote huchukuliwa kuwa ndio mfano bora kabisa katika Uarabuni, licha ya kuwa na matatizo yao.

Iraq hali ya kimadhehebu pia haikuwa mbaya, madhehebu ya Hanafi ndio makubwa kwa masunni wa Iraq, . na hawakufanya mapinduzi mabaya dhidi ya wengine, ama mashia nchini humo, wanavyuoni wake wakipigania umoja wakiwamo Sheikh Muhammad Husein Al-Kashiful Ghitaa, Sheikh Abdul Karim Zanjani na Sheikh Muhammad Al-Khalis.

Mapinduzi ya Iraq ya ishirini, 1920 (A.D.) ya kuufukuza ukoloni wa kiingereza yalishuhudia umoja wa kiislamu Iraq.
Wakati wa utawala wa Baath pamoja na dhulma na ukandamizaji waliowafanyia mashia, walio wengi, na Saddam kujipa madaraka mengi kwake na kwa ukoo wake, ila upinzani wa mashia dhidi ya Saddam ulikuchua mwelekeo wa kitaifa, kwa wao kuzingatia kuwa Sadam alitawala kiimla, na si mpinzani wa madhehebu, kwa jinsi ilivyoonekana kuwa hata ulamaa wenye mwamko wa kisunni pia aliwakandamiza.

Anayezisoma hotuba za harakati za kishia za Iraq kama za Hizbu Daawa, Majlisul A'ala na Muanadhamatul a'malul islami, na majlisul a'ala lithawra na wengineo ataona msimamo huu kwao wazi wazi. Na baada ya kuanguka Saddam majaribio yote ya kuyavuta makundi mawili kwenye vita hayajafaulu. Na twataraji watu wa Iraq washikane na mwamko huu wa kiislamu, waungane kupinga kukaliwa, na vile iilivyo sasa msimamo wa ushirikiano baina ya sunni na shia mpaka Iraq ishinde kukaliwa.

na kurudi uhuru na wajenge utawala wa demokrasi ya pamoja, kuheshimi haki za watu wa makabila yao.

Ningeomba iendelee roho ya mashia wa Iraq, licha ya kuwa wao ni wengi, na wafanye kazi pamoja na ndugu zao wa kisunni na makabila na madhehebu mengine.

**Mwandishi:** Ee Sheikh Hasan, samahani, katika uliyoyasema kuna makosa. Mashia wa Iraq wengi wao, ukimtoa Muqtadha Sadr, wako pamoja na mlowezi wa kimarekani, bali imefikia hata kushirikiana naye, nasema hivyo kwa neno la kuchukiza..mpaka...

Ningelipenda kusema jambo moja tu, kuwa watu wa Iraq ni jirani zetu wawe masunni au mashia, ni sehemu ya umma wetu, naogopa isiwe kuumizwa nchini kwao na misimamo yao ikaleta madhara kuhusiana na sisi kwa mustakbali na wao. Watu wa Iraq wote wana ghera na nchi yao, wala hakuna mmoja wao anayekubali kukaliwa, japokuwa walifurahi kuanguka kwa Saddam, lakini hakukuwa na mmoja wao aliyepinga wimbi la Marekani la kukuandaa Saddam kwa ujinga wake.

Ama kupinga kukaliwa na Marekani katika mkondo huu kwa kutumia jeshi hilo ni jambo lenye ushindani kwa watu wa Iraq, na mimi nionavyo ni kwamba, nguvu nyingi za kidini na za kisiasa hazichagui mapambano ya kijeshi.Na kuna kikundi cha Sunni na Shia kilichoamua kupambana kijeshi.

Natumai ndugu yangu mismamo ya kisiasa usiifanye ya kimadhehebu, hata masunni wengi wa Iraq hawakupambana na ulowezi wa Marekani.

Makurdi hali zao ziliwalazimisha kukubaliana na ulowezi wa Marekani, je wao ni mashia? Waafghanistani ambao wengi walikubaliana na ulowezi wa Marekani nchini kwao, je wao shetani dhidi ya nduguyo."Kinachopitia umma, wala tusiwe wasaidizi wa shetani dhidi ya ndugu zetu, Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Usiwe msaidizi wa shetani dhidi ya nduguyo."

**Mwandishi:** Hebu niingile katika nukta ya pili, ee Sheikh Hasan, umedai uingi wa mashia Iraq, lakini uingi huu unatofautiana na hivyo tukikusanya idadi ya masunni na makurdi.

Hainikeri kuwa masunni ndio wengi Iraq au si muhimu kwangu mashia kuthibitishwa kuwa ndio wengi, masjala za uchaguzi na masanduku ya kura ndio yatakayohibitisha, mimi najikita katika maneno yako ee Ustadh Abdul Aziz juu ya mgongano katika kuhusu kushirikiana na Marekani. Inadhihiri watu wa Iraq wamethibitisha kuiva na kuchunga nchi yao kwa namna isiyodhaniwa, kwani utawala uliopita ulikuwa umechimba mashimo ya fitna na matatizo tulikuwa tuna wasiwasi wa kulipuka moto wake baada ya kuangushwa utawala huo, lakini jinsi watu wa Iraq walivyoonyesha mshikamano mkubwa wa umoja, ni jambo lenye kutoa bishara ya kheri inshaallah.

Ilikuwa inawezekana mashia waliepuke baada ya mlipuko wa tarehe 10 mwezi wa Mfungo nne (Muharram) katika miji ya Karbala na Kadhimiyya, au baada ya mlipuko uliomuua kiongozi Seyyid Muhammad BAqir Al-Hakim huko Najaf, lakini muongoozo wa kidini wa Najaf na wa baadhi ya viongozi wa pande mbili, umewashinda maadui.

Wakati baadhi ya mashia walipokimbilia kuchukua misikiti ya masunni iliyojengwa na utawala uliopita katika maeneo ya kishia, Marjaa Seyyid Sistani aliharakisha kutoa fatwa ya kuirudisha misikiti hiyo kwa masunni, na maimamu wake kurejeshwa wakiwa wanaheshimiwa, na hata alitoa gharama za kuikarabati na kuitengeneza kama vilivyotangaza baadhi ya vyombo vya habari .
Hakika hali ya kuiva kama hii ya watu wa Iraq inastahiki tusaidie kuiunga mkono na tusiiichochee na kuitia matatizo kama tunavyoishi kwetu.

Wallahi Sheikh masomo yako ya mantiki Najaf si ya bure yanaonekana katika majibu yako hapa, hebu nithibitishe hapa kazi waifanyao ndugu zetu masunni huko Iraq, tumeona katika televisheni misaada ya watu wa Faluja masunni inaenda Najaf.

**Sheikh:** Na kabla ya hapo pia misaada ya mashia kwa watu wa Faluja ilianza kitambo.

Sheikh, suala hapa si kuzidiana bali ni mlingano wa udugu ili kuzidi mapenzi.

**Sheikh:**Kuzidiana hakutakiwi, usawa ndio unaotakiwa.

**Mwandishi:** Nenda kwenye mifano mingine: Bahrain na Kuwait, inaonekana kwamba ilivyo kwa Kuwait kwa pande mbili si hali nzuri kama ilivyo Bahrain ambapo kuna ushirikiano. Kwa nini Kuwait iwe hivi, sababu ni nini? Na kwa nini Bahrain wawe na mshikamano?

**Sheikh:** Kadri nijuavyo, hakuna tatizo la mshikamano katika ya Sunni na Shia nchini Kuwait, hakuna kushikana mashati kati yao, kwa mnasaba huu hebu niseme kuwa maneno ya kusema kuwa katika dunia hii kuna maneno ya Sunni kuwa dhidi ya Shia au khatibu huyu wa Shia kuwa dhidi ya Sunni, haya hayawahusu tu sana madam maisha yao hayathiriki na maneno kama haya. Lakini tatizo ni kuyageuza maneno haya kuingilia kwenye haki za watu.

**Mhemko wa kijamii Kuwait**

Samahani sheikh, kutokuwapo mvutano, sijui Sheikh, lakini nahisi kuna mhemko wa kijamii huko, je nikukumbushe kanda ya Yasir Habib na alivyoeleza wazi juu ya kuwatukana maswahaba wa Mtume (r.a.)?

**Sheikh:** Nishaisikia kanda hii, hii ni kazi ya mtu mmoja tu pekee, ambapo kundi la wanavyuoni wa kishia walitoa taarifa ya kujitenga na kanda hiyo na kuikemea, huyu si mwanachuoni wala hana wadhifa wowote wa kidini au wa kijamii. Na wote walikubaliana kupelekwa kwenye hukumu, ndivyo ilivyotokea .Na kama ilivyotokea kwa baadhi ya mashia kufanya makosa haya, hata kwa baadhi ya masunni pia ambapo Kuwait, ukumbi wa mashia uliteketezwa miaka miwili iliyopita. Na kukatolewa vijitabu na kanda dhidi ya Shia lakini serikali ya Kuwait na masunni na mashia wa Kuwait wanatambua hatari ya mizozo hii, hivyo wanaidhibiti ikiwa bado ni michanga kwa njia moja au nyingine.

**Mwandishi:** Kama hali iko hivyo, alhamdu lillahi, na mimi wallahi nafurahi kwa kusikia hivyo. Hebu uende Bahrain, na tuone unavyoona hali ya jamii mbili huko.

**Sheikh:** Bahrain pia hali ni nzuri, hakuna matatizo kati ya uhusiano wa Sunni na Shia, bali hata wanaoana, wanashirikiana kibiashara na kikazi. Wiki chache zilizopita niliona katika televisheni, idhaa ya *Al-Arabiyyah* kipindi kiitwacho '*Idhaa at*' mjadala na Sheikh Adil Al-Mua'wadah,mwanachuoni mashuhuri wa Bahrain ambaye aliusifu uhusiano hhuo Bahrain.

Nanyi mwajua kuwa katika Baraza kuu la mambo ya kiislamu la Bahrain lina mashia nusu na masunni nusu, chini ya uongozi wa waziri wa mambo ya kiislamu, naibu wa waziri mkuu, Sheikh Abdallah bin Khalid Al-Khalifa.

Je Sheikh, si tuko pamoja kwamba mifano hii ya kusaidiana baina ya pande mbili imekuwa ni maslahi ya kushirikiana ya nchi waliomo, yote yamewafanya waungane wawe na umoja, tukiangalia kwetu sisi, je si vizuri kuungana pande mbili na kushirikiana?

**Sheikh:** Naam, ilitakiwa iwe hali ya kwetu sisi ni ya karibu zaidi ya kuungana kwa kuwa nchi yetu ina hali ya kidini inayotambulika, haki ya kushirikiana kati ya madhehebu nchini Saudia itakuwa na athari kubwa kwa ulimwengu wote wa kiislamu, ambapo hali ya kutokuwa pamoja ya kimadhehbu ina athari mbaya kwa umma wote kama ilivyo hali hiyo sasa.Lakini kuna mambo mawili tofauti kati ya nchi hizo tulizozitaja na Saudia:La kwanza, Serikali ya Saudia imeshikamana na utaratibu maalum wa kiislamu wa kisalafi.

Pili: madhehebu ya kisalafi yana msimamo mkali dhidi ya maoni ya wengine na mfano ni iliyotoka kwenye *Ar-Risala* tarehe 11 mfungo sita mwaka 125 (A.H.)

ya ulama wakubwa akimjibu Dkt.Abdul Azizi Tuwayjiri, makala inayoitoa Shia kwenye Uislamu, na inakataa kuwaona kuwa ni ndugu katika dini, nainukuu: "Ama kauli yako kuwa mashia ni ndugu zetu katika dini na katika nchi, tunasema kuwa wao ni ndugu kwa anayewaridhia kuwa ndugu, ama anayewajua uhakika wa itikadi yao iliyomo katika vitabu vyao, Marjaa wao na wayasemayo katika dua zao na mihadhara yao, huyu hawezi kuwazingatia kuwa wao ni ndugu zake, kuwa mwananchi si udugu wa kidini."

Maneno haya mafhumu yake ni kuwakufurisha mashia kama ilivyo wazi.

**Mwandishi:** Hapo nitakuingilia haraka Sheikh, kwa nini kutokana na mazungumzo yako kama ulivyosema juu ya kanda ya Yasir Habib, hukuzingatia kuwa hii ni rai ya mtu binafsi tu? Hapa najiuliza umlaumu Sheikh Ali Swaleh pekee?

Mungu anisamehe mimi na wewe ee ustadh Abdul Aziz, Yasir habib ni kijana mwenye jazba tu hana cheo wala kufuatwa na yeyote, na maoni yake hayazingatiwi na yeyote, ambapo Sheikh huyu ni sehemu ya uongozi rasmi, na maoni yake yana athari kubwa kwa wafuasi wengi wanaomuamini.

**Mwandishi:** Kwa nini unapinga rai yake tu juu ya wimbi kubwa kwenye nchi nzima, nawe unaweka mipaka ya mjadala wa nchi aliouchunga kiongozi wa Saudia na jumla ya walinganiaji na wanavyuoni.

Natamani yatolewe katika wimbi hilo pana yanayopinga maneno haya hapa nitasema dondoo zifuatazo:

Kwanza, sisi tuko katika nchi ambayo haimpi uraia ila Muislamu, vipi tunyamaze juu ya mtu anayemkufurisha mwananchi wa hapa na kumchukulia uraia wake?

Pili, maneno haya yamekuja katika wakati ambapo sauti zimepaazwa juu ya kupinga kumkufurisha mtu ambapo kumetoka taarifa kutoka kwa kitengo cha ulamaa wakubwa na watawala pia wakliaeleza wazi wazi hilo. Kwa nini lilinyamaziwa jambo hili linalokwenda kinyume na siasa ya nchi na misimamo iliyotangazwa na taasisi ya dini dhidi ya kukufurisha?

Tatu, nchi sasa hii inakabiliana na hatari ya makundi ya kigaidi je haihofiwi makundi haya yachukue fursa kwa ajili ya maoni kama haya katika kutekeleza ugaidi wao?

Hii hapa fatwa ya mwanachuoni mwingine katika ulama wakubwa, imetolewa na kitabu kilichotolewa na kitengo cha *Ighaathatul Islamiyya*, kutoka kwenye ofisi yake mjini Ahsaa ambapo mashia ni nusu ya wakaazi mjini humo. Chini ya kichwa: '*100 sual wa jawaab fil a'mali khayr*', mwaka 1423 (A.H.) Ukurasa 11-12:"Ni wajibu kwa waislamu wa Ahli sunna kuwachukia watu wa 'bidaa' na kuwadharau kama vile maraafidha, na Muu'twila, Quburiyyuna na Ibadhiyyuna, kama vile inavyopasa juu ya muislamu, kwa wingi wao (wakiwa wengi) na kumakinika kwao nchini kujiepusha nao ili kuokoka na shari zao, ikiwa hakuweza kuhama yafaa kuzoeana nao na kuondoa shari yao japo kwa sehemu ya Zaka na mzingatie kuwa ni katika wanaozoeshwa nyoyo zao (*muallaftu quluubuhum*).

Haifai kuwasaidia kwa vile ni kuwatia nguvu mambo yao na kudhihirisha bidaa zao, kwani kumakinika kwao kutakuwa ni kuwadhalilisha na kuwatweza Ahlu sunna.

Ni juu ya kila muislamu wa Ahli Sunna afanye bidii katika kila yenye kumtweza mzushi wa bidaa, wasiwafanye wafanya kazi wala watumishi, pia wao wasiwatumikie wala wasifanye kazi nao katika yatakayowapa nguvu na kukuza tija zao, wala asinunue bidhaa zao, lakini asipoweza kuepukana na shari zao inafaa kuwalipa kwa kiasi cha kujiepusha na maudhi yao.

Maoni kama haya na misimamo kama hii inayotoka kwa ulama ambao wao wana nafasi kwao, na taasisi zina matukio yake pia, ni kawaida yatakuwa ni kizuizi cha kufikia mkuruba na mshikamano katika jamii ya kisaudi na katika mustawa wa umma.
Mungu anashuhudia, sitaji hivi kwa ajili ya kumtangaza mtu, haya ni maoni yaliyoenezwa na kutangazwa, lakini nataraji kuwe na rekodi kutoka upande wao.

**Kutokea mema na kuona ukorofi**

Ewe Sheikh, nakusikiliza ukizungumza kwa nguvu na ukali, hebu nikushtukize kwa swali, je waona kuna mazuri yajayo, licha ya yote hayo?

**Sheikh:** Nahisi kuna mazuri mengi makubwa licha ya kuwapo yote hayo.

Vizuri, mwenye kusoma yaliyotajwa hapo awali au kupata bahati ili aweze kusikiliza kama mimi mazungumzo ya ukweli ataamua sivyo ulivyojibu, je una sababu ya kuyaona mazuri baadaye?

**Sheikh:** Sababu za kuona mazuri baadaye ni katika kuelekea uongozi wa kisiasa Ili kuweka mpango wa mazungumzo na uwazi baina ya jamii za Saudia

Kupitia mkutano wa kitaifa ulioitishwa na kusimamiwa na mrithi wa mfalme, na kupata fursa ya pande mbali mbali kutoa maoni yao baada ya kuwa nafasi hiyo ilikuwa ya upande mmoja, hii yamaanisha kujuana na kuamsha maoni ya kiujumla ya nchi kwa maslahi ya unyoofu, umoja na kukurubiana.

Na naamini kwamba kuinua kiwango cha mwamko wa pamoja kwa watu, na kukua mawasiliano kumetoa njia nyingine ya mafunzo na maoni ya pande mbili hii inaondoa yale waliyokuwa wakiyasikia kutoka kwenye upande wao wa kidini.

Pia ninaomba kizazi kilichoamka cha ulamaa na wanatablighi wawe katika mwamko wa kiislamu kwani kugundua kwao vipingamizi hatari na kufunguka kuona maoni ya wengine watakuwa ni wepesi kuelekea kwa wengine, na ihvyo kuachana na misimamo iliyoganda. Nimewahi kukutana na idadi ya mabwana katika wao nikawaona wana maridhiano na maandalizi mazuri.

**Mwandishi:** Nikiwa nahitajia kukukata maneno yako...ningependa utaje baadhi ya majina ya hao ulama wenye mwamko na kwa maelezo yako, ukawaomba.

Mbali na kuwaomba, nasema kuwa nimekutana na idadi ya ulamaa na walinganiaji nikasikia kutoka kwao mazuri akiwamo Mufti aliyefariki Sheikh Abdul Aziz bin Baaz, kiongozi wa baraza la hukmu la juu Sheikh Swaleh Al-Lahidan, waziri wa zamani wa wakfu na mambo ya kiislamu Dkt. Abdallah Turki, waziri wa sasa Sheikh Swaleh Al-Sheikh, waziri wa uadilifu Dkt. Abdallah Al-Sheikh, Sheikh Salman Al-U'udah,Dkt. Sheikh Awadh Al-Qarni,

Sheikh Ibrahim Abu A'abaa, Dkt. Hamdi Sulayfih, Sheikh Muhammad Dahim, Dkt. Hamza bin Husein Alfa'ar Sharif, na wengineo, na baadhi ya kukutana huku kulikuwa ni kwa kwenye mikutano ya kitaifa.

Nilikutana kwa vizuri na Dkt. Maanii' Al-Jahni katibu mkuu wa zamani wa *Nadwal a'alamiyya lishabbaabil islami* nilikutana naye kwenye makao makuu yao Riyadh. Pia nilitembelea mara kwa mara nyumbani kwa Sheikh Muhammad bin Zaid yumo kwenye kitengo cha ulamaa wakubwa, na ni raisi wa Mahakama ya kisheria wa Mkoa wa mashariki na kwenye ofisi ya mahakama Dammam, pia nilikuwa nikikutana kwa vizuri na Sheikh Muhammad bin Nasir Al-Abudi, katibu mkuu wa *Rabitatul aalami l-islami* wakati wa mkutano wa mkuruba baina ya madhehbu uliofanyika Bahrain, pia nakutana na mahakimu wa mahakama kuu ya Qatif.

**Mwandishi:** Mimi nakufuata kwa makini unavyotaja majina naona umeghafilika kutaja majina mawili, nao ni Safrul Safrulhawali na Nasir Al-Umar.

Mpaka sasa sijapata fursa ya kuonana nao na natamani hivyo, hakuna matatizo au kizuizi cha kunizuia kuonana nao, kutofautiana kimaoni au kuwa na misimamo tofauti hakuzuwii kukutana, lakini ningekuomba uniruhusu nikamilishe maelezo yangu umenikatiza, Mungu atusamehe.

Tatu, kuinua kiwango cha kuwafunza watu hasa masunni na mashia wanajifunza  na kupata misimamo yao yote kwa kuigiza tu hapo mwanzo mshia alikuwa akipata mafunzo yake kutoka kwenye husainiyya (kumbi zao),

Kutoka kwa Sheikh na kwa khatibu wa kishia, na msunni pia akipata mafunzo yake kutoka kwenye khutba ya Ijumaa na kwa Sheikh wa kisunni, hivi sasa kumefunguka njia za kupata elimu na mafunzo, idhaa za runinga, Tovuti (*Internet*), na vitabu, watu waakanza kuona, huku wakigundua na huku wakichunguza.

Msunni aliyekuwa zamani kwamba mashia wanafanya kadhaa, sasa imekuwa vyombo vya habari vinawaletea moja kwa moja mambo ayafanyayo mshia. Hivyo akili yake haitodanganywa na Sheikh anayeemuona kwenye zawiya yake. Pia wanasikia maneno ya ulamaa wa Shia na wanaona misimamo yao.

**Mwandishi:** Hapa Sheikh nitasema tunavyoona kwa vijana wa kishia kwa usawa ambapo wanasoma na kufuatilia mambo ya ulama wa Sunni.

Ndio, kuna uwazi kwa Mshia juu ya ulamaa na wasoni wa kisunni, wengi walikuwa wakifuatilia mhadhara wa Sheikh Shaa'rawi katika Tafsri ya Qur'an, na wanasoma ya Sheikh Muhammad Al-Ghazali, na hivi sasa wanasoma na kusikiliza ya Sheikh Yusuf Al-Qardhawi na wengine kama hao wanaozungumza lugha ya mwamko wa kisasa.

## Kukutana muhimu kwa kihistoria

Tukirudi kwenye maudhui ya kukutana kwako na Sheikh Abdul Aziz bin Baaz kukafuatiwa na tuhuma nyingi kama kawaida ya vyombo vya habari ningelipenda uzumgumzie mkutano huu kwa bayana, kwani ulikuwa lini?

**Sheikh:** Ulikuwa Mfungo pili, mwaka 1416 (A.H.).

**Mwandishi:** Je ulikuwa ni kwa maombi yako au ya Sheikh?

**Sheikh:** Kwa maombi yangu.

Je unaweza kunieleza na wasomaji nini hasa madhumuni ya kufanya hivyo?

**Sheikh:** Mimi ninatosheka kabisa kwamba kukutana na mtu mkubwa kunaleta kujuana kuzuri zaidi, na ilitokea kwamba nimesoma juu yao lakini kukutana nao kumeniongeza kuwajua zaidi, kuanzia hapa nikapenda kuonana na mkubwa yeyote aliye na umuhimu, hivyo nikawa napenda kukutana na Sheikh Bin Baaz.

Kwa upande mwingine, naamini kwamba picha ya wananchi wa kishia haiko wazi kwenye asasi za kidini nchini kwetu na vitabu na ripoti zimeichafua picha hiyo, na hiyo ilisaidia kuwafunga mashia kutokana na sababu zilizowazunguka, nikaamua kuvunja hili, na kujiweka wazi kwa uongozi wa kidini wa kisalafi wa nchi yetu, ili kukutana huko kufungue picha hiyo na kuanza mkondo wa mazungumzo na kujuana.

**Mwandishi:** Je unaweza kuniambia maudhui mliyoyazungumzia na Sheikh Ibn baaz?

Nilikutana na Sheikh Ibn Baaz katika baraza yake kukiwa na masheikh na watu wengine ambao wanaweza kuwa ni wafanyi kazi wake wa nyumba hiyo, nilikuwa na wenzangu watatu,akatupokea vizuri sana na baada ya mazungumzo ya kujuana na hali ya nchi, Sheikh alitaja habari zinazomfikia kuhusu kuwapo bidaa na yanayopinga itikadi katika jimbo letu.

Tukamsikiliza maneno yake, alipomaliza, nikamuomba nizungumze, ili nimshukuru kwa kutupokea, na nikafuatiliza na aliyoyasema Sheikh kwamba sehemu ya unayoyapata si sahihi, huko kuna kutofautiana maoni na ijtihad baina ya medhehebu, na nikamwambia kuwa wanavyuoni wa kishia wametunga vitabu wakabainisha humo uhakika wa maoni na itikadi zao. Akaniuliza vitabu hivyo nikamtajia kati ya hivyo vitabu viwili:

1. Cha Sheikh Ali bin Abil Hasan Al-Khanizi aliyekuwa ni Marjaa na kadhi wa Qatif (1291-1363 A.H.). kiitwacho, *'Ad-daa'watul islamiyya ila wahdati ahli sunna wal imamiyyah'* na kina juzuu mbili zinazofikia kurasa 950.

2. Kitabu *'Ad-daa'wa fi kalimati tawhiidi'* cha Sheikh Muhammad Swaleh Al-Mubarak (1318-1394 A.H.), huyu alikuwa kadhi wa shia wa Qatif. Sh. Ibn Baaz akaonyesha hamu yake ya kutaka kuvijua vitabu hivyo.

3. Mazungumzo yaliendelea yakaisha kwa vizuri, akatualika kwake, chakula cha mchana, lakini tukamuomba msamaha wa kutokula kwa sababu ya muda wa ndege, akatuuliza kama tuna gari kutupeleka uwanja wa ndege, tukamwambia tutakodisha,

akaamrisha gari ya Darul iftaa kutupeleka uwanja wa ndege.

Baada ya miezi nilimtembelea tena nikiwa na ndugu kutoka Ahsaa na Qatif akiwamo wakili, mwanafasihi Seyyid Hasan Al-Awami, mazungumzo yakawa mafupi juu ya kutupokea tu, hakusema jambo jingine zaidi, akatuomba sana tule chakula cha mchana lakini tulikuwa na shughuli nyingine, nakumbuka Seyyid Hasan Al-A'wami alikuwa na jazba sana tulipofuta mwaliko wa Sheikh, na ananilaumu mpaka leo hii kwa nini fursa ilitupita ya kuwa wageni wa Sheikh Ibn Baaz. Alipofariki mimi na baadhi ya wanafunzi wa Qatif na Ahsaa tulikwenda nyumbani kwake Riyadh kuwahani (tazia) kwa watoto wake na familia yake.

**Mwandishi:** Uliyoyataja ni mambo yanayomfurahisha kila mpenda nchi, lakini mbona hamjakutanana Mufti mkuu wa nchi wa hivi sasa Sheikh Abdul Aziz Al Sheikh, naye , kama tujuavyo, ni mwenye moyo mkunjufu na maoni ya kusameheana ya nchi.

Kabla ya miaka matatu mmoja katika viongozi aliniuliza suali hili, nikamuonyehsa hamu yangu ya kukutana na Mufti Sheikh Abdul Azizi Al-Sheikh, akaniahidi kufanya utaratibu wa kukutana naye, na akamwambia mkuu wa ofisi yake afuatilie jambo hili, lakni hatujakutana bado mpaka sasa, sijui ni kwa sababu ya udhaifu wa ufuatiliaji au kwa hali zake Mufti.

### Kurudi Qatif

**Mwandishi:** Huenda Mwenyezi Mungu akaleta baada ya hayo jambo zuri na kurahisisha kukutana na Mufti. Niruhusu nirudi nyuma, Kuwait, ulikaa muda gani?

**Sheikh:** Katika Madrasa Ar-Rasul ya hapo nilikaa miaka matatu, na katika muda huo nilikuwa nikisafiri kwa ratiba za dini k.v. Ramadhani, siku za Ashura, nikienda Muscat, Oman au nikija nyumbani, baada ya hapo nikarudi kumakinika nyumbani Qatif, nilirudi mnamo mwaka 1397 (A.H.).

Vizuri, baada ya kurudi Qatif, bila shaka ulileta fikra nyingine sio ile uliyoondoka nayo, swali ni je, ni nishati gani ulizozifanya uliporudi?

**Sheikh:** Nilirudi Qatif nikiwa na hima kubwa ya malezi ya vijana na elimu kwa jamii.

Hali ya kidini ilikuwa ni ile ile ya kuiga tu, khutba za kidini zilikuwa zinayoishia juu ya hukmu za sharia na kueleza historia isipokuwa wachahce katika Wanavyuoni na makhatibu lakini pia wakichunga mfumo wa kuiga tu katika baadhi ya misimu ya kidini kulikuwa kukija ulamaa kutoka Iraq kama Seyyid Hasan Qabanji, Seyyid Husein Shami, Seyyid Murtadha Al-Qazwini na Sheikh Muhammad Ali Taskhiri na kupata watu wengi kwa jinsi walivyoona kuwa khutba zao zina maendeleo mapya.

Vijana walikuwa wakipotea, wengi wao wakiishi tu maisha ya kutojali, na kutokuwa na ilimu.

Hapa ndipo Mwenyezi Mungu aliniwafikia na baadhi ya ndugu wanafunzi kuweka ratiba ya kushughulikia vijana nazo ni:

1. Kuwashujaisha vijana kutoka kila mji kusoma ilimu ya dini na Alhamdu lillah, majimbo mengi sasa yanavuna matunda hayo kwa kuwapo ulamaa na makhaibu katika wale tuliowashujaisha.

2. Kueneza vitabu na kanda za kidini kadri tulivyoweza.

3. Kuweka darsa za Qur'an na kuzizingatia Aya zake, tulikuwa tukiweka vikundi katika kila sehemu kukutana mara moja kwa wiki katika nyumba ya kijana mmoja wa kila mkoa naye atawaalika rafiki zake na katika kila jalsa tunawafafanulia Aya na tunawataka wazizingatie.

4. Tukifanya mihadhara na hafla kwa minasaba ya kidini na kuwashujaisha vijana kuiendesha, kuandika na kutoa maudhui humo, hasa katika mwezi wa Ramadhani, siku za Ashura kwa lugha ya kuondoa mambo ya kuiga tu.

5. Kwa kweli nilikuwa mmoja wa wanafunzi waliokuwa wakifanya harakati kwa mustawa huu, na kulikuwa na wengine waliokuwa na kazi yenye kushukuriwa naaja miongoni mwao hapa ni masheikh kutoka Aal Seif, Sheikh Tawfiq na nduguze wawili, Sheikh Fawzi na Sheikh Muhammad Aal Seif, baba yao Al Haj Taqiy Seif aliwashujaisha katika kutafuta elimu ya dini na walikuwa ni watu waliofanya kazi katika mambo ya dini na ya jamii, na walikuwa na uhusiano na Marjaa wengi, ulamaa na makhatibu wa kishia katika nchi mbalimbali.

   Aliwapeleka kwenye Hawza ya ilimu ya Najaf tukufu, lakini hawakufurahishwa na hali ya kuiga tu ilyokuwako huko, wallpoijua ratiba ya masomo ya Madrasa Rasul ya Kuwait wakaona ni kheri kubadilisha, wakawa pamoja nami wakafanya kazi kubwa katika kuwafunza vijana na kueneza elimu.

6. Pia namkumbuka Sheikh Yusuf Salman Al-Mahdi, na Sheikh Makki Al-Khuwaldi kuoka mji wa Swafwa, pia Sheikh Musa Abu Khamsin na nduguye Sheikh Hasan abu Khamsin kutoka Ahsaa na wengineo waliokuwa na nafasi katika kuleta nishati kwenye jimbo letu, Mungu awalipe kheri wote.

**Mwandishi:** Hebu nisimame nawe hapa Sheikh, Umesema mwanzo wa majibu yako kuwa kuna baadhi ya vijana kwenu wameathirika na misukumo mingine isiyo kuwa ya kiislamu kwenye jimbo lenu, je, je unaweza kututajia?

Ni kupanuka kwa mawimbi ya kifikra na kisiasa yaliyoletwa kwenye majimbo mablimbali katika ulimwengu wa kiarabu, na kuingia katika jamii yetu ya Saudia k.v. Ukomunisti, Ubaath, Nasiriyya na Qawmiyyah.

**Mwamko wa Sunni na Shia**

**Mwandishi:** Je nishati hiii ya kulingania au roho ya mwamko tuliozungumzia hapo awali je umeleta athari katika mwamko wa kiislamu? Je umewavuta pamoja au ni kinyume na kusababisha mwelekeo wake kuwa dhidi yake?

Hatukuwa na mawasiliano na kuwa na mwamko ndani ya Saudia kutokana na vikwazo vilivyokuwapo lakini kusoma kwetu maandishi ya harakati za kisunni kulleta mafunzo na nishati ya kidini hivyo ni vikundi kama vile: Jamaatul islamiyya cha Pakistan, Daaru nadwa cha India, Ikhwanul Muslimiina na Hizbu Tahriir.

Isitoshe masomo yetu hayakuwa kwenye muelekeo wa kupinga, bali wa kuungana japo hali tunayosihi inatulazimisha hali fulani ya hisia za kimadhehebu na utaifa kuwa ni akisi ya shinikizo na kusongeka.
Lakini msingi ulikuwa ni katika kutengeneza shakhsiyya ya kiislamu na kuwalinda vijana kupotoka kutokana na vitendo na tabia, na kuishujaisha jamii iamke na iendelee katika mambo ya dini na mafunzo ya jamii.

**Mwandishi:** Unayoyasema kwa wakati huo ilikuwa ni mafunzo ya kiislamu kwa ujumla bila ya kuingiza ukabila wa kwenu au ni ya ukabila tu?

Mwanzo tulitilia umuhimu kwa vijana juu ya mafunzo na kuwaamsha kuelekea upande wa kidini, kwa sababu vijana wengi wakati huo, hawakuwa wakihudhuria Swala za jamaa misikitini, na fikra potofu zilianza kuwaingiza wengine, ikawa tumekita katika kuwaelekeza vijana kidini, hatukujikita katika utofauti wa kimadhehebu ila tu katika baadhi ya masuala.

Tungo zetu tulizokuwa tukizielekeza kwao zilikuwa ni kwa mwamko wa kiislamu kwa ujumla, na zaidi ilikuwa vitabu vya Marjaa Seyyid Muhammad Shirazi, vinavyojikita zaidi katika kuurudisha Uislamu uaminike kuwa ni mwendo na utaratibu na waislamu kurudisha maendeleo yao, na vilipinga hitilafu katika Uislamu, kati ya hivyo nakumbuka ni: *Ibadatul islam, Fii dhwillil islami, Kayfa antashirul islam, Fadhilatul islamiyya, Anfiquu likay tataqaddamuu* na vinginevyo.

Pia vitabu vya Seyyid Ustadh Seyyid Muhammad taqi Muadarrisi k.v. *Buhuuth fil Qur'anil karim, Al fikrul islam kuwaajahatu hadhariyya, Il-islamu thawratun iqtiswaadiyyah* n.k.

Na vitabu vya ndugu yake, Ustadh Seyyid Hadi Mudarrisi vilivyokuwa vikivutia sana vijana kwa lugha yake ya kisasa na staili mzuri vikiwamo: *Hawar saakhin maa' twarafil aakhar, Laa liraasilmaaliyya, laa lilmarkisiyya, naa'm lilislaam, kayfa kuna wa limaadhaa na alfu baaul islaam,* hivi na vingine kama vinavyoonekana majina yake ni kwa mwelekeo wa kiislamu kwa ujumla.

Pamoja na vitabu vya sera za maimamu kwa upande wa kimaendeleo.

**Mwandishi:** Vitabu hivi ulivyovitaja, je vilikuwa vikiingia kwenye jamii yeu kwa ugawanyaji wa kimipango?

Vitabu hivi vilikuwa vikizuiwa kuingia hapa nchini kwa kuonekana kuwa ni vya Shia na watuzi ni mashia, na tulikuwa tukivinunua ghali kutoka kwa wauzji wa soko nyeusi (magendo) waliokuwa wakiviingiza kwa njia mbali mbali, kitabu ambacho Bahrain tulikinunua kwa riyal 10, kikiingia Saudia tlikinunua kwa riyal 30 au zaidi. Pia tulikuwa tukieneza vitabu vya kisunni kama vile vitabu vya Nadwi, Seyyid Qutbi, Muhammad Al-Ghazali na vya Yusuf Qardhawi.

**Lakini msimamo wa watu wa kwenu ulikuwa vipi**

Ni vizuri Sheikh, kwako roho hii ya kujifungua, kwa hivyo mimi nagundua kuwa unayo kweli, lakini swali linalokuja haraka kichwani kwa mwandishi kama mimi ni juu ya ndugu zako mashia kukubali mfano wa nadharia hizi za kuwa karibu, kwa uwazi, Sheikh, nafikiria kuwa Marjaa wenu wako dhidi ya jambo hili hapana budi wakupinge.

**Sheikh:** Kwa picha ya kiujumla, Marjaa wa kishia na ulamaa wao wanatoa mwito wa umoja na mkuruba hali ya upinzani mkali dhidi ya Sunni uko kwa kiasi kidogo, ndio, kulikuwa na kukereka kwa baadhi ya mashia muhafidhina, ya kuwa isiwe kuwa karibu na masunni isiwe kuwa karibu na masunni juu ya misingi na mambo ya kimadhehebu, kwa sababu masunni ndio wenye uongozi wa nchi, huenda wakalazimisha wale mashia wanaotaka kuwa karibu nao kuacha baadhi ya mambo yao ya kimadhehebu

Hapa tuna tatizo, naamini liko kwa masunni pia, kuyakuza baadhi ya mas-ala madogo na kuyafanya kuwa ndio misingi na nguzo zake,

Hivyo basi kuyajadili au mtu mwingine atoe maoni yake dhidi yayo, ni kama kuiteremsha imani na kujitenga na nguzo. Na wakati mwingine mwelekeo wa kufuata tu wa Sunni au wa Shia hupinga mabadiliko na Maendeleo hata katika baadhi ya ada kwa madai kuwa kufanya huko kunateremsha mengine.

Kwa insafu mimi sikupinga upinzani kutoka kwa mshia wa Saudia juu ya msunni kwa kule kuwa wazi kwangu na masunni, bali ni kinyume, kuna kufurahiwa hilo kwa ujumla, pamoja na kuwa kuna shaka juu ya kuukubali upande mwingine.

Mara nyingi baadhi ya mashia hunijia na vitabu na fatwa za masunni dhidi ya Shia, wakanambia: 'Athari yako ya kufunguka na ukaribu na hao masunni ikoa wapi?' faida ya kulingania kwako ukaribu na umoja i wapi hali wao wanang'ang'ania kutukufurisha na kutushuku katika dini yetu na kutubagua?

Si kitambo sana nakumbuka, mmoja katika walinganiaji wa kisalafi maarufu ambao watu wanajua nilikutana naye, katika idhaa moja mashuhuri, ambapo alisema maneno makali juu ya Shia na kunilaumu, huyu ndio unasema ni mwenye kuwa wazi na mwenye mwamko, mtu kama huyu anafaa kuwa karibu naye?

**Mwandishi:** Sielezi kumtetea Sheikh uliyemtaja lakini najua yakini, nakuomba ruhusa nirudi kwenye asili ya swali na hutonikimbia ee Sheikh, je ungetufafanulia ile fatwa tuliyoisoma kwenye Tovuti (*Internet*), na iliyowekwa na Marjaa kuu yenu naye ni Seyyid Khui aliyesema: "Ama kuhusu Hassan Saffar, tumeshatangulia kujibu juu ya swali...na limerudiwa jibu kwa baadhi ya watu wa Qatif kwamba jambo lake ni lenye kutia shaka na si lenye kuaminika na mliyoyataja yanasisitiza kukosekana kumuamini." Je unaweza kutufafanulia ukweli wa fatwa hii kali kwako?

Fatwa hii inafungamana tofauti na mvutano baina ya mawimbi mawili na Marjaa mbili, kwani Seyyid Khui (Mungu amrehemu) alikuwa ana maoni yenye upinzani kwa Seyyid Muhammad Shirazi kuhusu uMarjaa, na kwa kuwa mimi nilikuwa niko upande wa Seyyid Shirazi. Ilikuja fatwa hii, kama ilivyo wazi, kutokana na maswali na majibu.

Ningependa kusisitiza hapa kwamba naheshimu shakhsiyya ya Seyyid Khui na cheo chake, alikuwa ni Marjaa wa hali ya juu na kiongozi wa Hawza, naye ana daraja ya baba hata kama mtoto atapinga msimamo wa baba yake, hiyo haifanyi kuvunja heshima yake, nalo ni tukio la zamani lishapitwa na wakati, lakini baadhi ya mitandao ya Tovuti walilikuza.

**Mwandishi:** Sahih, tarehe yake ilikuwa ni 25 Mfungo Mosi 1399 (A.H.), nitaacha yaliyopita na kuangalia ya sasa, yaonekana Sheikh umepambana na upinzani mkubwa kutoka kwa wenye kufuata tu wanayoambiwa kutoka kwa mashia wa Saudia nini upeo wa usahihi wa dhana hii?

Mpambano kati ya msitari wa kufuata tu waliyoyakuta na ule unaoangalia kuleta mambo mapya uko katika mashia na masunni, ni mgongano wa vizazi na vizazi, kama umewahi kupata upinzani kitambo naamini sasa umerudi tena sana, kwa kuwa kiwango cha kuamka kwa watu kimekuwa kikubwa, na hali niliyo nayo imekuwa ni wimbi lenye uzito linaloshikiliwa na ulamaa makhatibu wasomi na wana harakati wengi.
Naeleza hapa kuwa Marjaa kubwa ya kishia hivi sasa ambayo ni Seyyid Sistani, yeye ana mpango wa kimwamko, katika mielekeo mbalimbali ya kitaifa na anashujaisha kuwe na kukurubiana na kushirikiana, na kumkubali kuwepo kwa madhehebu mengi na kutofautiana maoni. Hilo limesaidia kupunguza mpambano wa kindani kama inavyoonekana Iraq.

**Mwandishi:** Nitakuwa nasema wazi juu ya mashia wanaokupinga hivi sasa kwamba fikra zako ni bidii ya kibinafsi tu, ili upate Khumsi! Na mengineyo..zaidi ya hayo, maono yako ya kisiasa ni kwa ajili ya kujiweka karibu na serikali ya Saudia ili upate nafasi rasmi.

Kila mtu anayeshughulikia jamii, atakuwa na wapinzani, asiwe na tamaa ya kuwaridhisha wote kutokana na shakhsiyya na kazi yake, au misimamo yao wote kwa kila maoni na miongozo yake.

Kama yeye alivyo na maoni, na wengine pia wana yao,wana haki ya kuyaeleza, unachotaka katika jamii yetu ni kuongoza mbinu ya kutofautiana iwe ni kwenye mwelekeo wa kujadiliana maoni na si kuumizina na kuharibiana sifa na kila upande maoni ya sehemu yake badala ya kujisughulisha na kuwaingilia na kuwatendea kinyume wengine.

Katika uzoefu wangu juu ya haya, mimi nimefaidika kwa kuwa na wapinzani kwani nagundua mapengo na mianya ya miadi yangu, binaadamu si maasum, wapinzani wake wanampa faida kwa kuzizigundua sehemu za udhaifu wake, basi ni juu yake asiyakuze na aende mbio kaika kutengeneza na kusahihisha.Vile vile kuwapo wapinzani kunaleta hima kwa mwanaadamu na kufanya bidii ya kupanda kibinafsi kwa kiwango cha wimbi alilo nalo. Namuomba Mwenyezi Mungu na nawaombea wanipingao pia uongofu, ufanisi, msamaha.

**Mwandishi:** Sheikh Hasan, naenda upande mwingine na nakuacha na watu wako ili Mungu achague njia ifaayo zaidi kwetu sote. Umetaja kuwa Marjaa wenu ni Seyyid Sistani, nami nina makala ya Dk. Fuad Ibrahim, mtunzi wa kitabu, *Tatwawwurul fikri siyasii* anasema kuwa marjaiyya ya watu wa Qatif ukiacha Sistani huko Najaf, kuna wanaomfuata Khamenei, Muhammad Sadiq Ruhani, na wanaomfuata Shirazi huko Iran, wengine Seyyid Fadhlu Llah nchini Lebanon, je unaweza kutufungulia kitendawili hiki cha umarjai'yyah?

Kwa sababu kuchagua Marjaa kwa mashia kunakuwa kwa kiwango cha wakaazi wa mahali,wala hakuna mwongozo unaowajibisha marjaa maalum,

Kila mukallaf anachagua Marjaa ambaye atakuwa ametimiza sharti za kisharia katika hilo, na ni ijtihad na uadilifu, pia kuna sharti la ujuzi zaidi baina ya mafakihi hivyo basi, watu watategemea maoni ya ulamaa wa pale mahali pao walioko iwe ni Qatif, Ahsaa na Madina, na kila mmoja katika hao ulamaa , kadri ya ilimu yake, anachagua Marjaa ambaye anaridhika naye na kuwaongoza wafuasi wake wamfuate.

Hapa ndio kunakuwa na idadi ya Marjaa na mara nyingi kunakuwa na marjaa anayefuatwa na wengi ambaye kwa sasa ni Seyyid Sistani, hakuna tofauti za muhimu sana kati yao, ila katika baadhi ya mas-ala machache ya kifiqhi, na hutokea baadhi ya tofauti kati ya Marjaa katika msimamo ya kisiasa na au ya kimafunzo, au njia za kuongoza uMarjaa, lakini akisi hii katika tofauti za kimiji huwa ni chache, kwani ulamaa wa miji ndio wanaoathirika kwa daraja ya mwanzo katika yanayotokea kwa jamii.

**Mwandishi:** Hebu niruhusu kwa swali la wazi hapa, mfuato huu wa kifikra hauzai mfuato mwingine kama wa kisiasa mathalan?

Ukiwa unakusudia mfuato wa kisiasa, kwamba Marjaa wa kidini ndiye anayewathibitishia mashia katika miji yao misimamo yao ya kisiasa ya nchi na namna ya uhusiano wao na serikali, hii si sahihi kabisa, kwa mambo mawili:

La kwanza, ni kujitoa kwa Marjaa wengi wa kishia kuingilia mambo ya kisiasa na kuangalia kutoa fatwa katika mambo ya kisharia, ambapo uhusiano kati ya mashia na Marjaa ni juu ya mambo haya.

La pili, huenda akainglia Marjaa jambo la kisiasa katika nchi yake, kwa sababu yeye ana maoni ikiwa hali itamhitajia kufanya hivyo, lakini kamwe hajiingizi katika mambo ya siasa ya nchi nyingine, huziachia hayo nguvu za kishia zilizoko kwenye miji hiyo, kwa sababau wao ndio wajuao zaidi hali za nchi yao.

Kama mfano wa hivi karibuni, ilivyotokea Bahrain kabla yauwazi ulioongozwa na mfalme wa Bahrain Sheikh Hamad bin Isa na baada yake, kwa mfano Marjaa wa hapo hawakujiingiza katika mambo ya uchaguzi wa wabunge mashia wakagawanyika, ambapo baadhi walishiriki na baadhi hawakushiriki, lakini kushiriki na kutoshiriki kuliamuliwa na uongozi wa kitaia bila ya kuingilia Marjaa wa huko.

Jamii ya masunni na mashia huchukua elimu ya kisheria na hukmu za kidini kutoka kwa ulamaa waaminifu popote walipo, mipaka ya kisiasa haiwazuii kufaidika na elimu na maoni yao, waislamu wa nje ya nchi anayoishi Sheikh wa msikiti wa Ijumaa wa Azhar (Misr) huchukua maoni yake, na ulamaa wakubwa kama marehemu mufti Ibn Baaz waislamu wa miji mbalimbali wakichukua maoni yake, pia Sheikh Yusuf Qardhawi naye ana nafasi ya marjaiyya katika miji mingine ya kiislamu wala hakuna anayezingatia kuwa kuchukua elimu ya kisharia kutoka kwa fakihi anayetegemewa nje ya nchi huko ni kufuata kisiasa.
Mimi naona kuwa ni bora uongozi (marjaiyya) wa kidini uwe kutoka kwenye jamii ile na nchi anayoishi. Kabla ya miaka hamsini hivi, marjaiyya ya mashia Qatif na Ahsaa yalikuwa ni ya hapo hapo. Nataraji Hawza za kishia zilizoko Qatif na Ahsaa zitachukua fursa ya zitusaidie kupata wenye kiwango cha Marjaa inshallah.

## Kazi ya marjaiyya (uongozi wa mujtahid) wa Shia

Umekanusha ufuasi wowote wa kisiasa kwa Marjaa, twataka kujua kazi hasa ya Marjaa wa kishia, lau ungelitufafanulia, tunasikia hawa Marjaa lakini hatujui kazi zao hasa na upeo wa harakati zao.

**Sheikh:** Wajibu wake ni kama ufuatavyo:

1. Kufanya *istinbat* katika hukmu za kisheria na kujibu maswali.

2. Kuilea hawza ya elimu kwa kusomesha kiwango cha utafiti wa kiwango cha juu katika Fiqh na Usuul yake, kuangalia mahitaji ya waalimu na wanafunzi na kutatua matatizo Hawza inayokumbana nayo ya kisiasa, kijamii na ya kipesa.

3. Kutoa *ijaza* na uwakala kwa ulamaa katika jamii mbali mbali waweze kuzinakili fatwa zake na wapokee haki za kisheria kwa niaba yake, na wasimamie mambo ya dini yanayohitaji idhini ya mujtahid, kama kuhukumu.

4. Kuwa na nafasi ya baba na kuilea jamii kwa kuwashujaisha na kusaidia taasisi za dini, na kugawanya Khums kwa mafukara na wahitaji.

5. Huenda akasimama Marjaa kwenye nafasi ya mambo ya kisiasa ikiwa maslahi ya dini yatahitajia hivyo na hali zikiruhusu.

**Mwandishi:** Naomba unifafanulie zaidi na utoe mifano katika hali yetu sisi masunni.

**Sheikh:** Kufananisha kwa kazi inayofanywa na Marjaa wa kishia ni kama ile inayofanywa na Mufti katika jamii ya kisunni, japo kuna tofauti pia, kama vile kuchaguliwa kwake, ambapo kisunni kuteuliliwa kwa Mufti wa kisunni huwa ni rasmi kiserikali, ambapo kishia huteuliwa tu kitaifa.

**Mwandishi:** Kuna majina ya mashia mfano Ahmad mwandishi, Ahmad Al-Kasrawi aliyeuliwa na baadhi ya mashia Kuwait, pia Al-Barqai' na Musa Al-Musawi na wengineo, walioikosoa misingi na kaida za Shia, mnawaangalia vipi hao?

Mwenye kuwa na maoni yanayopinga dharura miongoni mwa dharura za madhehebu huyo huangaliwa kuwa ametoka nje ya madhehebu, lakini yumo kwenye uislamu madam anamuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake (s.a.w.w.) na Siku ya Mwisho. Kuna tofauti kati ya aina mbli za watu hao, kuna aina ya yule mwenye maoni ya kupinga madhehebu bila ya kuchanganya na mengine, huyu hufanywa mjadala naye ili arudi kwenye madhehebu, kama hakutosheka na kuzidi kueneza maoni yake , hapo ulamaa watamjibu na kueleza makosa yaliyo katika maoni yake mpaka isathiri watu wengine katika madhehebu.

Na aina nyingine ni ya yule anayeanzisha maoni kwa uadui dhidi ya madhehebu na jamii, akishirikiana na wapinzani au na upande wenye shaka, hapo inabidi achukuliwe msimamo mkali dhidi yake kwa kiwango cha kijamii na kielimu.

Saa nyingine hutokea dhana mbaya, na misimamo akisi kwa sababu ya jazba kali ya kidini kwa wamashariki kwa ujumla, wakiwa na dini na madhehebu mbali mbali, ambapo baadhi ya nyakati kunakuwa ni kwa sababu ya haki za kibinaadamu na kutoa maoni tu.

**Mwandishi:** Nitaacha majina niliyokutajia, nirudi kwenye asili kuhusu uadilifu na insafu, nimeishi kwenye matukio hayo, je kuna uongozi wa kisunni ulioathirika na fikra za baadhi ya maimamu wenu wa kishia, kwa kiasi cha mlivoathirika nyinyi na waandishi na wanafikra wa kisunni?

Ni maarufu kwamba kuna wanavyuoni na wanafikra wa kisunni walioathirika na fikra za Seyyid Jamalu din Al-Afghani, k.v. Sheikh Muhammad Abduh, na Sheikh Muhammad Rashid Ridhaa, jarida lake alilokuwa akilitoa mjini Paris liitwalo *Al-Urwatul wuthqaa* lilileta mwamko wa kiislamu wa kisasa.

Na najua pia vitabu vya Seyyid Muhammad Baqir Sadr k.v. *Falsafatuna*, *Iqtiswaduna* na *Al-Bank laa ribaa fil islami* vimekuwa ni vitabu vinavyotegemewa sana na ulama na wanafikra wengi wa kisunni.
Na baada ya mapinduzi ya kiislamu ya Iran, elimu ya Shia ilifunguka sana kwa ulamaa wa kisunni, na wakafaidika sana na tajriba ya kiiran, kisiasa na kifikra.

Lakini inawezekana kusema kuwa kufunguka kwa elimu ya Shia kwa Sunni ni kukubwa zaidi kuliko ya Sunni kwa Shia, na sababu ni kuwa mashia hawaishi na kujifungua kunakowazuia kuangalia maoni ya wengine, wala hawakuogopa kuathiriwa na maoni ya wengine, ambapo kwa Sunni tunaona baadhi ya jambo hili.

Mafunzo ya Shia ni tirathi muhimu katika nyanja mbali mbali, haifai kwa ulama au msomi wa kisunni kujinyima kuisoma, na kufaidika nayo na hasa inapohusika na vipawa na sera nzuri za maimamu wa Ahlul Bayt (a.s.).
Uislamu unatushujaisha kufungua kuangalia rai za wengine ili tujue ukweli wake, huenda kuna kitu tutafaidika nacho.
Mwenyezi Mungu mtukufu anasema: "..wale wanaosikiliza maneno wakayafauata yaliyo mazuri zaidi. Hao ndio aliowaongoza Mwenyezi Mungu, na hao ndio wenye akili." Imekuja Hadith katika Tirmidh, kutoka kwa Abu Hurayra, amesema: 'Mtume (s.a.w.) amesema: "Hekima ni kitu kilichompotea Muislamu, popote anapokipata ana kahi zaidi ya kukichukua."

**Madhehebu ya Jaa'fariyya je ni madhehebu ya tano?**

Samahani Sheikh Hasan, wewe wewe hapa upande huu unatoa fikra ya kishia kwa mkabala na ya kisunni, kama kwamba, katika mazungumzo yako awali, unasema kuwa madhehebu ya Ja'afary ni ya tano, je ninavyohisi ni sahihi?

**Sheikh:** Bila shaka, madhehebu haya yana msingi katika historia yake, ulamaa wakubwa wa kisunni na maimamu wao wamesoma kwa maimamu wa Ahlu Bayt, hapa nakumbuka neno la mwanachuoni mmisri maarufu, Sheikh Muhammad Abu Zahra katika kitabu *Al-Imamu Sadiq*, aliposema: "Hawajawahi kuwa pamoja katika kukubaliana ulama wa kiislamu pamoja na tofauti ya mataifa yao katika jambo kama walivyokubaliana katika ubora na elimu ya Imam Jafar Sadiq, maimamu wa kisunni waliokuwa zama zake, walisoma kwake."

Imam Malik (r.a.) alisoma kwake, na tabaka yake, kama bile Sufyan bin U'yayna na Sufyanu Thawry, na wengineo wengi.

Pia Abu Hanifa, japokuwa walikuwa rika moja, na alimchukulia kuwa ni mjuzi zaidi wa watu wote na walichukua kwake riwaya ya Hadith wengi katika Tabiina, akiwamo Yahya bin Said Al-Answari, Ayyub Sakhitani, Aban bin Tagh'lab, Abu Umar bin A'laa na wengineo katika maimamu wa Tabiina katika Fiqh na Hadithi, na hivyo ni juu ya wale waliopokea kutoka kwake katika waliowafuata tabiina, na waliokuja baada yao , na maimamu mjtahid tuliowataja."

Ikiwa maimamu wa kisunni wana madhehbu, je itakuwa ni kuongeza ikiwa Imam Jafar na maimamu wa Ahlu Bayt nao watakuwa na madhehebu?

Kuna baadhi wanashuku wanayopokea mashia kutoka kwenye madhehebu ya Ahlu Bayt kisha hawaleti njia ambazo zinazingatiwa kuwa ni sahih, natija inakuwa ni: Hakuna madhehebu ya Ahlu Bayt. Kila imam katika maimamu wa madhehebu yake yalikuja kwa njia ya wanafunzi wake walio karibu naye, na pia madhehebu ya Ahlu Bayt tunayapata kwa njia ya wanafunzi wao walikuwa karibu nao, ikwa sisi mathalan tutashuku mapokezi ya Abu Yusuf Al-Qadhi na Muhammad bin Hasan Shaybani na Zafar bin Hudhayl kutoka kwa Sheikh wao Abu Hanifa, basi madhehebu yake tutayapata kutoka wapi?
Ikiwa hatukubali mapokezi ya Swaleh mtoto wa imam Ahmad, ndugu yake Abdallah bin Ahmad, Ahmad bin Muhammad Al-Ashram, Abdul Malik Al-Maymuni, Ahmad bin Al-Maruzi, Ibrahim bin Is-haq Al-Harbi, na wengineo,

na aliyokusanya baadaye Abu Bakr Al-Khilal kutoka kwa imam Ahmad bin Hambal, vipi tutaweza kufikia madhehebu yake na rai zake za kifiqhi?
Na hali ni hiyo hiyo, hutapata madhehebu ya Ahlu Bayt na fiqh yao ila kupitia kwa wanafunzi wao walio karibu nao, hiyo haina maana ya kukubali kila kinachopokewa kutoka kwa Ahlu Bayt, kama ambavyo haiwezekani kukubali kila kinachopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) pia kutoka kwa maswahaba na kutoka kwa maimamu wa madhehebu, bali lazima kufanya uhakiki na kutafiti na kkuangalia kwa jicho la mazingatio.

Kwa hiyo, madhehebu ya Jafar yako, na wafuasi wake si wachache sana kama wa madhehebu ya madhehehebu manne ya kiislamu, na haisihi kuzidisha katika sharia, kila madhehebu yanaona kuwa wafuasi wake ni wengi, hapana budi tujuane, tuheshimiane na tusaidiane katika mema na kumcha Mungu kama alivyotuamrisha Mwenyezi Mungu.

**Mwandishi:** Sheikh hapa nitasimama kidogo mbele ya mazungumzo yako, mwanzo, maimamu wa Ahlu Bayt wana daraja na heshima na yaliyonukuliwa kutoka kwao kwa sanad sahih yanazingatiwa, kwa msingi wa kupewa umuhimu zaidi si kwa kustahiki kurithi, kama mnavyoitakidi nyinyi mashia, hakuna matatizo makubwa katika Fiqh yao, ila yapo katika wanayonasibishwa nayo kutokana na makosa na uzushi ambayo ulama wa kisunni wanawasaisha wao na mambo hayo.
Nilijiuliza juu ya maoni rai ya Ahlu Bayt katika mambo ya ki-fiqh, nasawirisha kuwa tatizo si katika masuala ya kifiqhi bali katika itikadi wanazonasibishwa nazo, je kuna utengano wa kiitikadi na mgongano wa kimisingi?

**Sheikh:** Mashia hawasemi kuhusu haki ya kurithi, bali wanasema juu ya nassi zilizopokewa juu ya uimamu, imethibiti kwao katika silsila ya kizazi cha Mtume kitukufu, hii si aibu. Mwenyezi Mungu ametaja juu ya kuendelea utume katika kizazi cha Nabii ibrahim (a.s.): "Na tukampa yeye Is-haq na Yakub na tukajaalia kitabu na utume katika dhuriya wake."

Ama kuhusu uzushi hata mashia pia wanamtakasa Mtume (s.a.w.w.) na Ahlu Bayt wake kutokana nayo, lakini kuona kuwa kila linalopinga maoni yenu ni uzushi na ni makosa hii haifai, na ni haki ya wengine waangalie yenu mliyo nayo pia. Yafaa tuingie kwenye ukumbi wa mdahalo kwa adabu na kwa njia ya Mtume (s.a.w.w.).

Inapokuwa ni kawaida kila upande uamini kuwa uko kwenye haki, basi si kawaida kumkubali upande mwingine na kukubali kufungua aliyo nayo na kuyajadili na mwenzake. Kisha kupinga madhehebu ya Ahlu Bayt si upande wa itikadi tu kama ulivyosema, bali hata upande wa kifiqh.

**Mwandishi:** Mwenyezi Mungu Mungu atulinde sote. Na nataraji Sheikh uelewe tabia ya maswali katika mahojiano, katika mazungumzo yako ya mwanzo, wewe unazungumza ukisema shia, sisi mashia...mashia wamesema...mashia wamefanya...naona kama suala hili lahitaji ufafanuzi kwani kama ajuavyo mtu wa kawaida kama mimi kutoka kwa Ahlu Sunna, kwamba chini ya Shia kuna makundi mengi yasiyokuwa Jaafariyya au Ithna-ashariyya, sijui mizani yako iko wapi na sijui kwa nini umeweka fikra ya Shia kwenye dhehebu moja tu? Na unatumia kuita Shia tu, unasarifu ushia kwa nani?

**Sheikh:** Je Sunni wote wana maoni mamoja? Hakuna maashaira na muutazila, wenye rai na wenye hadithi, wenye madhehebu manne na madhehebu ya Dhahiri na mengineyo? Je wanakuwa ni wengi? Pia kuna masalafi, kuna masufi, lakini najua kuwa unapozungumzia madhehbu ya Ahli Sunna unakusudia masalafi walioshikamana na Hambali, ni sehemu isiyodhihiri kuwa ni kubwa sana kuliko ukumbi wa Ahli Sunna, nawe wajua kuwa mimi ni wa madhehebu ya Imamiyya, Ithna-ashariyya na nazungumzia madhehbu yao. Na inapotajwa Shia inakusudia wao kwani wao ndio wenye nafasi kubwa zaidi, wanapotajwa wasiokuwa wao, nitaongeza kitu, sasa je uteitei wa Shia uko wapi?

**Mwandishi:** Tukiachia pale uko Saudia ukifanya tablighi na kuinua roho ya kiislamu baina ya watu, hapo Qatif ulikaa muda gani, na kituo chako cha pili kilikuwa wapi?

Nilibaki Qatif mpaka baada ya Ashura mwaka 1400 (A.H.) ambapo nilienda Teheran, katika jamhuri ya kiislamu ya Iran na hiyo ni baada ya yaliyotokea Qatif katika siku ya Ashura, watu wa jimbo hilo walikasirika dhidi ya wamarekani ambao walikuwa wakitoa vitisho dhidi ya serikali ya kiislamu ya Iran wakati uliposhikwa ubalozi wa Marekani ulioko Teheran, ilikuwa siku ya Ashura ndio fursa ya vijana wenye kuyapenda mapinduzi ya kiislamu ya Iran na wanaochukia utawala wa kimarekani, fursa ya kuonyesha hisia zao wakati wa kumuomboleza Imam Husein ambao mashia wa sehemu mbali mbali wanaufanya, maombolezo yalikuwa yamekatazwa kufanywa nje ya kumbi (*Huseiniyya*-sehemu zinakofanywa maombolezo) kuinua picha za Imam Khomeini.

Serikali ya Saudia ikachukulia kuwa hii ni siasa, na ni maandamano na ikaafikiana na tukio lililotokea kwenye haram la Jahiman Al-Utaibi. Vyombo vya usalama vikachukua hatua kali mpaka kufikia kupiga risasi na kuua baadhi ya watu, mwisho wakashikwa watu wengi waliokuwa wakiandamana au kutuhumiwa kushiriki katika miji ya Qatif, Safwa, Sihat na sehemu nyingine.Hii ndio ilikyokuwa sababu ya kutoka kwangu nchini.

**Mwandishi:** Nisamehe Sheikh, lakini wewe unayafikisha mambo zaidi ya mipaka yake, ambapo akili haikubali, lau ungekuwa ni kwenye sehemu rasmi ukayaangalia mambo haya kisiasa, iwe ni katika harakati za Jahiman za kisalafi au au upande wa mapinduzi ya kiiran na mwito wa Khomeini wa kimapinduz na hasa katika Bara Arabu, Simtetei hapa mwanasiasa nikiangalia mambo yalivyo hasa, na lazima serikali iwe kali, tukio hili lilikuwa na mrengo wa kisiasa unaotishia umoja wa nchi, na si kama ulivyosema ni suala la kiibada tu.

Mazungumzo yangu juu ya yaliyotokea ilikuwa ni kuendeleza kujibu swali lingine, na niliyoyataja ni picha kwa ufupi tu si kwa lengo la kufafanua na kujadiliana katika tukio, katika jambo hilo hakuna kulifanya dogo, kama ambavyo hakuna haja ya kulifanya kubwa kama unavyoonyesha wewe.

Ikiwa mambo huhukumiwa kwa natija zake, hiyo imesababisha kupanda hali hiyo, ikaendelea hali hiyo kiasi miaka kumi na minne, mpaka kukapatikana kufahamiana na serikali na udugu ukarudi mnamo mwaka 1994 (A.H.).

**Mwandishi:** Samahani Sheikh, unataka niandike mistari michache tu na mambo hayo katika historia ya MsHia wa Saudia ya kisiasa, yametimu miaka 14. Nauliza, je serikali ya Iran ilikuwa ina msaada wowote na kuwaelekeza nyinyi katika upinzani huu kwa serikali ya Saudia, au ni upokezi tu kama alivyofanya mfalme Faisal kwa Ikhwanul Muslimina?

Ni haki yako kama mwandishi wa gazeti uwe na pupa ya kazi yako, lakini mimi nina ikhlasi juu ya kadhiya hii ya nchi, kulingana na hali nyeti za kimaisha.

Swali lako kuhusu nafasi ya Iran. Anga za kimapinduzi wakati ule zilikuwa zinatokota dhidi ya Marekani na tukio la kutekwa nyara ubalozi wa marekani na mateka wake, na Marekani kujaribu kuingia kijeshi Iran, zikafanya lugha ya Iran iwe ya kimapinduzi na hivyo athari zake kupatikana nchini na kwenye nchi zingine za kiislamu kama ilivyokuwa wazi kwa mtu aliyeishi kipindi kile au aliyesoma habari zake.
Lakini wairan walikuwa wakijishughulikia wenyewe hata bado walikuwa hawajamakinika kujenga dola yao mpya, kisha wakawa na matatizo makali ya ndani, mara wakashtukizwa na vita na Iraq haya yote hayakuwawezesha kusaidia upinzani Saudia.

Tulikuwa tukifaidika na kukaa Iran, ikiwa mfalme Faisal aliweza kuwapokea Ikhwanul Muslimina na hata wengine kuwapa nyadhifa na kuwapa pesa kama ulivyosema, sisi hatukupata kama hayo Iran, tulikuwa tukijisimamia maisha yetu sisi wenyewe, hakuna hata mmoja wetu aliyepata wadhifa wowote, bali tulisumbuka kupata vibali vya kuishi walipoanza kupanga utaratibu wa kiusalama nchini humo.

Ndio, tulikuwa na urafiki na uhusiano na baadhi ya ulamaa na viongozi wa mapinduzi, kama nilivyosema hapo awali, na hapo ndipo tulifaidika na kuendesha baadhi ya mambo yetu.

Kutilia umuhimu wairani kwa Saudia kulidhihiri kwa yale yaliyotokea Makka waliyoyayafanya walipokwenda kuhij imwaka 1408 (A.H.) - (1987 A.D.). Nasi tukathibitisha kutoka Iran ili tusiwe ni chombo cha mpambano uliokuwa utokee wakati huo, ili tusiwe ndio sababu ya vita vya upande wa Iran dhidi ya Saudia.

Tulitoka Iran, tukahamia Syria na Lebanon, na baadhi ya ndugu zetu wakahamia Ulaya, ili tuhifadhi kuwa huru kwetu, na tusiwe ni chombo cha mpambano ambayo hatukupenda kuwamo ndani yake.

**Mwandishi:** Ni wangapi uliokwenda nao Iran?

**Sheikh:** Ni vigumu kutaja idadi maalum.

**Mwandishi:** Takriban...

Waliokuwa katika kazi yetu kisiasa walikuwa ni wachache, kama makumi hivi, lakini kuna waliokwenda kusoma dini, kuna waliokimbia, baadhi yao walikaa kwa muda mchache tu kisha wakarejea. Idadi yao inaweza kuwa mamia.

**Mwandishi:** Upinzani wenu ulikuwa vipi, je ni kama anavyofanya Saad Al-Faqih mathalan, idhaa na kuandika tu?

Kazi yetu ilikuwa:

1. Kukuza anga za fikra, kisiasa na kiuongozi.
2. Matangazo na kuelimusha kupitia vitabu, magazeti, na kurekodi hadith na mihadhara.
3. Harakati za kisiasa kufafanua kadhia yetu sehemu mbalimbali.

Tulikuwa tukikataa kutumianguvu kama njia ya ya upinzani, hivyo hatukuiunga mkono. Marjaa tuliyekuwa tumeshikamana naye ni Seyyid Shirazi aliyekuwa akiitangaza nembo ya 'Hakuna kutumia nguvu.' Aliandika na kuhutubia mara nyingi dhidi ya kutumia nguvu na jeshi, kwa sababu kufanya hivyo ni kinyume na mafunzo ya dini na ni sababu ya kuvunja yaliyoharamishwa na kukosa usalama na majibu ya watu kwa anayefanya hivyo. Na mara nyingi hayapati natija nzuri.

**Mwandishi:** Umesema kuwa matatizo ya kisiasa yalipoanza kati ya Saudia na Iran, mlijiweka mbali na mpambano huo, sijui ee Sheikh Hasan, je hamkuhisi kwamba nyinyi, kabla ya matatizo hayo, mlikuwa ni kama karatasi ya kisiasa mkononi mwa Iran dhidi ya Saudia?

Wakati huo hakukuwa na mpambano kati ya Saudia na Iran nasi hatukuhisi kuwa ni karatasi ya mtu yeyote, na hatukubali hilo, lakini kuna ukweli ambao ni lazima niutaje: Ni kwamba, hali, katika nchi yoyote zisipowapa nafasi wananchi wake, hilo litawafanya wajitegemeze na kwengine kama vile ambavyo uhusiano na wengine unakuwa ni wa maslahi wanayofaidika nao pande mbili, inafaa kwa mwananchi mkweli awe na ikhlasi na nchi yake, asiwe ametegemea matakwa ya nje dhidi ya maslahi ya nchi yake.

**Mwandishi:** Samahani...Samahani.. lakini ni kwa sbabu ya matatizo yaliyotokea na Saudia kusaidia Iraq na hilo lilitangazwa.

Sahihi, na hilo ndilo lililotupa fursa ya kubaki Iran, na kufanya siasa lakini wairani walikuwa na tahadhari kufungua sehemu zingine kwa upana zaidi, hawakutaka kuingia mzozo na dola za jimbo hili, huku wakisumbuliwa na vita, na shinikizo la marekani na Ulaya lilikuwa pia ni kubwa kwao, hivyo hawakujiingiza matatani na Saudia ila kabla ya matukio ya Makka. Na hapo tulihamia Syria, Lebanon, na ndugu zetu wengine Uingereza.

**Mwandishi:** Nisamehe Sheikh, kwa ufunguzi wako katika upande huu kwa kweli siasa imeniingia, bado nakanganywa, kwani kwenda kwenu Syria ambayo ina uhusiano mzuri na Saudia, hamkuhofia, mathalan, juu ya nafsi zenu serikali ya Saudia itaiomba ya Syria mshikwe na mkabidhiwe kwa Saudia?

Tuliichagua Syria kwa sababu ilikuwa ndio nchi pekee ya kiarabu iliyokuwa ikiionea huruma Iran katika vita vyao na Iraq, na watembezi kuoka Saudia walikuwa wakiizuru, hii ilitupa fursa ya kukutana na jamii, pia maisha huko ni mepesi, pamoja na hawza za kishia zilizoko jimbo la Sayyida Zainab karibu na mji wa Damascus.

Tulipachagua ili pawe ni mahali petu pa kuishi, si kwa ajili ya kufanya mambo ya kisiasa, hilo wasyria hawaliruhusu, lakini kuwa karibu na Lebanon kulituwezesha kupata nafasi tuliyoikosa Syria.

Siasa ya Syria ilikuwa ni kuwaheshimu wakimbizi madam hali yao ni ya kufuata kanuni na hawapendi kinyume na nchi zao walizotoka, mfano wa hivyo ni kuwa, pamoja na uhusiano mzuri wa Iran na Syria huko Syria kuna baadhi ya wakimbizi wa kiiran wanaoipinga serikali ya kiislamu ya Iran.

Kwa kweli kuishi kwetu Syria ilikuwa ni majaribio ya kimaisha, Lakini uaminifu juu ya msimamo wetu na ikhlasi yetu uilikuwa ukitusaidia kustahmili kiasi hicho.

**Mwandishi:** Nitajaribu kuangalia maana ya Syria kuwakubali nyinyi mkae, ni juu yako useme kama ni sahihi au nimekosea, naona hiyo ilikuwa ni kama majibu ya Saudi, yasiyo ya moja kwa moja, ya kule kuwachukua Saudia wafuasi wa Ikhwanul Muslimina kuishi Saudia mwanzo wa miaka ya thamanini, je na Syria si ilikuwa kama inajibu kwa kuwapokea nyinyi?

Sijui kilichokuwa akilini mwa viongozi wa Syria, lakini walituchukulia ni kama sehemu ya watu wa hawza za kielimu katika jimbo la bibi Zainab, ambapo tulikuwa tukisoma, kusomesha na kufanya nishati za mafunzo ya kijamii, na si jingine.

**Mwandishi:** Mlikaa miaka mingapi Syria?

**Sheikh:** Yapata miaka sita (1409-1415 A.H.).

**Mwandishi:** Je ulikuwa na uhusiano na Marjaa wa kishia huko? Na je Hizbu llah ilikuwa ina matawi huko?

**Sheikh:** Syria hakuna marjaa, kuna Hawza tu, alizozianzisha Seyyid Hasan Shirazi mwaka 1369 (A.H.) - 1975 (A.D.), naye ni nduguye Seyyid Muhammad Shirazi, sisi tulianzisha Hawza maalum kwa vijana wetu 'Hawzatul Imam Swaadiq, katika jimbo la Bi Zainab.

## Uzoefu wa maka mingi

Muda huu tunaozungumza hakika umeona mengi katika hisia za kuunga mkono mapinduzi ya Iran, na pande mbili za kiislamu zimepitia kwenye mawimbi makali yaliyoishia kwenye hali ilivyo hivi sasa, mimi niko mbele ya Sheikh Hasan sasa, aliyepitia uzoefu wote huo, sasa unazionaje zama zile na hotuba zako bado zinafaa? Au uzoefu umekufunza kurudi nyuma kwenye zingine na ubadilishe mtindo wako wa tabligh, je una nasaha gani kwa kizazi chetu kipya na cha kiislamu kwa ujumla ili kisianguke kwenye kasoro zako, na kifaidike na pande nzuri za uzoefu wako?

**Sheikh:** Naamini kwamba tuliyoyafanya wakati ule yalikuwa na faida kulinganana wakati ule, kimajmbo na kiislamu, na sijutijuu ya mapinduzi ya kiislamu, nayaonani mwanzo wa mwamko wa kiislamu, yalikuja katika njia ya uma kushikana na na dini yake na kukataa miongozo ya kimagharibi na utawala wa kimarekani na mashia na masunni wengi waliyaangalia hivi.

Sasa kuhusu makosa yaliyofanyika kwenye mapinduzi ya serikali ya Iran, hili ni jambo liko na hasa mwanzo ilikuwa ni wajibu kuwasaida kuyavuka makosa hayo, lakini la kusikitisha ni kuwa, mtazamo wa kitaifa uko upande mwingine na kuathiriwa na matangazo ya kigeni kuko upande mwingine,

Hayo ndiyo yaliyofanya hali ya Uislamu wa Iran iwe ni yenye kutupiwa maswali. Ilidhihirika kuwa walioongoza upinzani kwa Iran ndio walioongoza upinzani dhidiya Saudia k.v. Serikali ya Iraq iliyoanguka na idara ya Marekani.

Haya ndio maoni juu yangu juu ya mkondo huo. Ama kuhusu upeo wa kuzungumzia mfumo wake, hakika mwanaadamu hukua na kukamilika kwenye kipindi cha uzoefu na mafunzo kama ambavyo uongozi wa Marjaa ni muhimu kwa ajili ya kuziba mapengo na kuondoa makosa, aidha kubadilika kwa hali kunahitajika katika kubadillika mazungumzo na mfumo, sote twajua kwamba mfumo wa utume wakati wa nyuma haukuwa sawa na wakati wa Makka, pia katika baadhi ya sehemu.

Nawasihi ndugu zangui na mimi wasiache msimamo wao si kwa hamasa tu, bali waziangalie miji, akili na jamii zao kwa jicho la mazingatio, mtindo unaofaulu katika nchi moja huenda usifaulu kwa nyingine.

**Je Saffar ni Khomein wa Qatif?**

Najiuliza Sheikh, mtu anayesoma namna unavyomuunga mkono Khomeini na uwanamapinduzi aliokuwa nao, huenda ikasemwa hivi sasa Sheikh Hasan Saffar atashika nafasi yake Qatif na atafanya kazi ileile aliyoifanya Khomeini, wasemaje hapo.

**Sheikh:** Hapo kuna udunishaji, hakuna haja kabisa ya kulinganisha, si katika sifa ya kiutu, kihali, kijamii na wala ya kisiasa. Imam Khomeini alikuwa ni fakihi na marjaa, na mimi ni mwanafunzi mdogo tu, yeye ametoka sehemu ambayo wengi ni mashia, Iran, na mimi kwetu

mashia ni wachache; yeye alikuwa akipinga serikali ya Shahinshah (Shah) alliyetaka kuugeuza umma wa kiislamu, na alishikana na utawala wa kizayuni; ambapo sisi tunaishi katika serikali ya inayopinga kushinikizwa na wamagharibi, na kukataa kuwapo uadui wa kizayuni. Na tofauti nyingine nyingi.

**Mwandishi:** Kwa hivyo Sheikh Hasan, ningependa kuuliza mfumo mnaoufuata hapa Saudia.

Ratiba yetu baada ya kurejea nchini iko katika mambo mane:
La kwanza, kuitengeneza jamii kwa ndani kwa kueneza mfumo wa sawa, kupitia njia zilizoko, kusaidia taasisi za kheri kwa jamii, na kumshujaisha kila anayetaka kunufaisha jamii na kuitumikia kwenye maendeleo yake.
La pili, kufungua nyanja za nchi kwa kuweka daraja la kuwasiliana na wananchi wengine, ili kuiacha ile hali ya kukatana kimadhehebu, kujifungua kikabila, na kutoa mafunzo katika upande huu.
La tatu, kuwasiliana na wahusika na viongozi wa nchi ili kutengeneza kadhia husika, na kuondoa matatizo yaliyoko, hii inasaidia kuunganisha uongozi na wananchi.
La nne, kutoa mchango juu ya mambo yanayohusu nchi kwa ujumla katika nyanja mbali mbali.

**Mwandishi:** Naingia kwenye upande wa pili ambao mwenye kufuatilia kama mimi anaujali. Nyinyi mna fatwa hasa katika kadhia za kujiunga na jamii, japo katika upande wa kwanza mna maoni mapya, kama vile fatwa zenu katika Ashura ya kujitolea damu, na mengineyo, je mmetufafanulia fikra hii?

**Sheikh:**Kujiunga katika jamii ni kadhia nzuri inafaa kila mwenye mwamko afanye bidii sana katika, hii nni nchi kubwa, ambayo umoja wake umehakikika kwa mkono wa muasisi wake mfalme Abdul Aziz (Mungu amrehemu), nchi hii ina majimbo na makabila mengi, huku ikiunganishwa na lugha moja ya kiarabu na dini moja ya kiislamu, alhamdu lillah.

Lakini pupa ya kimaumbile ya kijamii ni juu ya mambo yake na kuyaheshimu, kupanua imani ya nchi nzima, hali hii inapodhoofu, ndipo kunapozidi kushikamana kwa wengine na mambo yao, ndipo nchi inapokuwa ni uwanja wa mapambano baina ya mambo fulani yaliyojigawanya, huku nchi ikiathirika na kuwapo mafunzo ya wengine katika jamii, na kuwa dhidi yake tofauti ya kijamii au ya kimadhehebu, au fikra hii inazuia kuungna kinchi na kufanya baadhi ya watu ni kasha linalojitosheleza lenyewe tu.

Umpja wa nchi kiislamu ni amana shingoni kwetu, tuna majukumu ya kuutilia mkazo, kufanya upya na kuondoa vumbi linaloingia kwenye uso wake mweupe pe pe pe.

Upande huu wa Uislamu wa nchi ndio umenishughulisha nikatoa mihadhara mingi nikiwaomba jamii yetu kujifungua zaidi katika sehemu zao, na kuonyesha mapenzi ya nchi yao, kuutukuza ushirikiano kiujumla, na kutilia umuhimu kadhia hii kwa uangalizi maalum ili kuondoa athari za usongo wa zamani na kupambana na magumu yaliyopo.

Na nikaandika vitabu na tafiti katika maudhui mbalimballi k.v. *At-taa'ddudiyya wal-hurriyya fil islaam, At-tasaamuh wathaqaafatul ikhtilaaf, At-tanawwuu' wat-taa'aayush, As-slmul ijtimaai' muqawwamaatuhu wahimaayatuh, Kayfa naqraul aakhar, Al hawwar walinfitah a'lal akhar, At-tatwaau lilwahda na vinginevyo.*

Na alhamdu lillah mwito wa mrithi wa mfalme w majadiliano ya nchi, na baadhi ya walinganiaji na wannafikra wwlishiriki katika fikra hizi kupitia magazeti na waandishi kuku wakiandaa uwanja wa kinchi zaidi kuliko hapo zamani ili kuhakikisha hali ya muungano na kuuenzi.

**Sheikh**: Ama kuhusu kulingani kwetu kujitolea damu wakati wa Ashura kila mwaka hili limepokewa vizuri na mashia na kushinda benki ya damu ya jimbo, tulianza Qatif mnamo mwaka 1416 A.H. Na kuenea mpaka Ahsaa mwaka 1424 A.H. Na Bahrain miaka mitatu iliyopita, pia jimbo la Bi Zainab Syria na nataraji siku ya Ashura iwe siku ya kimataifa ya kujitolea damu, kila mtu kujitolea kwa ajili nya mwanaadamu mwenziwe mgonjwa.
Na hii si fatwa, kwa sababu mimi siko katika daraja ya Marjaa na kutoa fatwa, bali ni mwito wa kupata faida na kukumbuka kufa shahid kwa Imam Husein (a.s.).

### Mandhari ya Ashura na picha yake isiyofaa

Lakini ni kinyume cha mnavyofanya, vyombo vya habari viyeleza kuwa mnamwaga damu na kujipiga vichwa, hii inaleta picha isiyofaa kwenu.

**Sheikh:** Haya mandhari uyaonayo katika baadhi ya jamii ya kishia siku ya Ashura yana hitilafu ndani ya Shia yenyewe. Ameandikakwa kuyapinga mmoja wa ulamaa mashuhuri wa kishia Seyyid Muhsin Al-Amin Al-Aamili (1284-1371) wa Lebanon, katika kitabu kiitwacho *At.* Pia Imam Khomeini alitoa amri ya kuyakataza hayo, pia kiongozi wa sasa wa jamhuri ya kiislamu ya Iran, Seyyid Khamenei pia Seyyid fadhlu Llah, Marjaa maarufu

Marjaa maarufu Lebanon, kwamba kufanya hivi ni kuiudhi nafsi na kuharibu mandhari mbele ya wengine, lakini Marjaa wengine sehemu zingine wanatilia mkazo haya wanaona kuwa ni njia ya kuhuisha mnasaba wa Ashura na kuingiza anuani ya mahaba kwa Ahlu Bayt, na kuhisi walivyodhulumiwa. Na wapinagao wanasema kuwa kufanya hivyo si kuudhi nafsi tu ni haramu, lakini vile vile kuharibu nafsi au kiungo kimoja.

Ama mimi binafsi naelemea kwenye wenye fikra za kwanza, na naona kuwa maadam hakuna nassi (nukuu) iliyothibiti kwa mmoja wa maimamu wa Ahlu Bayt inayotaka kufanya mambo haya, bali ni mtindo unaokuwa katika jamii fulani katika kueleza mapenzi yao kwa Ahlu Bayt, na pia huwa yanageuka, mimi naona umuhimu wa kuweka picha nzuri ya madhehebu kama anavyosema Imam Jafar Sadiq (a.s.): "Muwe ni pambo kwetu, msiwe chukizo."Lakini kama nilivyosema mwanzo bado inabaki katika maoni, mimi siko katika daraja ya Marjaa na kutoa fatwa.

**Mwandishi:** Hapa nina swali la wazi juu ya kutoswali mshia na msunni, licha ya kuwa kuna fatwa ya Khomiein aliyoitoa akaondoa hilo, kwa kufaa kuswali nyuma ya maimamu wa *Haram* ya Makka na kwenye msikiti wa Mtume (s.a.w.w.)?

Naam, mashia wanaswali nyuma ya maimamu wa msikiti wa *Haram* wa Makka, na msikiti wa Mtume, na pia sehemu zingine. Nassi na fatwa zilizotolewa na Marjaa wa Shia zinaita mashia kushirikiana kaika Swala ya jamaa na ndugu zao wa kisunni, wakati wanapofika mahali panapokimiwa Swala. Ama mahali wanapokuwa wamemakinika, ni jambo la kawaida Swala zao

Zinakuwa nyuma ya imam katika ulamaa zao, kama ilivyo kwa masunni, wao mjini Qatif na vitongoji vyake, wana misikiti yao maalum na hawaswali na maimamu wa kishia.

Napenda kusema hapa kwamba mashia saa nyingine hupata matatizo wanaposwali kwenye msikiti wa Mtume mathalan, rai ya madhehebu ya Shia ni kutosihi kusujudu ila juu ya ardhi, au kilichomea juu ya ardhi, kisicholiwa, na kuvaliwa, na sehemu nyingi ya msikiti wa Mtume imetandikwa mazulia, wao wanalazinika kuweka udongo au kibao au karatasi wakisujudu juu yake, hili wengine hawaliwezi, hata hutokea tabu katika tofauti ya kimafungu katika mas-ala haya.

Na miongoni mwa matatizo wayapatayo mashia katika Swala ya jamaa na ndugu zao wa Sunni ni kwamba kuna baadhiya maimamu wa kisunni wanawatukana maimamu wa kishia katika khutba zao, na kuwataja kwa shirk upotevu na uzushi, je mtu atakubali kuswali nyuma ya mtu mwenye tuhuma kama hizo?

Ishatokea ujumbe wa kishia kutoka nchi za nje uliacha kuswali jamaa pale imam alipovama katika kutukana kama huku.Nataraji zitafanywa juhudi kuondoa matatizo kama haya ili iwe Swala ya jamaa ni mandhari ya umoja wa umma na kukusanya mambo yao inshaallah.

**Mwandishi:**Tukirudi Syria, mlirudi vipi, je unaweza kutufafanulia sababu na jinsi mlivyorudi Saudia?

Baada ya Iraq kuikalia Kuwait, na Saudia kusaidiana na majeshi ya ushirikiano ili kuilinda Saudia, na kuiweka huru Kuwait, jimbo letu liliingia kwenye hali mpya, na tukaona hatari inanyemelea nchi yetu, na hasa upande wa jimbo nyeti la mashariki, serikali ya Iraq ilijaribu kwa uwezo wake wote tuelekee kwenye msimamo wao,

Tupinge kuja kwa majeshi ya nje na tuzidishe upinzani wetu kwa serikali, ulikuwa kwenye upande huo,harakati nyingi za kiislamu za kisunni ziliwasiliana nasi zikitushujaisha kufanya hivyo, kwa sababa msimamo wao kiujumla ulikuwa kwenye upande huo, lakini tulichunguza mambo hayo kwa makini na kwa roho ya kupenda nchi yetu, tukaamua tujiunge na nchi yetu na tusimame pamoja nayo katika wakati huu wa shida nikatangaza kwenye taarifa iliyotolewa na wakala wa habari wa Reuter, kwamba sisi, pamoja na kuwa ni jamii yenye kupata matatizo, lakini hiyo haina maana sisi tusimame pamoja na adui Muiraq, tukakataa hadaa zote, na tukawaomba watu wetu katika jimbo la Mashariki kujitolea katika kuilinda nchi yetu na kuhifadhi usalama na utulivu katik hali hiyo nyeti.

Msimamo huu ulipokelewa vizuri na serikali ya mfalme wa Saudia (*Khaadimul haramain*) na kwa heshima, na kulikuwa na wasita kama vile balozi wa Saudia aliyekuwa Syria Ustadh Ahmad Al-Kahimi ambaye alifanya kazi nzuri, na Dk. Nasir Al-Manqur, balozi wa Saudia Uingereza, akiwa mjini London, huyu alikuwa kabla ya Dk. Ghazi Al-Qusaibi na baadhi ya ndugu wengine Marekani pia walikutana na balozi wa Saudia Amir Bandar bin Sultan, mawasiliano na mikutano ikawa mingi kutokana na hali ilivyokuwa ikiendelea nchini na heshima ya nchi juu ya msimamo tuliouchukua.

Mfalme akatuma mjumbe London akiwaita ndugu zetu kule kukutana na mfalme haraka ili kupata utulivu juu ya msimamo wa serikali na kushughulikia jambo hilo, wane wakaenda Jeddah, wakakutana na mfalme mnamo September 1993 (A.D.),

Pia wakakutana na waziri wa mambo ya ndani na mkuu wa jimbo la mashariki.

**Mwandishi:** Sijui ..ee Sheikh Hasan, kama kwamba baadhi ya habari zimetaja kazi ya Dk. Ghazi Al-Qusaibi, naye ni mwenye kuwapenda nyinyi, je unaweza kuliweka wazi jambo hili?

La, haikuwa kwa kutumia wasita, sisi tunaelewana sana na anayetumikia kupata umoja wa nchi, yeye alikulia Ahsaa na ameishi na mashia huko na Bahrain.

**Mwandishi:** Tukirudi kwenye wale ndugu zenu wane mliowatuma, nakuomba ututajie majina yao kwa sababu ya uthibi.

**Sheikh:** Ni Dk. Sheikh Tawfiq Seif, Mhandisi Jafar Shaayib, Ustadh Isa Al-Mudhii'l na Sheikh Sadiq Al-Jabrani. Wakarudi na mwelekeo mzuri na mfalme akamuru kuachiliwa huru wafungwa wa kishia kutokana na matukio yaliyopita, na akawasemehe waliokuwa nje warejee nyumbani kwa amani, na akaondoa vizuizi vya safari kwa aliyezuiwa.

Vilevile akaahdi kutatua matatizo yanayowapata wananchi mashia; hivi ndivyo harakati zetu za nje zilivyokwisha, alhamdu lillah, tukarudi nchini tukae kwenye kivuli chake.

**Mwandishi:** Licha ya kuwa katika sehemu yetu ya pili ya mahojiano yetu ulisema kuwa katika kipindi hiki tunachoishi, hatuna mashia wapingao, ila ni sauti tu zinazojitokeza huku na huko.

**Sheikh:** Kucheleweshwa kushughulikiwa mambo na kutatua matatizo ndiko kulikowakangaya baadhi ya ndugu zetu, huenda baadhi yao wakawa na shaka, hili kwa dola tu, bali hata kwa mustawa wa mashia, tunapambana na maswali kutoka kwa watu waliokuwa na tamaa ya kushughulikiwa, hali ya kuchelewa ikawakanganya. Katika hali kama hii kutakuwa na wenye kupinga, lakini twataraji ili kupunguza njia ya mwelekeo huu, ni muhimu sana kuyashughulikia matatizo ya watu hao, kwani wao ni wananchi na wana haki ya kuburudika na neema zilizoko katika nchi yao.

**Manifesto ya 'Washirika wa chini'**

Haifai sisi tukielekea mwisho wa mahojiano haya marefu nisitaje juu ya maombi yenu, mlitoa manifesto mwaka uliopita mkayiita '*Shurakaaun fil watan*' (Washirika nchini), humo mlitaja matakwa yenu mkiwa ni mashia, nini sababu ya hiyo, je jambo hilo lina uhusiano na anga ya kisiasa iliyoko nchini kwetu, ndipo huenda wengine wakasema huko ni kupatiliza fursa ya kisiasa na kijamii inayopitia nchi. Una maelezo gani hapo?

**Sheikh:** Hiyo haikuwa manifesto bali ulikuwa ni karatasi ya ujumbe aliyopelekewa mtawala na ujumbe wa mashia 18 kutoka Qatif, Ahsaa na Madina, ujumbe huo ulisainiwa na watu 450 tukitangaza mapenzi yetu kwa nchi, kusimamia pamoja na dola dhidi ya nguvu za kutoka nje, pia ujumbe ulikita juu ya umoja wa nchi, na kuungana watu na uongozi, na kwamba mashia ni sehemu tu

haiwezi kuwa kinyume na wengine, na wapatiwe nafasi katika nyanja zote kama wananchi wengine bila ya kuwabagua au kuwatenga, na mambo yao ya kimadhehebu yaheshimiwe.

Mapokezi ya mfalme (Mungu amhifadhi) yalikuwa mazuri mno, kiasi kwamba wajumbe wote waliridhika kuwa anashughulikia jambo hilo yeye mwenyewe, akawasifu mashia na mambo wanayozidishiwa kidini na kinchi, na akatuambia azma yake ya kuita mlingano wa kukutana kwa mdahalo wa nchi nzima.

Ama kusema kuwa kupeleka ujumbe huu ni kuitumia fursa, si sahihi, pande zote zimetoa manifesto na jumbe zao, lakini shia wakipeleka zao mbele ya viongozi wanaambiwa wameitumia fursa, Mungu ndiye mwenye kushtakiwa.

Samahani Sheikh, mbali na hisia za kijamii na kimkoa mpaka....tuhuma ziko kwa wote Sheikh Hasan... Je katika hili mko sawa na wengine?

**Sheikh:** Ikiwa ni hivyo basi nina haki niwatetee wote, ambapo haifai kukutuhumu, na nchi isumbuke kwa sauti za watu wake, wahusika nchini wanaona fahari kuwa na siasa ya mlango uliofunguliwa, basi na uwashujaishe wananchi kuzungumza na viongozi wao, katika hilo ndio mwanzo wa nasaha na kutowapa fursa maadui.

**Mwandishi:** Je una neno la mwisho katika kuhitimisha mahojiano haya?

**Sheikh:** Nakushukuru kwa kuitumia fursa hii ya mahojiano na wewe kujadiliana juu ya mambo haya yanayotuhusu waislamu ili tupambane na vipingaminizi, tukiwa ni wananchi, tunafanya bidii juu ya usalama na utulivu wa nchi yetu,na natumai mahojiano kama haya yasaidie kubadilishana mawazo kuliko bora zaidi,Na kuwe kutaka majadiliano kwetu ni kwa ajili ya kusaidiana katika mema na kumcha Mungu.

Na katika mahojiano yetu sikukusudia kuyafanya upya mambo ya kimadhehebu wala mjadala wa kitaifa wa siku nyingi, bali nilitaka kuiweka wazi picha ili watu wa upande mwingine wafahamu kuwa upande mwingine una maoni, hoja na dalili zao.

Nawaomba ndugu zangu walinganiaji na wasomi watililie umuhimu kushughulikia wa kukubaliana na mwafaka mpana kati ya madhehebu ya umma na watu wake, badala ya kujikita kwenye dondoo chache za hitilafu, watabaki pia badhi ya wenye kushadidia katika madhehebu mbali mbali, lakini wenye akili na walio kati kati wa pande zote wasiache uwanja kuchezewa na na nguvu za kushadidia, na wainue sauti zao na kuzidisha juhudi zao ili kuuokoa umma kutokana na hali nzito tunayoishi.

***

Sheikh Hassan bin Musa bin bin Sheikh Ridha Saffar,amezaliwa mnamo mwaka (1377 A.H.) huko mjini Qatif, Mkoa wa Mashariki, nchini Saudi Arabia. Alipohitimu kusoma katika Chuo cha Quran. Alijiunga na Madrasa ya msingi ya Zainul-Abidin, kisha akajiunga na Madrasa ya Kati ya Amin mjini Qatif, na hivyo kuanza kutoa khutba za kidini katika mwaka 1388 (A.H.) (1968 A.D.).............................................

Mnamo mwaka 1391 (A.H.) (1971 A.D.), alikwenda huko mjini Najaf, Iraq kwa ajili ya kuongeza elimu na baadaye alikwenda kuendelea zaidi kwenye Hawza ya Qum (Iran).

Kisha alijiunga na Madrasa ya Rasuulul-Akram nchini Kuwait, na hapo ndipo alipokuwa ni miongoni mwa viongozi wa mwamko wa kiislamu nchini humo............................

Sheikh Saffar amesimamia taasisi nyingi za kidini katika pande nyingi duniani ikiwemo Saudia, Oman, Syria, Iran na Marekani.........................................................................

Vilevile ameshiriki katika matangazo mengi kupitia kwenye idhaa na magazeti mengi duniani. Ameshiriki mikutano mingi ya kiislamu ikiwemo Mkutano wa vijana wa kiislamu Marekani, na mkutano wa Umoja wa kiislamu chini Iran, pia vikao juu ya fikra katika Saudia; pia mkutano wa mlingano wa ....... kuwa karibu baina ya madhehebu, nchini Bahrain......................................

Ametoa vitabu zaidi ya sabini na vimetarumiwa katika lugha mbali mbali za kigeni..............................................................

Sheikh huchukuliwa kama ni mmoja kati ya watu.......... wanaopenda kuzungumzia uhuru wa kuwapo kwa wingi wa kiitikadi, na juu ya uelewa wa uzalendo na pia kufikia kuwa na neno moja katika Uislamu.